Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 6 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Taarifa ya Mwaka ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo kwa Mwaka 2003/2004 *(The Annual Report of Activities and Audited Accounts of the University College of Lands and Architectural Studies (UCLAS) for the year 2003/2004).*

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, Tanzania kwa Mwaka 2002/2003 *(The Annual Report and Performance of the Higher Education Accreditation Council of Tanzania for the Year 2002/2003).*

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Mwaka wa fedha 2005/2006.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 206

Uboreshaji wa Uwezo wa Utendaji wa Madiwani

**MHE. EDSON M. HALINGA (K.n.y. MHE. JOHN L. MWAKIPESILE)** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa Serikai imedhihirisha kwamba Madiwani ni kiungo muhimu sana kati ya wananchi na Serikali na kwamba, wao ndio wasimamizi wakuu wa miradi ya maendeleo katika Kata zao na kwa kuwa, hivi sasa zaidi ya robo tatu ya fedha zote za Serikali zinapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya na kusimamiwa na Madiwani na kwa kuwa baada ya Serikali kutambua umuhimu wa Madiwani katika suala zima la maendeleo na utawala bora imejitahidi sana kuinua/kuboresha viwango vyao vya uwezo wa kusimamia shughuli mbalimbali katika mipango ya uboreshaji:-

(a) Je, Serikali inaweza kutazama upya posho na mafao ya madiwani ili yafanane na uzito wa majukumu yao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuwalipa mshahara watendaji wa vijiji na kuwaacha Madiwani hoi ni kosa ambalo halielezeki?

(c) Ili kuboresha zaidi utendaji kazi wa Madiwani. Je, Serikali haiwezi kuandaa mpango wa kuwakopesha pikipiki Madiwani kama vile wanavyokopeshwa Wabunge magari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua nafasi na umuhimu wa Waheshimiwa Madiwani kama viongozi wa kuchaguliwa wenye jukumu la usimamia majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa kutambua umuhimu huo na kwa kuzingatia uzito wa majukumu waliyo nayo Serikali imeamua kutazama upya posho na mafao ya Madiwani ili yafanane na uzito wa majukumu yao. Ili kutekeleza azma hiyo ya Serikali, Ofisi yangu imemteua Mtaalam Mshauri *(Consultant)* ambaye tayari ameanza kazi na ambaye atapita katika Halmashauri kukusanya maoni ya wadau mblimbali wakiwa ni pamoja na Madiwani. Aidha, Ofisi imeunda Kamati *(Reference Group)* ambayo itaratibu na kumsaidia mtaalam mshauri katika kufanikisha zoezi hilo. Kamati hiyo kama nilivyowahi kusema hapa Bungeni inaongozwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. Kamati hiyo imeshafanya vikao vyake viwili na cha tatu kitafanyika tarehe 13/7/2005 ambapo mtaalam mshauri *(Consultant)* atatpa taarifa yake. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kosa lolote linalotokana na watendaji wa vijiji kulipwa mishahara na Madiwani kupewa posho kwa sababu vyeo hivyo viwili havifanani. Ieleweke kuwa Mtendaji kuwa Mtendaji ni Mwajiriwa ambaye kwa mujibu wa Sheria za kazi anastahili kulipwa mshahara wakati Diwani kwa mujibu wa sheria zilizopo sasa ni kiongozi au *Civic Leader* ambaye siyo mtumishi. Aidha, kama nilivyosema katika jibu langu la (a) hapo juu, Serikali inatambua umuhimu wa Waheshimiwa Madiwani na ndiyo mana inapitia upya posho na mafao yao mengine kwa madhumuni ya kuyaboresha.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuwakopesha Madiwani pikipiki kwa hivi sasa kutokana na sababu kubwa mbili zifuatazo. Kwanza posho wanazopata kwa sasa haziwezi kutosheleza kulipa deni la pikipiki hata kama watakatwa posho yote ya mwezi kwa miaka yote mitano.Lakini pili kama nilivyosema wao kwa mujibu wa Sheria hivi sasa si watumishi wa Serikali ambao taratibu zinatoa fursa ya mikopo ya aina hiyo.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa hapa. Lakini naomba niulize maswali mawili madogo. Suala la kusema kwamba Madiwani wasikopeshwe magari au baiskeli au pikipiki haoni kwamba utendaji wa kazi ni mgumu sana hasa katika Kata ambazo zina vijiji vingi na wanashindwa kukabili matatizo na kufuatilia utekelezaji?

Pili, Serikali haioni kwamba hata Wenyeviti ambao wanapaswa kuwepo kazini wakati wote wasipolipwa kitu ni tatizo katika kufanikisha shughuli za utekelezaji na za maendeleo katika vijiji vyao Serikali inafikiri nini juu ya Wenyeviti wa Vijiji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya maeneo ambayo yanaongozwa na Madiwani ni makubwa na katika hali ya kawaida walitakiwa kuwa na vitendea kazi vya namna moja kuwasaidia kuweza kufanya kazi hizo vizuri. Lakini kama nilivyosema kwa utaratibu ulivyo sasa na kwa hali halisi ilivyo haitawezekana kumkopesha Mheshimiwa Diwani wala gari wala pikipiki kwa sababu posho ya elfu 30 tu na hii ilitokana na msingi wa kisheria ambao Wabunge mliona kwa wakati ule mwaka 82 kwamba wangeweza kufanya kazi zao kama viongozi au tunaita *Civic Leader* bila pengine kuhitaji mahitaji makubwa. Lakini mabadiliko yaliyotokea ndiyo yamepelekea uamuzi wa Serikali wa kufanya jambo hili lichambuliwe. Nafikiri tusubiri tuone matokeo wa hiyo Kamati na mapendekezo yake. *(Makofi)*

La pili, kuhusu Wenyeviti, Mheshimiwa Naibu Spika, tunahangaika kwanza na Madiwani hivi sasa. Hatujaweza kukidhi mahitaji yao kikamilifu. Lakini unaona sasa linaibuka suala la Wenyeviti nao kutazamwa ambao ni wengi sijui mara ngapi ukilinganisha na hata hao Madiwani. Kwa hiyo, mimi naomba sana tuendelee kutazama nafasi nyingine hizi katika ngazi za vijiji pamoja na mchango mkubwa walionao tuendelee kutazama kwamba ni nafasi ambazo kwa sehemu kubwa ni uongozi ambao unatokana na wananchi wenyewe katika maeneo yao sehemu kubwa itategemea namna watakavyokuwa wanajitolea hadi hapo uwezo wa Serikali utakapokuwa umeongezeka na

kuwa mkubwa kidogo. Lakini tunakubali na Serikali imekwishaamua hivyo kwamba asilimia 20 ambayo zamani ilikuwa inabaki vijijini hata baada ya kuwa tumeondoa ushuru na kodi mbalimbali tumedhamiria kurejesha ili angalau kwa kiasi fulani uweze kusaidia kukidhi haja hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba wanaandaa sasa wanafanya uchunguzi na kuona uwezekano wa kuweza kutazama hali ya baadaye ya maslahi ya Madiwani. Lakini kwa kuwa vile vile kitu kama baiskeli si kitu cha gharama sana haoni kama ingekuwa jambo la busara angalau kukubali Halmashauri hizo ziwakopeshe hata baiskeli ambayo haizidi elfu 70?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa ajili ya Madiwani ya baiskeli ni jambo linazungumzika na kwa kweli linaweza likafanyika katika ngazi ya Halmashauri. Kinachohitajika ni Halmashauri kuwa mdhamini kwa Madiwani hawa kwa ajili ya ukopeshaji wa baiskeli na nataka tu nimthibitishie Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwamba katika baadhi ya Halmashauri zilizopita walikwishafanya hivyo. Madiwani walikopa baiskeli wakadhaminiwa na zimelipwa kutokana na posho kwa kipindi walichokubaliana. *(Makofi)*

Na. 207

**Ardhi Kama Dhamana ya Kukopa**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha sera ya kuwamilikisha wananchi ardhi ili waweze kuitumia kama dhamana na hivyo kupata mikopo kutoka Benki:-

(a) Je, tangu sera hiyo ianze kutumika ni wananchi wangapi wamenufaika na mpango huo?

(b) Kwa kuwa mpango huo ni ukombozi kwa wananchi wa kipato cha chini lakini unakwenda taratibu sana.

Je, Serikali inatoa kauli gani ili kuharakisha mpango huo na wananchi wengi waweze kunufaika?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Bukombe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-0

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kutumika kwa Sera ya Taifa ya Ardhi, Sheria mpya za Ardhi na Maamuzi mengine ya Serikali hapa nchini, ardhi inatumika kama dhamana na kuwanufaisha wananchi moja kwa moja. Walionufaika ni wengi na

siyo rahisi kupata takwimu kamili kwa nchi nzima. Hata hivyo mifano michache ya walionufaika ni kama ifuatavyo:-

(i) Wananchi 1,131 waliowekeza rehani hati zao kati ya mwaka 2002/2005 walipata mikopo kutoka kwenye vyombo vya fedha.

(ii) Kati ya mwaka 1993 na 2005 jumla ya wananchi 4,304 waliokuwa wapangaji wa Shirika la Nyumba la Taifa waliouziwa nyumba hizo na kulipia kikamilifu, sasa wanazitumia hati miliki zao kuombea mikopo.

(iii) Jumla ya wananchi 4 kati ya wananchi 422 waliopewa hatimiliki za kimila katika Wilaya ya Mbozi Mkoani Mbeya wamekwisha kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha.

(iv) Jumla ya wananchi 85 kati ya wananchi 167,676 wanaoishi kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela waliohakikiwa na kuingizwa kwenye kompyuta Jijini Dar es Salaam wamepatiwa leseni za makazi. Hivi sasa wanatafuta mikopo katika vyombo vya fedha na wananchi wote ambao wana hatimiliki sasa wanaweza kutumia fursa hii ya kutumia hati hizo kama dhamana kwenda kwenye vyombo vya fedha kukopa fedha. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini Tanzania yaani (MKUKUTA) ambao unalenga kuzinufaisha Sekta zote ikiwemo sekta ya Ardhi. Hivyo, suala la kuifufua ardhi mfu kuwa rasilimali iliyo hai linatekelezwa kwa kasi nchini kote. Wizara yangu imeanza kutekeleza mkakati wa kurasimisha rasilimali na biashara Tanzania yaani (MKURABITA) kupitia utekelezaji wa Sera na Sheria za Ardhi. Mipango hiyo imefanyika kwa majaribio katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutambua nyumba katika maeneo yasiyopimwa na Mbeya Wilayani Mbozi kwa kupima vijiji na mashamba ya wananchi.

Kutokana na uzoefu huo, kwa sasa Serikali inajijengea uwezo Wizara yangu pamoja na Halmashauri zote za Miji na Wilaya kutekeleza miradi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi, kutambua miliki kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela na kutoa leseni za makazi na kupima vijiji na mashamba ya wanavijiji na kutoa hati miliki za kimila. Mipango hiyo itagharamiwa na Bajeti ya Serikali na wafadhili. Aidha, natoa wito kwa Halmashauri za Miji na wilaya kuzingatia katika Bajeti zao mipango ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi, upimaji wa viwanja na mashamba, upimaji wa vijiji na utambuzi wa maeneo yaliyojengwa kiholela ili kuwawezesha wananchi kutumia ardhi yao na majengo yao kama dhamana kuombea mikopo katika vyombo vya fedha. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa sera hii ni ukombozi kwa wananchi wetu na kwa kuwa zoezi hili limenufaisha wachache ukilinganisha na idadi ya Watanzania walio wengi. Je, ni lini zoezi hili litaendelea kuhudumia na kuenea nchi nzima?

Swali la pili, je, katika muundo huu hati ya kumiliki ardhi itakamilika kwa muda gani tofauti na sasa hati ya kumiliki ardhi inachukua hata mwaka nzima haijakamilika?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kusisitiza kama nilivyosema kwamba zoezi hili limekwishaanza na ni la nchi nzima. Halmashauri zote nchini zinatakiwa katika mipango yake kama nilivyosema lizingatie kwamba sasa hivi wananchi wana fursa ya kuweza kukopa kwenye vyombo vya fedha kwa kutumia hatimiliki zao.

Kuna wananchi wengi katika nchi hii katika Halmashauri zote ambao tayari wana hatimiliki na sasa hivi tunapima vijiji na wananchi vijijini wanapata hatimiliki za kimila nao pia wanaweza kutumia fursa hii. Kwa hiyo, sasa hivi ni zoezi la nchi nzima. Kwa hiyo, naendelea kutoa wito kama nitakavyoendelea kutoa wito tarehe 14 wakati wa hoja yangu kwamba sasa Halmashauri zote waweze kutumia fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge atakuwa amesoma hotuba zetu zilizopita hasa mwaka jana 2004 tulieleza kwa kirefu sana kuhusu suala hili la utoaji wa hati. Sasa hivi utoaji wa hati unashughulikiwa kwenye Halmashauri zetu huko huko na haichukui muda mrefu na kwa wale ambao wamepata vyeti pale Dar es Salaam siku hiyo hiyo unapopata barua ya toleo baada ya wiki moja hati yako inakuwa tayari. Kwa hiyo, sasa hivi hakuna ucheleweshaji wa utoaji hati. Iwe Wizarani au kwenye Halmashauri zetu, kama kuna matatizo mahali popote wanaweza wakatufahamisha ili tufuatilie kwa nini kuna tatizo la namna hiyo.

Na. 208

**Barabara Inayounganisha Wilaya za Mkoa wa Mtwara**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoani Mtwara ipo barabara inayounganisha Wilaya za Mtwara, Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala na Masasi ambayo ni barabara ya udongo; na kwa kuwa barabara hiyo ndiyo tegemeo la Mkoa kwa kupitishia mazao lakini ni mbovu na pia barabara toka Newala, Kitangari hadi Mtama, katika baadhi ya maeneo imejifunga:-

(a) Je, ni lini Serikali inakusudia kuifanyia matengenezo barabara ya Mtama ambayo inaunganishwa na Mkoa wa Lindi?

(b) Kwa kuwa katika barabara itokayo Mtwara hadi Masasi zimekuwa zikitokea ajali za kila mara kutokana na kuwa mbaya. Je, Serikali haioni kuwa iko haja sasa ya kuweka lami barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imekwishaanza kuchukua hatua za kuifanyia matengenezo barabara ya Newala-Kitangari-Mtama ili iweze kupitika wakati wote wa mwaka. Jumla ya kilometa 18 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa gharama ya shilingi 10.70 milioni. Aidha, jitihada zinaendelea katika kushughulikia kikamilifu sehemu zenye mchanga ambazo huwa zinasababisha barabara kujifunga. Kazi hizo zitaendelea tena katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Mtwara hadi Masasi kupitia Tandahimba na Newala ni tegemeo la wananchi wa Mkoa wa Mtwara kusafirisha mazao yao hususan zao la korosho kutoka Wilayani kwenda bandari ya Mtwara. Kwa kuzingatia ukweli huo, Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara *(TANROADS)* inatoa kipaumbele katika kuifanyia matengenezo ya kawaida na ya dharura na matengenezo ya sehemu korofi barabara hiyo ya Mtwara-Tandahimba-Newala-Masasi yenye urefu wa kilometa 211 kwa kutumia fedha toka kwenye mfuko wa barabara *(Road Fund)* zinazotolewa kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mtwara imefanya matengenezo yafuatayo kwenye barabara hiyo:-

(i) Jumla ya kilometa 157 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 115.

(ii) Jumla ya kilometa 6 kutoka Masasi Mjini hadi kijiji cha Chiwisi, zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 90.072. Aidha, matengenezo kwa kiwango cha changarawe yanaendelea kati ya Mbawala na Ngorongoro (km 4) kwa gharama ya shilingi milioni 66.923 na yatakamilika mwezi Agosti mwaka huu 2005.

(iii) Matengenezo kwa kiwango cha lami kwa jumla ya kilometa 5.6 katika mlima Nanyamba na mlima Namaleche yanaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 104 na yatakamilika mwezi Agosti, 2005. Aidha, awamu ya pili ya matengenezo hayo itakamilika mwaka 2005/2006 kwa gharama ya shilingi 311.931.

(iv) Matengenezo kwa kiwango cha lami katika jumla ya kilometa 3.5 kati ya Masasi mjini na Kijiji cha Chiwisi yanaendelea kwa gharama ya shilingi miliioni 270 na yatakamilika Septemba, 2005. Aidha, awamu ya pili ya matengenezo hayo inagharimu shilingi milioni 162.413 itakamilika katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa mitambo hususan ya lami Mkoani Mtwara unasababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hii. Kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Serikali kifedha, kwa sasa ni vigumu kuijenga barabara ya Mtwara-Tandahimba-Newala-

Masasi kilometa 211 yote kwa kiwango cha lami. Mkazo sasa hivi ni ujenzi wa barabara kuu zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kwa kiwango cha lami.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Kabla sijauliza swali napenda kupongeza Serikali kwa jitihada ya Wizara ambayo wameanza kuonyesha kutengeneza hiyo barabara ya Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Swali. Katika kutengeneza vipande vya mlima wa Nanyamba na mlima wa Namaleche, sawa na Naibu Waziri alivyosema. Mkandarasi yule ambaye amewekwa ameharibu lami na si sahihi ile lami. Je, Serikali hilo inajua na kama inajua, yule ambaye ameharibu taratibu zile amechukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya ukorofi wa mkandarasi huyo tumeipata na hii ni kwa sababu ya ukosefu wa mitambo ya lami na *TANROADS* wanachukua hatua sahihi ambazo huwa wanachukuliwa makandarasi wa namna hiyo.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa barabara hii ya Mtwara-Tandahimba-Newala inachongwa mara kwa mara na kufanya mto sasa wa kupita maji wakati wa masika. Serikali inajua na kwamba bila kuweka kwenye mpango wa *Mtwara Corridor* barabara hii watu wa Tandahimba na Newala hawatendewi haki kupata mradi wa barabara *Mtwara Corridor?*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajua matatizo ya barabara hii pamoja na nyingine ambazo ziko Mkoa wa Mtwara na ni mabarabara ambayo yanafika mpaka Masasi na katika mradi wa *Mtwara Corridor* barabara zingine zitatazamwa lakini barabara muhimu ni ile Mtwara-Masasi hadi *Mbambabay* ndiyo barabara ambayo inawekewa mkazo kwanza. Tukisema tuanze kupangua hii tukaanza kuweka barabara zingine *Mtwara Corridor* haitakwenda na haitakuwa kwa faida kwa wananchi wa Mtwara peke yao.

Kwa hiyo, naomba wananchi wa Mtwara wastahimili wakubali kwamba ipo haja ya kupanga na kuchagua kwanza. Kwa hiyo, tunapanga barabara ya Mtwara-*Mbambabay* kwanza.. *(Makofi)*

Na. 209

**Ununuzi wa Kivuko Kipya**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili(2,000,000,000/=) kwa ajili ya kununulia kivuko kipya cha Kigongo – Busisi, na

kwa kuwa kivuko kilichopo sasa kimechoka na mara nyingi huharibika na kuzimika kikiwa majini:-

(a) Je, ni lini kivuko hicho kipya kitakuwa tayari na kina ukubwa gani, uwezo gani wa kubeba magari na abiria wangapi kwa wakati mmoja kikilinganishwa na kile kilichopo sasa hivi?

(b) Kama kivuko hicho kitakuwa tayari. Je, Serikali itakuwa tayari kutenganisha magari yabebayo mizigo hatari ya mafuta ya petroli yavushwe na kivuko cha zamani na gari za abiria na mizigo ya kawaida yavushwe na kivuko kipya?

(c) Je, wafanyakazi wa kivuko watakuwa tayari kabla ya safari kuwaeleza abiria juu ya vyombo vya kujiokolea, namna vinavyofunguliwa na kutumiwa wakati wa hatari na kutoa onyo la kutovuta sigara na kadhalika na hali ilivyo sasa ambapo haya hayafanyiki?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kivuko cha Kigongo-Busisi kipo kwenye Barabara ya Usagara-Sengerema-Geita hadi Biharamulo. Kivuko hicho kinahudumia magari mengi yanayopeleka mafuta kwenye migodi na kwenye nchi jirani. Ni kutokana na ongezeko hilo la magari, Serikali katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2004/2005 ilianza kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kununulia kivuko kipya katika eneo hilo.

Kivuko kipya kitakuwa tayari katika kipindi cha miezi 14 kuanzia tarehe 10/5/2005 ambapo Serikali iliingia Mkataba na Mkandarasi anaitwa *Sinnautic* wa Uholanzi wa kuleta kivuko hicho. Kivuko kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 250 yaani magari madogo 40 na abiria 1,000 kwa wakati mmoja ukilinganisha na Kivuko cha *MV Sengerema* chenye uwezo wa kubeba tani 170 yaani magari 25 na watu 600 tu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kivuko hiki kuwasili, huduma ya kuvusha katika kivuko hicho itaboreshwa ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kutenganisha abiria na mizigo ya mafuta wakati wa kuvuka na hilo ndiyo lilikuwa lengo mojawapo la Serikali kununua kivuko kipya.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na utaratibu alioushauri Mheshimiwa Mbunge wa kutoa elimu ya usalama kwenye Kivuko cha Kigongo-Busisi pamoja na vivuko vyote nchini ili kuelimisha watumiaji wa vivuko jinsi ya kutumia vifaa vya kujiokolea pamoja na kutoa onyo kuwa wasivute sigara wakati wakiwa kwenye kivuko.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani kwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana juu ya swali hili. Lakini ninalo swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa ununuzi wa kivuko hiki cha Busisi-Kigongo utaambana na ujenzi wa barabara ya lami Usagara hadi Geita-Sengerema mpaka Bihalamulo hadi Bukoba na kwa kuwa katika ujenzi wa barabara ya Kibiti-Lindi katika daraja la Mkapa, Wizara ya Ujenzi imejenga vituo vya Polisi kwa ajili ya ulinzi wa daraja.

Je, Wizara ya Ujenzi haiwezi ikashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo inasema haina hela wakati wa kujenga barabara ya lami wajenge Vituo vya Polisi Busisi na Kigongo kwa ajili ya ulinzi wa kivuko na abiria na usalama wa vifaa vyote vinavyopita pale, kama walivyofanya Rufiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kumweleza Mheshimiwa Musalika, Kigongo kuna kituo cha polisi, na Busisi kuna kituo cha polisi. Kwa hiyo, hakuna sababu ya Wizara ya Ujenzi kujenga tena kituo cha polisi ambapo kituo cha polisi kipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ujenzi wa barabara ambao ni ya kutoka Usagara kwenda kuunganisha na Bukoba unaendelea na katika Bajeti ambayo mliipitisha hapa zimetengwa bilioni 10.9 ambazo zinahusika katika ujenzi wa barabara ya Usagara hadi Buzilayombo. Lakini pia katika mazungumzo yanayoendelea sasa hivi na *European Union (EU)* wamekubali kutoa fedha zingine ambazo zitajenga barabara ya lami kutoka Kisesa kuja Usagara ili iweze kuwa kiunganisho vizuri na *ferry* ambayo imenunuliwa kwa bilioni 3.7 ambayo katika Bajeti ya mwaka huu 2005 itaweza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nitoe ufafanuzi mdogo kuhusu usafiri wa kwenye *ferry*, saa nyingine ni vigumu sana kutenganisha watu na usafiri wowote unaotumia mafuta. Ndege inapotoka hapa Dar es Salaam kwenda Ulaya huwa imejaza mafuta. Kwa hiyo, huwezi ukatenganisha watu kwenye ndege ambayo inaendeshwa kwa mafuta. Vilevile hata kwenye *ferry* linaloendeshwa kwa mafuta. Kwa hiyo, itatokea siku moja, siku nyingine tutakuwa tunapakia watu pamoja na mizigo iliyopakiwa humo humo kwa sababu hili ni suala gumu la kuhakikisha kwamba mizigo tu isafiri peke yake na watu wasafiri peke yake kutokana na uwezo halisi wa Tanzania, lakini tutaendelea kulishughulikia hili.

Na. 210

**Usumbufu wa Kufuatilia Madai Hazina**

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kusa wastaafu na ndugu za Marehemu waliokuwa watumishi wa Serikali, bado wanaendelea kupata usumbufu mkubwa wa kufuatilia madai/stahili zao mbalimbali bila mafanikio:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kurekebisha hali hiyo kwa wale wanaoendelea kufuatilia madai yao?
(b) Je, ni nani hasa anayehusika ili wale wanaofuatilia madai yao waweze kumwona kwa urahisi?

(c) Je, itachukua muda gani kwa wastaafu au wafiwa kufanikiwa kupewa madai yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wazri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tarehe 23/6/2005 wakati najibu swali Na. 122 la Mheshimiwa Dr. Luoga, Wizara ya Fedha imewaagiza waajiri wote kuwasilisha majalada zenye kumbukumbu za wastaafu zilizokamilika, miezi sita kabla ya wahusika kustaafu ili waweze kuandaliwa mafao yao mapema na waweze kuyapata malipo husika mara tu wanapostaafu. Wanatakiwa pia wawasilishe kumbukumbu za watumishi waliofariki mara baada ya taratibu za mirathi kukamilika. Aidha ni jukumu la kila mstaafu mtarajiwa kuhakikisha ana kumbukumbu husika anapostaafu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali Na. 121 la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, wanaohusika na malipo ya mirathi ni Waajiri, Wizara ya Fedha na Mahakama Kuu. Kwa mikoani, baada ya kumbukumbu kukamilika malipo hupelekwa Hazina Ndogo za mikoa yote Tanzania Bara na kwa Zanzibar malipo yote hupelekwa Ofisi ya Wakfu Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama waajiri wote watatekeleza agizo la kuwasilisha kumbukumbu kwa wakati na bila mapungufu, basi wastaafu wote watalipwa mafao yao bila kuchelewa ndani miezi mitatu tangu jalada kufunguliwa Hazina na kupitishwa ukaguzi na kulipwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufumbuzi wa kudumu Serikali ilianzisha Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma ambao hukusanya nyaraka muhimu wakati mtumishi akiwa kazini. Malipo toka mfuko huu yameshaanza; hivyo hapo baadaye hapatakuwa na usumbufu tena kwa kuwa kumbukumbu zote zinazohitajika zitakuwepo.

Wizara ya Fedha itaandaa matangazo maalum kwenye vyombo vya habari ili watumishi, waajiri na umma kwa ujumla wajiandae kutopata usumbufu wanapodai malipo yao ya kustaafu. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu yake mazuri ya Naibu Waziri. Lakini hali tuliyonayo sasa hivi wanaoendelea kupata usumbufu ni hawa ambao sasa hivi wanahangaika, unavyosema kwamba utaratibu unapangwa inamaana hawa waajiriwe upya ili waupate huo utaratibu? Au wafe tena waweze kupata stahiki yao maana yake tatizo sasa hivi lipo.

Pili kwa nini tusitafute utaratibu wa kuweza kupanga labda kuunda Kamati ambayo itafuatilia kikamilifu matatizo yaliyoko hivi sasa, ili hawa waweze kupata jawabu la kuweza kupata pesa zao badala ya kufikiria tu tahadhari itakayochukuliwa watakaostaafu hapo baadaye. Tatizo tunalo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Kigwalilo kwa jinsi anavyoshughulikia matatizo ya wapiga kura wake pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lipo ni kweli lipo na Serikali inafanya kila njia kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondolewa kwa hawa ambao wamestaafu. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba tatizo ni kumbukumbu kutokukamilika. Kama kumbukumbu hazijakamilika Wizara ya Fedha haiwezi kufanya lolote mpaka kumbukumbu zikamilike, na ili kumbukumbu zikamilike ni waajiri ndio wanatakiwa kuzikamilisha hizo. Kwa hiyo, kama waajiri hawajaleta kumbukumbu ambazo zimekamilika, Wizara ya Fedha haiwezi kulipa. Kwa hiyo, hili ni jukumu la waajiri pamoja na waajiriwa.

Pili kuna tatizo la watu kugushi ama kufanya utapeli kwa kuchukua fedha za wastaafu kwa niaba ya. Kwa hiyo, mtu analipwa ambaye hahusiki na baadaye wanarudi Wizara ya Fedha kusema hawajalipwa. Kwa hiyo, Wizara ya Fedha inakuwa makini kuhakikisha kwamba wanaolipwa ni wale tu wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla tumejipanga kuhakikisha kwamba kero hii inamalizwa na Wizara ya Fedha kama utakavyoona ukipita hapo jengo la pensheni limeshakarabatiwa na waastafu wote wametengewa mahali pa kukaa sio kama ilivyokuwa zamani.

Lakini pia ndani ya Wizara ya Fedha tumejiandaa kwamba watumishi wote ambao wanashughulikiwa mafaili yao wanapewa namba, na wanaelekezwa ni mtumishi gani anashughulikia tatizo lao. Kwa hiyo, ndani ya Wizara ya Fedha na ndani ya Serikali tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba hili linatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba wastaafu wanaofuatilia pensheni zao Dar es Salaam, waanzie kwanza kwenye ofisi zetu za Hazina Ndogo mikoani kwa sababu wengine wanakuta *cheque* zimeshafika kwenye *Sub Treasury* kwenye hazina ndogo mikoani. Lakini wanakuja Dar es Salaam, waanzie kwanza Hazina Ndogo, kabla hawajaja Dar es Salaam Wizara ya Fedha ahsante.

**MHE. MARIAM J. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba pengine nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya suala zima la kumbukumbu za wastaafu. Mtumishi kafanya kazi Serikali zaidi ya miaka ishirini, thelathini na kumbukumbu hizo zilikuwepo toka huko awali. Sasa kama kulikuwa na upungufu wa kumbukumbu za mtumishi kwanini zingoje kuja kutafutwa wakati amestaafu zisitafutwe mapema?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililoko la msingi kabisa, ni uwekaji wa kumbukumbu katika mafaili ya watumishi. Kazi ya kuweka kumbukumbu ni maofisa Utumishi wa popote pale wanapofanya kazi. Maofisa Utumishi ndio wanaotakiwa kuhakikisha kwamba *records* katika *file* la kila mtumishi ziko na kuna kumbukumbu nyingine zaidi sio moja tu ambazo zinatakiwa ziwe kwenye *file* hilo siku ile akistaafu. Kwa bahati mbaya sana kinachotokea tuchukue mfano wa mtu aliyekuwa mwalimu, baada ya muda akaingia akawa Katibu wa Wilaya, baada ya muda akawa Mkuu wa Wilaya, baada ya muda akawa Mbunge. Mtu huyu inatakiwa *file* lake lionyeshe miondoko yake yote hiyo mpaka pale alipostaafia.

Lakini kwa bahati mbaya sana mambo haya yanavyofanyika unakuta labda *records* ziliyoko ni ile akiwa mwalimu hapa katikati zote hizi nyingine haziko. Kwa hiyo, sasa *file* linakuja hazina halina hizo *records* nyingine lakini yeye anaweza akawa anadai miaka ishirini, kumbe kwenye *file* lake ni miaka mitano tuinayojiontyesha. Kwa hiyo, ukimlipa miaka mitano hatakubali mpaka umlipe ishirini ambayo ndio haki yake.

Hili ndilo tatizo la msingi la watu kutofuatilia *records* za mtumishi toka alivyoondoka kutoka mwajiri mmoja mpaka mwingine mpaka akaishia pale anapodai mafao yake. Sasa hili ndilo tumesema kwamba linakwisha kwa sababu tumeanza utaratibu mpya ambao unatumia kompyuta, lakini mwishowe ni maafisa Utumishi na mimi naomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie sana mnapopata wapiga kura wenu wakiwalalamikia juu ya mambo haya msiharakishe kuja Hazina. Kule sisi hatuna kitu, hatuna hata hilo *file* la huyo mtu hatuna. *File* linakuja tu pale anapotaka kulipwa na sisi tunaangalia kumbukumbu (a) (b) na ( c) zipo, *yes* lipa. Kumbukumbu (a) (b) na (c) zipo hapana baibai. Ndio utaratibu ulioko Hazina hatulipi bila kumbukumbu.

Na. 211

**Upungufu wa Walimu**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kwa dhati kuimarisha elimu ya Sekondari, kwa kufuatana na mpango wa MMES:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na upungufu wa walimu kwa nchi nzima?

(b) Ili kusiwe na uhaba wa walimu katika baadhi ya maeneo yenye upungufu wa walimu kama Mikoa ya pembezoni. Je, isingekuwa jambo zuri kwa Serikali kuanzisha vyuo vya walimu katika Kanda hizo ili kusiwe na tatizo tena la walimu?

(c) Kwa kuwa, walimu watakao fikia umri wa kustaafu na bado wana uwezo wa kufundisha shule za Sekondari. Je, kwa nini wasitumike kufundisha sekondari zenye upungufu wa walimu, kwa mkataba maalum?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali Na. 6 la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbuge wa Moshi Vijijini, katika mkutano huu wa ishirini kuwa, katika kutekeleza MMES 2004/2005 Serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa walimu katika shule za sekondari nchini ikiwa ni pamoja na:-

- Kuajiri walimu wote wenye Stashahada na Shahada ya Ualimu waliohitimu Mafunzo ya Ualimu miaka ya nyuma ambao walikuwa hawana ajira.

- Kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo ili kuchukua walimu tarajali wengi zaidi.

- Kuajiri waliofaulu vizuri kidato cha sita na wahitimu wa Chuo Kikuu wasio na vyeti vya Ualimu ambao watapatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mbinu za kufundisha. Hivi sasa kuna jumla ya walimu tarajali wa aina hiyo 374 wanaopatiwa mafunzo hayo katika Chuo cha Ualimu cha Morogoro na Butimba.

- Kubadilisha Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na shule ya Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu vya Elimu Vishiriki vya Chuo Kuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Ualimu cha Mtwara kuwa Chuo cha Elimu Ambata cha Chuo Kikuu Dar es Salaam, vitakavyotoa Elimu ya Ualimu kwa ajili ya shule za sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upungufu wa walimu katika baadhi ya maeneo halitokani na kutokuwepo Vyuo vya Ualimu katika maeneo hayo. Tatizo ni walimu wanaopangwa kutoripoti kabisa au kuripoti na kuondoka. Hata wale wanaotoka katika maeneo hayo hayo.Kutokuripoti kwa walimu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya ukosefu wa Nyumba za walimu zinazowafaa kuishi. Hata hivyo Wizara inaandaa mkakati wa Maendeleo ya Elimu ya Ualimu ambao utatilia maanani kukua kwa Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuongeza Vyuo vya Ualimu vingine.

(c)Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Ajira ya Mkataba kwa watumishi waliostaafu kwa umri au kuondolewa kazini haupo isipokuwa kwa kibali maalum. Kwa mujibu wa

kanuni ya Utumishi wa Umma kifungu 17 (3) ya mwaka 2003 mwenye mamalaka ya kutoa kibali hicho ni mkuu wa Utumishi wa Umma ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendesha zoezi la kubaini walimu wanaostaafu hivi karibuni ambao watapenda kuajiriwa kwa mkataba kwa lengo la kufanya mazungumzo na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuangalia uwezekano wa kupata kibali cha ajira kwa walimu hao kwa mkataba kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Sumbawanga, tunacho chuo cha Walimu ambacho kinafanya kazi nzuri sana kuwafundisha vijana wetu wa ngazi ya vyeti.

(i)Je, Waziri atakubaliana nami ya kwamba ili kupunguza kiu ambayo inaendelea kutokea hasa katika shule zetu za Sekondari ni vizuri mkafikiria uwezekano wa kukiongezea hadhi kidogo chuo hiki ili kiweze kutoa vijana wa *Diploma?*

(ii)Je, Wizara inakubaliana nami ili kupunguza gharama za kuwasafirisha walimu kutoka kona moja hadi nyingine ya nchi, kutoka Mtwara mpaka Bukoba, kutoka Musoma mpaka Sumbawanga ambayo inakuwa ni gharama kubwa. kwa Serikali. Je, isingeweza kuonekana njia nzuri ya kuhakikisha kwamba walimu wanapagiwa maeneo ambayo ni rahisi hata wao kwenda likizo kuliko mtu akatoka kona moja hadi nyingine ili kupunguza gharama ya Serikali, lakini pia kupunguza bughudha ya walimu wenyewe wahusika?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusu kuongeza hadhi ya Chuo cha Ualimu cha Sumbawanga, ninachoweza kusema tu kama nilivyosema katika hotuba ya Bajeti kwamba sasa hivi tunalo zoezi la kuvitizama upya na kupanga vipi viwe vya *Diploma* na vipi viwe vya ngazi ya cheti. Kwa hiyo, mawazo anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge yatazingatiwa katika mchakato huo. Swali la pili l a kupunguza gharama ni kweli kwamba katika miaka ya nyuma tulikuwa na sera inayosema lazima tuwachanganye wanafunzi wakifika ngazi fulani ya elimu. Ili wazoeane waishi pamoja kwa hiyo suala la gharama halikuwa linafikiriwa sana ilikuwa inachukuliwa tu kwamba watoto wa mikoa mbalimbali makabila mbalimbali ni afadhali wachanganyike katika ngazi ya elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na kupanda kwa bei za mafuta tangu kuanzishwa *OPEC* jambo hili kwa kweli inabidi tulizingatie zaidi kuendesha mambo yetu kwa kujali gharama na isitoshe ukweli ni kwamba Watanzania sasa hivi wamekwisha kuchanganyika vya kutoisha. Mwenyekiti wa CCM pale Iringa Mjini ni Ndugu Mushi, ndiyo Mwenyekiti wa CCM kule Iringa. *Meyor* wa Morogoro ni Ndugu Kayenzi, ni mpiga kura wangu anatoka kijiji cha Kitelewasi katika jimbo langu la uchaguzi. Kwa hiyo, ni ukweli kabisa kwamba sasa suala la kusema tuwachanganye Watanzania vijana shuleni halina msingi mkubwa kwa sasa. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa kwamba wakati umefika tupange vyuo vyetu upya na mkakati ambao Wizara yangu unautumia ni kujaribu kutoa elimu kwa vijana

wetu kwa kaangalia zile kanda nane za elimu, ndani ya kanda tuwe na shule za kutosha mpaka *A-level* ndani ya kanda. Ili gharama za usafiri zisiwe kubwa mno na utaratibu huu tunaweza kuufikisha mpaka kwenye vyuo, naomba Mheshimiwa Kimiti atupe muda tu jambo hili liko katika mchakato.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba niulize swali dogo tu kwa Waziri. Ninachojua ni kwamba tulipokuwa tunajifunza ualimu na kazi zingine zote huwa kuna mkataba kwamba utapangwa mahali popote kama mwalimu na unakubali kwamba niko tayari kufanya kazi mahali popote. Sasa mtindo uliozuka sasa hivi ni kwamba walimu wanaopangwa wanakataa kwenda maeneo fulani, wanakataa shule fulani. Sasa nataka nimwulize Waziri huo utaratibu ambao tumejiwekea wa mkataba siku hizi umefutwa kwa sababu haiwezekani mwalimu anakwenda anakotaka na Wizara inafanya nini sasa kama mwalimu hataki kwenda mahali. Wizara inafanya nini na shule zingine zibaki bila walimu zijae za mjini tu, za porini zisijae walimu? Hii ni utaratibu gani tunataka Waziri atuambie hapa.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, anavyosema ni kweli kabisa kwamba mtumishi wa Serikali akiwemo mwalimu anatakiwa aende popote ambapo amepangiwa kufanya kazi na Serikali iliyomwajiri. Hiyo ni kweli kabisa na ndivyo ilivyo na napenda nirudie kauli niliyoisema hapa Bungeni juzi nilipokuwa najibu swali, sikumbuki la Mheshimiwa nani, niliposema kwamba wale walimu waliopangwa katika shule ambako hawakwenda tulipanga walimu tisa amekwenda mmoja tu, kwamba nimetoa maagizo kwamba wachukuliwe hatua ya kinidhamu pamoja na kujieleza kwanini wasifukuzwe kazi na ualimu.

Nilitumia maneno hayo mawili kwa makusudi kabisa, kuna kufukuzwa kazi na kufukuzwa ualimu, ieleweke kwamba baadhi ya hawa walimu wakipangiwa maeneo ambayo wanakuta wanaona maisha ni magumu hakuna nyumba za walimu, kwanza hawaripoti na pili wanajiunga na shule zisizo za Serikali. Kwa hiyo, wanakuwa wametoka Serikali kwa hiyo kusema utamfukuza kazi humpati, lakini nimesema tunaweza kuwafukuza na ualimu. Kwa sababu kila mwalimu amesajiriwa kwenye daftari kwamba yeye ni mwalimu, na akifukuzwa ualimu hawezi kufundisha katika shule yoyote hapa nchini. Kwa hiyo, napenda kurudia kwamba kuanzia sasa kutokana na mfumuko wa shule katika mpango huu wa MMES tumejenga shule nyingine katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi. Lakini kwa sababu kuna binadamu wanaishi kule na si sungura, lazima walimu waende kufundisha. Kwa hiyo, kuanzia sasa nitaweka mkazo mkubwa sana na kuchukua hatua kali kwa mwalimu ambaye atapangiwa mahali asiende kuripoti pale alipopangiwa. (*Makofi*)

Na. 212

**Madai ya Walimu wa Shule za Sekondari**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, walimu za Shule za Sekondari wanayo malimbikizo ya madai mbalimbali kama ilivyo kwa walimu wa shule za msingi na kwa kuwa, Serikali imehakiki na kuanza kulipa madai ya aina hiyo kwa walimu wa shule za msingi:-

(a) Je, Serikali italipa malimbikizo hayo ya walimu wa Shule za Sekondari?

(b) Kwa kuwa, wapo pia baadhi ya walimu wa shule za msingi ambao madai yao yamekataliwa kutokana na kupotea kwa risiti zao baada ya kukaa kwenye majalada husika kwa kipindi kirefu. Je, serikali inawasaidiaje hao ili waweze kupata haki zao?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, madai mbalimbali ya walimu yataendelea kuwepo kwa sababu yanatokana na mambo ya kikazi. Serikali itaendelea kulipa madai hayo kadri Bajeti inavyoruhusu. Hadi kufikia Juni 2005 madai ya walimu na wafanyakazi wasio walimu katika Idara ya Sekondari yalikuwa yamefikia shilingi 1,640,939,751.00. Kiasi cha shilingi 943,727,228.00 zimelipwa na kiasi ambacho hakijalipwa kwa hivi sasa ni shilingi 697,212,523.00.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mshahara wa Walimu wa shule za Msingi haulipwi kupitia Fungu la 46 la Wizara yangu, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuelekeza swali lake kwa Wizara husika, nina hakika huko atapewa maelezo yaliyo sahihi.

**MHE. DIANO M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na mimi kuchangia jana kwenye wizara yake lakini bado hakunipa jibu la kukidhi haja ya walimu kuhusu tatizo hili. Madai ninayoyasema mimi ni yale ambayo ya muda mrefu wala siyo madai mapya. Je, Serikali kwa nini haitoi tamko kwamba malimbikizo ya madai ya walimu shule za Sekondari, wakaguzi wa shule, walimu wa vyuo itamkwe ni lini *time frame* itajwe hapa walimu wasikie, haya madeni mapya yataendelea. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza kama amenisikiliza kwa makini tumeyapunguza kutoka bilioni 1.6 mpaka 697,000 hapo naomba aelewe kwamba ni bilioni nzima moja imekwishakulipwa. Pia katika jibu langu hapa nimesema kwamba haiwezekani kabisa tukawa hatuna madai yaani tukawa kwenye *zero* kwa sababu ya hali halisi. Walimu waliko katika shule zetu nchi nzima madai yao yafike wizarani yahakikiwe yapelekwe Hazina mengine yanayohusu mishahara na mengine pale pale wizarani kwangu tuyalipe lazima kiwango fulani kitakuwa bado kipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Diana Chilolo, alivyochangia kwa uchungu mkubwa sana jana na kwa kweli sikupata nafasi tu ya kuweza kujibu vizuri zaidi kwa sababu ya muda. Alisema tungeunda tume tusitumie mafaili. Lakini jambo hili kwa namna lilivyo na tunavyolisimamia hatuoni sababu ya kuunda tume yoyote ya pale pale Wizarani. Kawaida wizara haijiundii tume, wizara tunashughulikia mambo yanavyotakiwa kusimamiwa ndani ya utaratibu. Lakini pale linapoonekana kuna jambo halikufanyika vizuri linahitaji hatua maalum ndipo ambapo tume inaundwa. Kwa mfano tume ile iliyoundwa kwa ajili ya walimu wa shule za msingi haikuundwa na Wizara iliundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimekuwa nikipata *pressure* kwamba niunde Tume, napenda kufafanua siyo utaratibu kwa Waziri kujiundia tume mwenyewe, sisi tunasimamia ndani ya utaratibu.

Mwisho napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa sababu ana uchungu mkubwa sana wa maslahi ya walimu katika hilo mimi niko pamoja naye kabisa na namshukuru sana kwa ufuatiliaji wake unaonisaidia mimi kuhimiza utekelezaji ndani ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Na. 213

**Usimamizi wa Uchumi wa Soko kwa Mazao ya Wakulima**

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI (K.n.y. RAPHAEL MLOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sera ya Uchumi wa Soko kuruhusu ununuzi binafsi wa mazao asilia ulianza mapema kwenye miaka ya 1990 pasipo maandalizi mahususi, kanuni na taratibu za kusimamia Sera hizo; na kwa kuwa ununuzi huo mara nyingi umeathiri maslahi ya wakulima wa mazao hayo kama mapunjo ya bei, kuvurugika kwa taratibu za upatikanaji na usambazaji wa Pembejeo za mazao; hasa kwa Sekta ya Pamba ambapo athari hizo zimekuwa kubwa zaidi katika msimu wa ununuzi wa mazao wa 2004/2005 kwa sababu wanunuzi binafsi waliwakopa wakulima wa Pamba na kwamba, wameendelea kukaidi maagizo ya Serikali ya kurekebisha kero hizo.

Je Serikali itaandaa lini mkakati mahsusi *(Comprehensive Strategy)* wa kusimamia uendeshaji wa sera za uchumi wa soko, hususan kusimamia masoko ya mazao asilia kwani sheria na taratibu zilizopo hazitatui matatizo hayo ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Soko huru kuhusu ununuzi wa mazao asilia ulikuwa unasimamiwa na Sheria ya mwaka 1984 iliyoanzisha Bodi mbalimbali za Mazao na kama ilivyorekebishwa na Bunge lako Tukufu mwanzoni mwa miaka ya 1990. *(Makofi)*

Katika marekebisho hayo ya sheria ambayo ilikusudia kukidhi haja ya mfumo wa soko huru kila Bodi ya zao ilipata sheria yake ya kuiwezesha kusimamia uzalishaji, usindikaji na uuzaji wa zao lililopo chini yake. Hivyo dhana ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Sera ya uchumi wa Soko kuhusu ununuzi wa mazao ilianza bila maandalizi mahususi ya sheria, kanuni na taratibu za kusimamia sera hiyo si sahihi.

Hata hivyo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hapakufanyika maandalizi ya kutosha kwa wanunuzi wa ndani, hususan Vyama vya Ushirika kwa kuwawezesha kupata mitaji isiyo na vikwazo na misururu ya gharama nyingi ya kununulia mazao ili waweze kuwa na ushindani wa haki baina yao na wanunuzi wakubwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Sera ya mfumo wa uchumi wa soko huru unaoruhusu ushirika wa wanunuzi binafsi katika biashara ya mazao asilia umekumbwa na matatizo mengi. Matatizo haya, kwa kiwango kikubwa, yanatokana na mfumo dhaifu wa usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu za ununuzi.

Baada ya Serikali kubaini udhaifu huu, Serikali iliamua kuandaa Sera ya Masoko ya Mazao ya kilimo. Maandalizi ya Sera hii, ambayo yameshirikisha wadau mbalimbali, yapo katika taratibu za kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri ili ipitishwe na kuanza kutumika. *(Makofi)*

Moja ya vipengele muhimu katika Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo, kinaeleza juu ya kuboresha muundo wa taasisi, kanuni na sheria za masoko ya mazao ya kilimo. Sambamba na maandalizi ya sera, Serikali itapitia upya sheria, kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao yote ya kilimo, ikiwa ni pamoja na yale asilia ili kuondoa upungufu uliopo na hivyo kuziboresha ili ziweze kufanya kazi kikamilifu katika mfumo wa sasa wa soko. Aidha, Serikali itaandaa mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo, ambao utajumuisha pia programu ya utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini yake. Mkakati huo utahusu pia masuala ya usimamizi wa masoko ya mazao asilia yanayotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika swali.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Hivi soko huria tangu limeanzishwa katika miaka ya 90 mpaka sasa hivi na wakulima wanalalamika kuhusu kupunjwa mazao yao, pamoja na bei kuwa chini na ushindani wa ununuzi hakuna na vyama vya msingi vimetupwa kabisa, kwa sababu havina uwezo wa kuweza kuchukua fedha za kununulia mazao. Hivi Serikali imekaa pembeni inaangalia Wananchi wake wakidhulumiwa; hivi maana yake nini? Maana yake ni kwamba, kuwaruhusu hawa watu waendelee kuwadhulumu wakulima na Serikali ipo au imekwenda *leave? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali haijaenda likizo hata siku moja na haitaweza kwenda likizo hata siku. Serikali inafanya kazi yake kwa utaratibu wa kutekeleza majukumu yake kwa kuwahimiza wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niseme kwamba, katika kujibu swali la msingi hapa, nimeeleza hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na Serikali, ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria, kanuni na taratibu za kusimamia ununuzi wa mazao chini ya mfumo wa soko huru. Nilichoeleza hapa ni kwamba, tatizo lililopo ni usimamizi hafifu wa hizi taratibu zilizopo na ndio maana hivi sasa tumeamua kuanzisha Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo, ambayo itasimamia taratibu hizi kwa ukamilifu. Hivyo basi, si sahihi kusema kwamba, Serikali imekaa pembeni, kwa sababu katika hatua mbalimbali tunazozifanya, tunahimiza wakulima wajiunge katika Vyama vya Ushirika ili waweze kupambana na ushindani wa wanunuzi binafsi, ambao Mheshimiwa Mbunge anadai kwamba wanawanyonya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali haijaenda likizo na inafanya kazi yake kwa utaratibu. *(Makofi)*

Na. 214

**Madai ya Fedha za Mauzo ya Kahawa**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA (k.n.y. MHE. DR. TALALA B. MBISE)** aliuliza:-

(a) Je, wakulima wa zao la kahawa wanadai kiasi gani cha fedha kutokana na mauzo kupitia Vyama vya Ushirika; na kati ya madai hayo ni kiasi gani kinatokana na makato yaliyowekwa kwenye amana ambazo mpaka sasa wakulima wana vitabu vyake na ni kiasi gani kilikuwa ni malipo ya kahawa iliyouzwa lakini wakulima hawakulipwa?

(b) Je, Serikali iko tayari kusaidia kulipa deni hilo la wakulima wa kahawa na ni lini italipa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa taarifa tunazozipata kutoka katika Vyama vya Ushirika, wakulima wa kahawa waliouza kahawa yao kupitia Vyama vya Ushirika katika maeneo mbalimbali nchini hadi mwishoni mwa msimu wa 2004/2005, hawadai fedha zozote za mauzo ya kahawa. Hii ni pamoja na wakulima wa eneo analotokea Mheshimiwa Talala Mbise.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakulima wa kahawa waliouza kahawa yao kupitia Vyama vya Msingi 25, ambavyo ni Wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika Arusha *(ACU),* hawadai fedha zozote zilizotokana na mauzo ya kahawa yao kupitia vyama hivyo. Hii ni kwa sababu wakulima wote walikuwa wanalipwa malipo yao ya awali mara tu baada ya Vyama vyao vya Msingi, kukusanya kahawa yao na kuiwasilisha kiwandani kwa utaratibu ambao uliwekwa na wakulima wenyewe. Malipo ya pili kwa wakulima, yamekuwa yakilipwa kila mara inapotokea kuwa hesabu ya jumla ya mauzo ya kahawa ya Chama Kikuu cha Ushirika Arusha, inaonesha faida. Endapo hesabu hiyo itaonesha hasara, wakulima huwa hawalipwi malipo ya pili hata wale ambao vyama vyao vya msingi vinaonesha kupata faida. Hali hii ilitokea katika msimu wa 1995/96, ambapo *ACU* ilipata hasara ya shilingi 241.4 milioni katika hesabu yake ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingine ambazo wakulima wangepaswa kulipwa kutoka *ACU* ni zile walizohifadhi katika Mfuko Maalum ulioundwa mwaka 1989/90. Fedha hizo kiasi cha shilingi 675,896,278/= zilipatikana kutokana na makato katika mauzo ya kila mwanachama aliyeuza kahawa yake kupitia kwenye Chama cha Ushirika ili zitumike kwa namna watakavyoamua. Kwa mfano, katika mwaka 1995/96, jumla ya shilingi 287,078,416/= zilitumika kuwalipa wakulima malipo yao ya awali. Shilingi 251,170,528/= zilitumika kuwakopesha wakulima pembejeo lakini hawakuzirejesha na shilingi 134,574,392/= zilitumika katika uendeshaji wa Chama Kikuu cha Ushirika. Hadi sasa mfuko huo una salio la shilingi 46,371,826/= tu. Jitihada za Vyama Msingi kudai fedha za pembejeo, hazijaleta mafanikio yoyote. Aidha, katika Mkutano Mkuu wa *ACU* wa Aprili, 2005 wanachama waliamua kwamba, suala hili lirudishwe katika vyama vyao vya msingi ili uamuzi wa mwisho kuhusu fedha hizi upatikane.

(b) Mheshimiwa Spika, hatma ya fedha zilizotumika kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya swali hili, ambazo ndizo zinazoonekana kuwa madeni kwa wakulima, zipo katika mamlaka ya wanachama na wakulima wenyewe, kwa sababu wao ndio waliochanga na wao ndio waliozitumia. Serikali haina uwezo wa kuwafidia fedha hizo ambazo walizitumia kwa ridhaa na kwa manufaa yao wao wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Sasa nina tangazo moja tu hapa. Leo kutakuwa na sherehe ya kufungua Soko la Kimataifa kule Kibaigwa, nasikia kuna baadhi yetu wamealikwa, kwa hiyo, kwa wale walioalikwa wanaweza kuelekea huko. Lakini siamini kama ni Bunge zima, nadhani ni wachache, lazima shughuli za hapa ziendelee na jioni tutapitisha Bajeti, kwa hiyo, wawahi mapema.

Baada ya tangazo hilo sasa nafikiri hakuna tangazo lingine tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 -

**Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu**

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Aidha, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu na marafiki katika kuwafariji na kuwapa salamu za rambirambi familia, ndugu na wapiga kura wa Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum - Mkoa wa Rukwa. Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amina.*

Vilevile ninapenda kutoa salamu za rambirambi na kuwapa pole ndugu na Wananchi wa Majimbo yaliyofiwa na Wabunge wao katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005. Wabunge waliofariki ni Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rahaleo, Marehemu Mheshimiwa Kapteni Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki na Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, *amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kumpongeza, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze (CCM), kwa kuchaguliwa kwake kuwa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Aidha, ningependa kumpongeza Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2005. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wagombea Urais walioteuliwa na watakaoteuliwa kutoka Kambi ya Upinzani. Wote ninawatakia mafanikio katika uteuzi wao na Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu kwa kipindi kilichopita na ambao wametuwezesha kupanga mipango ya mwaka 2005/2006 na kuboresha hoja zetu ambazo tunaziwasilisha katika hotuba hii. Aidha, natoa shukrani kwa Wananchi wote wa Tanzania, kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Katibu Mkuu wangu, Bibi Ruth H. Mollel, Watumishi wa Wizara yangu, pamoja na taasisi na mashirika mbalimbali ya ndani na nje, kwa misaada na ushauri wao, bila kumsahau Mheshimiwa Benedicto Mutarchoka Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika

kuiboresha hoja hii. Kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, kwa uchambuzi wa kina na ushauri wao. *(Makofi)*

Mwisho, ningependa kuelekeza shukrani zangu kwa Wananchi wote hususan wa Jimbo langu la Maswa, ambao leo wamewakilishwa na kikundi hicho tunachokiona. Kuna Bwana Charles Bukoye, Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Maswa, Bwana Hinda Mwaniyuki, kuna Mkuu wa Wilaya, Bwana Jowika au Kasunga, pamoja na Maafisa Elimu waliokuja nao na Maafisa Kilimo, wako pale wote ninawashukuru kwa kunienzi na kunifikisha hapa nilipo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile shukrani zangu nitazielekeza kwa familia yangu, ambayo nayo imenienzi na kuweza kunifikisha hapa. Imewakilishwa leo na Binti yangu, Leticia na Mjukuu wangu, Getrude. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kikao hiki na baada ya Rais kulivunja Bunge lako Tukufu, nitakuwa nimetimiza takriban miaka 25 mfululizo kama Mbunge. Naelekeza shukrani zangu kwa Wananchi wa Jimbo langu la Maswa, kwa kunienzi na kunitunuku heshima ya kuwatumikia kama Mbunge wao kwa takriban miaka 20 mfululizo. Pia Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kwa miaka mitano kama Mbunge wa Taifa kutoka Mkoa wa Shinyanga, jumla miaka 25 ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu, ningependa kuchukua fursa hii, kuwaomba waniruhusu sasa ombi langu la kustaafu Ubunge wa Jimbo la Maswa, kama nilivyowaomba tangu mwaka 2000 mara tu baada ya kunichagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pokea pongezi zangu maalum, kwa niaba ya Spika, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwa uongozi bora, wa mfano na utumishi wa kutukuka katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pokea vilevile salamu zangu za pongezi kwa kumudu vema kiti hicho pindi unapokikalia. Napenda vilevile kutoa shukrani zangu na pongezi kwa Wenyeviti wetu, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwa uongozi wao mzuri katika Bunge hili. Kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nasema ahsante sana kwa ushirikiano wenu. Wale mtakaogombea tena nafasi zenu, nawatakieni kila la kheri na mafanikio mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka kumi, utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu, umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 na 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kupunguza Umaskini, Sera ya Elimu ya Juu, Sera ya Ufundi na Mafunzo, Sera ya Sayansi na Teknolojia, pamoja na Mpango Kamambe wa Wizara.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mafanikio katika kipindi hicho ni zaidi ya asilimia tisini. Baadhi ya malengo yaliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Kuweka utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi waliofaulu vizuri ambao wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia mafunzo ya elimu ya juu na ufundi;

- Kupanua, kuimarisha na kuboresha elimu ya juu na ya ufundi pamoja na ujasiriamali ili kusaidia ujenzi wa uchumi wa kisasa;

- Kuongeza nafasi ya elimu kwa wanawake na kuweka mazingira mazuri ya kupata elimu hiyo kuanzia elimu ya msingi hadi ya chuo kikuu;
- Kubuni mpango wa kuwaandaa mabingwa katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ya viwanda nchini na nchi za nje;

- Kutoa kipaumbele na kuweka mtandao bora wa vituo vya tafiti nchini na kusambaza matokeo ya utafiti kwenye masoko; na

- Kuhakikisha sayansi na teknolojia za kisasa zinabuniwa na kusambazwa kwa wanawake ili kuwapunguzia harubu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio katika maeneo mengine ni kama ifuatavyo:-

- Mamlaka ya Elimu Tanzania iliyoanzishwa mwaka 2001 hadi mwezi Mei, 2005 imetoa ruzuku na mikopo kwa taasisi za umma na binafsi yenye thamani ya Sh 12,537,979,195/= kwa lengo la kuboresha miundombinu;

- Wizara yangu imeunda Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu na Ufundi. Bodi ilizinduliwa rasmi tarehe 30 Machi, 2005 kupitia chombo hiki, ni imani yangu kitawasaidia Watanzania wengi kupata nafasi za elimu ya juu na ufundi;

- Mpango Kamambe kwa kipindi cha 2003 - 2018 ulikamilishwa ili kuongoza utekelezaji wa shughuli za sekta za sayansi na teknolojia, elimu ya juu na ufundi;

- Serikali imetoa udhamini kwa wanafunzi 262 wanaosomea udaktari katika vyuo vikuu binafsi ili kuongeza idadi ya madaktari nchini;

- Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio Na. 5 la Mwaka 2005 hapo tarehe 21 Aprili, 2005 ili kukibadili Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia kuanzia tarehe 1 Julai, 2005;

- Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya iliyokuwa Tume ya Taifa ya Mionzi *(NRC),* ambayo kwa sasa ni Taasisi ya Nguvu za Atomiki *(Tanzania Atomic Energy Commission -TAEC);*

- Imekamilisha na kupitisha Bungeni Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 *(Universities Act);*
- Imehusisha sekta binafsi katika kutoa huduma za usafi, ulinzi na mapokezi kuanzia tarehe 1 Desemba, 2004; na

- Serikali imekamilisha mfumo wa kutumia gharama ya mwanafunzi katika vyuo vikuu na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, idadi ya vyuo vya elimu ya juu na ufundi nchini imeongezeka kutoka vyuo 23 mwaka 1995 hadi vyuo 43 mwaka 2005 na hivyo kutoa fursa kwa Watanzania wengi zaidi kupata elimu ya juu. Ili kuhakikisha kuwa vyuo hivyo vina hadhi na ubora unaohitajiwa, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi limechambua na kutoa ithibati na usajili kama ifuatavyo:-

- Vyuo vinne vimepewa barua ya mamlaka ya kuvianzisha ambayo ni Chuo Kikuu cha Arusha, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika cha Stadi za Biashara - Moshi na Chuo Kikuu Kishiriki kitarajiwa cha Tumaini Dar es Salaam;

- Vyuo vinne vimepewa Hati ya Usajili wa muda. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha *Mount Meru* - Arusha, Kituo cha Elimu ya Jamii Changanyikeni - Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya cha Bugando - Mwanza na Taasisi ya Elimu ya Juu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan - Dar es Salaam;

- Vyuo saba vilipata Hati ya Usajili kamili navyo ni Chuo Kikuu cha Taifa - Zanzibar, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Zanzibar - Tunguu, Chuo Kikuu Kishiriki cha Iringa, Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Kilimanjaro *(KCMC)* - Moshi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu - Zanzibar na Chuo Kikuu Kishiriki cha Makumira; na

- Vyuo Vikuu vinane vina Hati ya Ithibati kama ifuatavyo: Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, Mikocheni - Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Tanzania - Mwanza, Chuo Kikuu cha Tumaini - Moshi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Usanifu Majengo, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Tiba cha Muhimbili na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mafanikio kwa kipindi cha miaka kumi (1995 - 2005), Serikali imepata mafanikio katika maeneo mbalimbali ya elimu ya juu na ufundi, sayansi na teknolojia kama vile maeneo ya udahili, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu na huduma, kuboresha mazingira ya ufundishaji pamoja na urekebishaji wa mitaala ili iendane na mahitaji ya soko la ajira na matumizi ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa udahili, idadi ya wanafunzi waliojiunga na vyuo vya elimu ya juu na ufundi iliongezeka kutoka wanafunzi 14,076 mwaka 1995/96 hadi wanafunzi 48,236 mwaka 2004/2005. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 243. Idadi ya wanafunzi wa kike waliojiunga na vyuo hivyo katika kipindi hicho

iliongezekea kutoka 2,369 mwaka 1995 na kufikia 15,782 mwaka 2004/2005, ongezeko hilo la wanafunzi 13,413 ni sawa na asilimia 566.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na kuboresha miundombinu katika taasisi kwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

- Ujenzi wa mabweni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam eneo la Mabibo yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 4,200 na mabweni mengine eneo la chuo yenye uwezo wa kulaza na wanafunzi 250;

- Ununuzi wa majengo ya *Tanzania Audit Corporation* barabara ya Chole kwa ajili ya Hosteli ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Tiba Muhimbili, yenye uwezo wa kutoa malazi kwa wanafunzi 595;

- Ujenzi wa mabweni matatu Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 620;

- Ujenzi wa vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

- Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara vyenye uwezo wa kukaa wanafunzi 600 - Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Tiba Muhimbili; na

- Ujenzi wa chanzo cha maji Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu Mzumbe na tangi la maji Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za elimu ya juu na ufundi, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, imepitisha Sheria ya Vyuo Vikuu, inayotoa taratibu rahisi za kuanzisha vyuo vikuu na vile vya ufundi. Aidha, kwa ajili ya kutoa elimu yenye kukidhi mahitaji ya soko la ajira, vyuo vya elimu ya juu na ufundi, vimefanya uchambuzi wa mitaala yake, matokeo ya uchambuzi huo yamesaidia kurekebisha programu zinazotolewa ili ziendane na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha Wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari, kuhusu umuhimu wa kutumia sayansi na teknolojia katika maisha yao ya kila siku. Kuanzia mwaka 1995, vipindi 52 vilitangazwa kila mwaka kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam. Aidha, Serikali iliandaa mpango wa miaka mitano (2003 - 2008) wa uendelezaji wa sayansi ya msingi nchini, pamoja na mwongozo wa kuwaendeleza wabunifu na wavumbuzi. Serikali pia iliendelea kuwatunuku Wananchi waliofanya vizuri hasa wanawake, ambapo Tuzo ya Sayansi ilitolewa kwa wasichana 27 waliofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza Kidato cha Nne mwaka 2001 hadi 2003 na wasichana watano waliomaliza Kidato cha Sita mwezi Mei, 2002 na 2003 katika masomo ya Hisabati, Kemia, Baiolojia na Fizikia. Wanafunzi wasichana waliopata Tuzo ya Kidato cha Nne mwaka 2001, wanagharamiwa masomo yao ya Kidato cha Tano na Sita hadi Chuo Kikuu, kulingana na maendeleo yao ya kimasomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara iliandaa mkakati wa kuongeza idadi ya Walimu utakaokidhi mahitaji ya Mpango wa Elimu ya Sekondari, hivyo imehuisha Vyuo viwili, Chang'ombe na Mkwawa kuwa Vyuo Vishiriki vya Elimu vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya mwaka 2004/2005, kwa upande wa Utawala na Utumishi Makao Makuu katika mwaka 2004/05, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo:-

- Imeajiri watumishi 20 kwa ajili ya Makao Makuu na Vyuo vya Ufundi Mbeya na Arusha;

- Imewadhamini watumishi 36 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi;

- Imetayarisha Mkataba wa utoaji huduma kwa wateja *(Client Service Charter),* kwa lengo la kuboresha huduma zitolewazo na Wizara;
- Imeshirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za mapokezi, ulinzi na usafi kuanzia Desemba, 2004;

- Imeendelea kutumia mfumo wa wazi wa upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma *(Open Performance Review and Appraisal System);*

- Imeendesha mafunzo kwa watumishi 43 kuhusu Sheria ya Manunuzi na Misingi ya Maadili katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kupambana na rushwa sehemu za kazi. Aidha, imeendesha mafunzo ya kompyuta kwa watumishi 70; na

- Imeendesha mafunzo kuhusu masuala ya UKIMWI kama ifuatavyo: Uelimishaji rika *(HIV/AIDS Peer Educators),* kwa watumishi 37 na wanafunzi 34 toka Makao Makuu ya Wizara, Vyuo Vikuu na Taasisi zake; imejenga uwezo wa kuratibu shughuli za UKIMWI kwa watumishi 20 toka Makao Makuu ya Wizara, Vyuo Vikuu na Taasisi zake na pia i metoa ushauri nasaha kuhusu masuala ya UKIMWI *(HIV/AIDS Para-Counseling),* kwa watumishi 70 Wizarani, Makao Makuu, Vyuo Vikuu na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO,* katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, imetekeleza maamuzi ya kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO.* Katika kikao hiki miradi ifuatayo iliidhinishwa kutekelezwa:-

- Mradi wa Kuboresha Maktaba ya Kituo cha Madini cha Kusini na Mashariki mwa Afrika *(Southern and Eastern Africa Mineral Centre);*

- Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji wa Elimu ya Wanyama kwa kutumia Teknolojia ya Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine;

- Kuadhimisha miaka mia moja ya Seminari ya Rubya. Ushirikiano wa *UNESCO* utaiwezesha Seminari kutafakari jukumu lake la kutoa elimu ya sekondari na kubuni mikakati mipya ya kuimarisha elimu hiyo ikiwa ni pamoja na kuchangia maendeleo ya jamii inayoizunguka;

- Mafunzo ya Uzamili kwa mtumishi mmoja katika eneo la Haki za Binadamu;
- Mradi wa Kikanda wa Kuimarisha Mtandao wa Shule zilizoshirikishwa na shughuli za *UNESCO* katika Kanda ya Ziwa Victoria *(UNESCO Associated Schools' Project);*

- Mradi wa kutoa mafunzo na kuimarisha vitendea kazi kwa kituo cha Televisheni ya Taifa;

- Tume iliratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi yaliyofadhiliwa na *UNESCO* kwa kushirikiana na nchi wanachama;

- Kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa mwaka 2003/2004 na taarifa zake kuwasilishwa *UNESCO;*

- Kufanikisha uwekaji saini Makubaliano kati ya *UNESCO* na Serikali kuhusu uendeshaji wa Ofisi ya *UNESCO* Kanda ya Dar es Salaam. Ofisi hii inawakilisha nchi za Comoro, Madagascar, Mauritius, Seychelles na Tanzania yenyewe kama mwenyeji; na

- Kuchapisha Jarida la *Tanzania and UNESCO* na kusambaza nakala zake kwa walengwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Elimu ya Juu, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

- Kuunda Bodi ya kuratibu Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi nchini na nje ya nchi;

- Kutayarisha kanuni za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya ufundi nchini na nje ya nchi;

- Kuratibu uboreshwaji wa mitaala na mbinu za kufundishia kwa lengo la kuboresha elimu ya juu;

- Kutathmini utekelezaji wa mpango wa ugharamiaji endelevu wa elimu ya juu;

- Kuelimisha wadau kuhusu upatikanaji na ugharamiaji wa elimu ya juu ndani na nje ya nchi;

- Kuendeleza ushirikiano wa kielimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Madola, Ushirika wa Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na nchi mbalimbali ambazo zina ushirikiano wa kielimu na Tanzania; na

- Kuendeleza udhamini wa wanafunzi 1,100 wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari, ambao kati yao, 262 wapo katika vyuo vikuu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:-

- Kuendesha mifuko ya kugharamia utafiti na kudhamini wanafunzi;

- Kuendeleza eneo lililotolewa kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari kwa kutayarisha michoro na *geosurvey;*

- Kupanua Maktaba ya Chuo ili iweze kutumiwa na wanafunzi kwa saa 24;

- Kuendeleza utaratibu wa kudahili wanafunzi wa udhamini binafsi;

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kutoka wastani wa asilimia 31 hadi kufikia asilimia 33;

- Kutoa mafunzo ya awali *(pre-entry)* kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, uhandisi, teknolojia na takwimu;

- Kufanya tathmini ya kuvipandisha hadhi Vyuo vya Ualimu vya Dar es salaam, Mtwara na Shule ya Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki na Ambatanishi vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

- Kukamilisha ukarabati wa sehemu ya kafeteria kuwezesha kutumika na wanafunzi wenye walemavu;

- Kutoa mafunzo kwa Wahadhiri katika utumiaji wa vifaa vya *Video Conference;*

- Kudahili wanafunzi 4,514 wa mwaka wa kwanza kwenye programu za Shahada ya Kwanza;
- Kuboresha mitaala kulingana na hali halisi ya matakwa ya wadau;

- Kuendeleza mikakati ya kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Madini, Nzega;

- Kutathmini mitaala *(Academic Audit)* kwa kutumia wataalam kutoka nje; na

- Kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma zisizo rasmi kama njia ya kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo, katika mwaka wa fedha 2004/05, kilitekeleza yafuatayo:-

- Kuunda mitaala ya masomo ya Shahada nyingine za Kwanza 12 na kusimamia kazi za kurekebisha mitaala ili kozi za msingi zinazofanana zifundishwe kwa pamoja;

- Kutathmini na kuhuisha mitaala 12 na kufanya mabadiliko pale panapostahili;

- Kuimarisha, kutangaza na kusimamia masuala ya kukuza uhusiano kati ya Chuo na taasisi mbalimbali za Kitaifa zisizopungua 50 na Kimataifa zisizopungua 20;

- Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi 27 za Walimu na madarasa 11 na kukarabati barabara za ndani na maegesho ya magari;

- Kukamilisha Jengo la Utawala kwa fedha za ndani; na

- Kudahili wanafunzi 1,060 kati yao wanafunzi wa kike ni 188 ikiwa ni asilimia 18, waliodahiliwa kwa mwaka wa kwanza ni 279, kati ya hao wanafunzi 250 walipata udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili, katika mwaka wa fedha 2004/2005, kilitekeleza yafuatayo:-

- Kukarabati na kuongeza uwezo wa maktaba ili iweze kuchukua wanafunzi kufikia 80 na kuongeza matumizi ya jarida za *electronic.*
- Kuwekeana Mkataba wa Maelewano na Hospitali Kuu ya Taifa Muhimbili kuhusu utaratibu wa namna ya kuendesha sehemu ya shughuli zao kwa pamoja;

- Kupata ardhi ya ukubwa wa ekari 3,800 huko Kibamba na Kisarawe kwa ajili ya upanuzi wa Chuo;

- Kuendelea na matayarisho ya ukarabati wa hosteli zilizoko Barabara ya Chole, *Oystebay,* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 595;

- Kudahili wanafunzi wa Shahada mpya za *BSc Nursing Midwifery* na *BSc Nursing Management;*

- Kusajili wanafunzi 1,467 kati yao wanafunzi wa kike ni 462 ikiwa ni asilimia 31.5. Wanafunzi waliodahiliwa katika mwaka wa kwanza ni 325;

- Kutoa mafunzo ya kompyuta kwa wahadhiri 32;

- Kuongeza uwezo wa nguvu za mtandao wa mawasiliano kutoka *megabit* 10 kwa sekunde kuwa 100 *megabit* kwa sekunde; na

- Kudhamini wafanyakazi 23 masomo ya sekondari na tisa masomo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, kilitekeleza yafuatayo:-

- Miradi mbalimbali inayojumuisha utafiti na mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa wakulima ikiwemo mradi wa bustani ya uzalishaji mboga na matunda, mradi wa kilimo cha mseto *(agro-forestry)*, mradi wa uhakika wa chakula kwa wakulima wadogo wadogo, mradi wa mbuzi wa kienyeji wa kuzalisha maziwa na nyama, mradi wa utafiti wa kufichua mabomu kwa kutumia panya buku na mradi wa *vanilla*;

- Kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu na ufugaji kwa wakulima na wafanyakazi;

- Kukarabati majengo na mtandao wa mabomba ya maji;

- Kujenga maabara ya *zoology* na kituo cha ujasiriamali na biashara;
- Kupanua jengo la maktaba ya kampasi ya Solomon Mahlangu na kukamilisha tathmini ya ujenzi wa chanzo mbadala cha maji kwa ajili ya kampasi hiyo. Kuendeleza ujenzi wa jengo la Patholojia ya mbegu kwa ufadhili wa *DANIDA;*

- Kukamilisha taratibu za kukifanya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

- Kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 2,280 kwa mwaka 2003/2004 hadi wanafunzi 2,480 mwaka 2004/2005, ongezeko hilo ni sawa na asilimia nane;

- Kununua majengo mawili *(Balhabou Hostels)* kwa ajili ya kulaza wanafunzi 188; na

- Kuhuisha mitaala 15 ya Shahada za Kwanza ili kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, katika mwaka wa fedha 2004/2005, kilitekeleza yafuatayo:-

- Kujenga mtandao wa kompyuta Makao Makuu *(Local Area Network)* na kuunganisha katika mtandao mkuu *(Wide Area Network),* vituo viwili vya mikoa, yaani Dar es Salaam na Mtwara, pamoja na kununua kompyuta;

- Kujenga maabara ya kompyuta 30, pamoja na kununua kompyuta kwa matumizi ya mafunzo kwa wanafunzi na wafanyakazi;

- Kutayarisha mpango mkakati *(Rolling Strategic Plan)* wa chuo wa 2004/2005 - 2008/2009, ambao umeanza kutekelezwa;

- Kutayarisha Sera ya Matumizi ya Mawasiliano ya Kompyuta *(ICT Policy)* na mpango thabiti wa kutekeleza sera ya matumizi ya kompyuta *(ICT Masterplan)* katika kufundishia na kuboresha utawala;

- Kudahili wanafunzi 3,759 kati yao wanawake 1,033 na wanaume 2,721; na

- Kuhamasisha na kufikia uwiano wa asilimia 27 kati ya wanafunzi wa kike na wakiume waliodahiliwa mwaka 2005. Lengo la muda mrefu ni kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Mzumbe, katika mwaka wa fedha 2004/2005, kilitekeleza yafuatayo:-

- Kuendeleza ujenzi wa Maktaba ya Chuo kwa msaada wa fedha kutoka Mfuko wa Elimu;

- Kuendeleza ukarabati wa majengo ya Chuo kwa ajili ya malazi ya wanafunzi;

- Kukamilisha ukarabati wa jengo la zamani lililogeuzwa kuwa bweni;

- Kununua majengo manne ya iliyokuwa Benki ya *NBC* huko Mbeya. Majengo hayo yana uwezo wa kuchukua wanafunzi 168 wa Shahada ya Kwanza au 84 wa Shahada ya Uzamili, pia yana uwezo wa kuchukua wanasemina 27;

- Kusomesha Walimu saba katika ngazi ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa *(Ph.D);* na

- Kusajili wanafunzi 2,550, kati yao wanafunzi wa kike ni 955 ikiwa ni asilimia 37.5. Waliodahiliwa kwa mwaka wa kwanza ni 945.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, katika mwaka wa fedha 2004/2005, lilitekeleza yafuatayo:-

- Kukagua na kutathmini mipango ya kuanzisha vyuo na hatimaye kutoa Hati za Mamlaka ya kuanzisha Vyuo Vikuu vitano vya Mwenge (Moshi), Ruaha (Iringa), *Muslim* (Morogoro), *Bishop Kisanji* (Mbeya) na *Azad* (Zanzibar);

- Kukagua na kutoa Hati Stahili za Usajili katika vyuo vinne vya Mzumbe, Chuo Kikuu cha Arusha, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu Kishiriki cha Bugando;

- Kukagua kwa dharura kwa lengo la kutatua matatizo yaliyojitokeza katika uendeshaji na utawala wa Chuo Kikuu Zanzibar na Chuo Kikuu cha *Mount Meru;*
- Kutathmini kwa lengo la kuidhinisha programu za masomo katika vyuo mbalimbali;

- Kufanya tathmini, kwa lengo la kutambua hadhi na uhalali wa Vyeti, Stashahada na Shahada za Kawaida na Kanuni za Uzamili kulingana na maombi ya wadau;

- Kuendesha warsha mbili za wadau wa sekta ya elimu ya juu kuhusu taratibu za kuanzisha vyuo bila kukiuka maelekezo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuhusu nafasi ya elimu ya juu katika maendeleo ya Tanzania; na

- Kutoa machapisho na taarifa za kuelimisha umma kuhusu mipango na taratibu za kupata elimu ya juu nchini na nje ya nchi *(Guide to Higher Education in Tanzania)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2004/2005, ilitekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha ziara za mikoa kufikia ishirini, kwa madhumuni ya kuwahamasisha wadau kuchangia katika Mfuko wa Elimu, kuanzisha Mifuko ya Elimu katika Halmashauri za Wilaya na kuwekeza zaidi katika miradi ya elimu;

- Kuanzisha kipindi maalum cha redio kijulikanacho kama Ujue Mfuko wa Elimu, madhumuni yake ikiwa ni kuwashirikisha wadau kutoa maoni yao juu ya Mfuko wa Elimu na kuwahamasisha kuchangia katika Mfuko na kuwekeza kwenye miradi ya elimu. Kipindi hiki hurushwa kila siku ya Jumapili saa 12.15 hadi saa 12.30 kupitia Redio Tanzania.

- Kutoa machapisho na vipeperushi vinavyoelimisha kuhusu Mfuko na shughuli za Mamlaka ya Elimu Tanzania;

- Kutoa ruzuku na mikopo yenye jumla ya Sh. 5,778,445,647/= hadi mwezi Aprili, 2005 katika vyuo na shule 27.

- Mfuko wa Elimu ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, tarehe 11 Machi, 2005 na kiasi cha Sh. 106 milioni zilichangishwa.
- Kuandaa Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* wa miaka mitano wa kuanzia 2005/2006 hadi 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ufundi, katika mwaka wa fedha 2004/2005, imefanya yafuatayo:-

- Kugharamia mafunzo ya watumishi 20 wa Vyuo vya Ufundi vya Mbeya, Arusha na Makao Makuu katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa, Shahada ya Uzamili, *Diploma* ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi;

- Kukarabati mitambo, majengo na vifaa mbalimbali katika Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya kwa gharama ya shilingi 64,281,200/=. Aidha, imenunua vifaa vya kufundishia vyuoni vyenye thamani ya shilingi 195,597,000/=;

- Kutoa mafunzo maalum *(Access Course),* kwa wasichana 19 katika mpango maalum wa kujiunga na elimu ya ufundi katika vyuo vya Arusha na Mbeya;

- Kutoa mafunzo maalum ya ualimu *(Pedagogical Training)* kwa Maafisa Elimu 25 walioajiriwa katika Vyuo vya Mbeya na Arusha;

- Kununua mashine na mitambo yenye thamani ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Mbeya katika kuimarisha ufundishaji wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi;

- Kununua vitabu vya kiada na rejea vyenye thamani ya shilingi milioni 85 katika fani za mitambo, umeme, magari, usanifu majengo, ujenzi na masomo ya jumla kwa Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya;

- Kumpata Mtaalam Mwelekezaji *(Consultant)* kwa ajili ya kuhuisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996;

- Kuendelea kujenga bweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika Chuo cha Ufundi Mbeya lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64;

- Kuongeza udahili wa wanafunzi katika Chuo cha Sayansi za Jamii Kivukoni kutoka 108 hadi 202;
- Kukamilisha upatikanaji wa hati miliki ya eneo la Bububu Zanzibar kwa matumizi ya Chuo cha Sayansi za Jamii Kivukoni;

- Kukamilisha mtandao wa *internet* na tovuti ya Chuo cha Sayansi za Jamii Kivukoni;

- Kununua kompyuta 35, printa, mashine ya kurudufu na vitabu; na

- Kukibadili Chuo cha Ufundi Mbeya *(Mbeya Technical College)* kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya *(Mbeya Institute of Science and Technology - MIST).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kuanza kutumia mitaala mipya ya masomo katika ngazi ya Shahada ya Uhandisi *(Bachelor of Engineering)* katika fani za Ujenzi, Mitambo, Umeme na Mawasiliano Angani;

- Kukarabati maabara tatu za Taasisi, hosteli moja ya wanafunzi iliyoko Chang'ombe, pamoja na mabweni matatu yaliyopo kwenye eneo la Taasisi baada ya kupata kiasi cha Shilingi milioni 165 kutoka Mfuko wa Elimu;

- Kugharamia mafunzo kwa watumishi 41 katika ngazi ya *Diploma* moja, Stashahada ya Juu ya Uhandisi/Shahada ya Uhandisi tano, Shahada ya Uzamili 18 na Udaktari wa falsafa 17;

- Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, vyuo vya elimu ya juu na vya ufundi vilivyo nchini na vya Kimataifa kama ifuatavyo: Kuendeleza Mkataba na Serikali ya Watu wa China, kwa kupeleka watumishi watatu China kwa ajili ya mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)* na kushirikiana na Chuo cha *Leeds Metropolitan University,* kuendesha kozi ya Uzamili, *MSc in Facilities Management,* kwa udhamini wa *Association of Commonwealth Universities;*

- Kuendeleza mradi wa utafiti juu ya taka ngumu *(Solid Waste Management)* chini ya udhamini wa *British Council;*
- Kuendeleza ushirikiano na *Cape Town University of Technology,* kupitia mikutano kati ya vyuo husika na kubadilishana watumishi kwa muda mfupi;

- Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya *e-Degree* (Afrika Kusini) kutoa mafunzo ya shahada mbalimbali kupitia mtandao wa kompyuta;

- Kuendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya utaratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA),* kwa kushirikisha wahadhiri watatu katika warsha ya kujenga uwezo kwenye usimamizi wa mafunzo na masuala ya jinsia; na

- Kuendeleza Mkataba na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* wa kukuza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuanza kufundisha programu mpya inayotoa cheti cha *IT-Basic Technician.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, limetekeleza yafuatayo:-

- Kusajili vyuo vya ufundi 52 kati ya hivyo 35 vimepewa Hati ya Usajili Kamili *(Full Registration)* na 17 Usajili wa Muda *(Provisional Registration);*

- Kukagua na kutoa Hati ya Ithibati Kamili *(Full Accreditation)* kwa vyuo vitano na Ithibati ya Muda *(Provisional Accreditation)* vyuo 17;

- Kuidhinisha kuanzishwa na kuanza kutolewa kwa elimu na mafunzo ya ufundi katika chuo kimoja binafsi cha *St. Joseph College of Engineering and Technology* cha Dar es Salaam;

- Kuweka viwango vya mafunzo *(Standards of Training Programmes)* kwa programu 12 za elimu na mafunzo ya ufundi;

- Kuidhinisha mitaala inayozingatia umahiri wa wanafunzi kwa programu za mafunzo 36. Mitaala hiyo tayari imeanza kufundishwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na chuo binafsi cha *St. Joseph College of Engineering and Technology*. Aidha, mitaala mipya inayozingatia umahiri, itaanza kufundishwa pia katika Chuo cha Mipango cha Dodoma, Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam mara mwaka mpya wa masomo utakapoanza;

- Kutayarisha mitaala mipya kwa progamu za mafunzo sita katika eneo la mafunzo la Uhandisi na Sayansi nyingine. Mitaala hiyo itaanza kufundishwa katika vyuo vya ufundi vya Arusha, Karume (Zanzibar) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya *(MIST),* mara mwaka mpya wa masomo utakapoanza;

- Kuendelea kuratibu Mitihani ya Kitaifa ya Ufundi Sanifu *(Full Technician Certificate)* na Stashahada ya Juu ya Uhandisi *(Advanced Diploma in Engineering),* kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mitihani *(NECTA)*; na

- Kutayarisha taratibu na kanuni za usajili wa wataalam, walimu na mafundi wengine wanaofundisha katika vyuo vya ufundi kwa lengo la kuhakiki sifa za wataalam hao. Aidha, Baraza limeendesha mafunzo katika kanda sita kuhusu usajili wa wataalam wanaofundisha katika vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2004/2005, Wizara yangu kupitia Idara ya Sayansi na Teknolojia imewasilisha kwenye Bunge lako Tukufu na kuridhia Mikataba minne na Itifaki moja inayolenga kukuza na kusimamia matumizi salama na ya amani ya nishati ya nyuklia kwa maendeleo ya Taifa, kama ifuatayo:-

- Azma ya kutokomeza au kutoendeleza utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia *(Non-Proliferation of Nuclear Weapons Treaty-NPT);*

- Kutumia Nishati ya Nyuklia kwa shughuli za amani tu na siyo katika utengenezaji wa Silaha za Nyuklia *(Safeguards Agreement);*

- Itifaki ya Kimataifa *(Additional Protocol to Safeguards Agreement);*

- Azma ya kutoa Taarifa ya Ajali ya Nyuklia Mapema *(Early Notification of Nuclear Accident);*

- Misaada ya kushughulikia Ajali ya Nyuklia au Dharura ya Ki-Radiolojia *(Convention on Assistance in Case of a Nuclear Accident or Radiological Accidents);*

- Kuandaa Mkataba unaolenga Kusimamia Utunzaji wa Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia *(Convetion on Physical, Protection on Nuclear Material),* Maazimio ya Mkataba huu yaliwasilishwa na kupitishwa katika Kikao cha Bunge cha mwezi Aprili, 2005;

- Kuandaa na kupitishwa Bungeni katika kikao chake cha mwezi Aprili, 2005, Sheria iliyounda Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy);*

- Kuwasilisha Baraza la Mawaziri, Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Utungaji wa Sera ya Bioteknolojia baada ya kujadiliwa na wadau mbalimbali;

- Kuandaa na kuboresha maeneo ya ushirikiano katika sayansi na teknolojia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali za Cuba, Korea, Vietnam na Switzerland;

- Kufanya maandilizi ya uanzishwaji wa Kituo cha *Radianuclide Monitoring,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya *CTBTO;*

- Kusaini Hati ya Maelewano *(Memorandum of Understanding)* ya Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uswiss katika kuendeleza ujuzi na mafunzo katika maeneo ya utafiti wa kisayansi na kiteknolojia, pamoja na uboreshwaji wa miundombinu ya asasi, taasisi za utafiti na maendeleo;

- Kufanya mazungumzo mapya ya mashirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kuhusu Mradi wa Nishati ya Jua, utakaotekelezwa katika Kijiji cha Mwasayi, Wilayani Maswa. Aidha, taarifa ya Maelewano *(Memorandum of Understanding)* ya Ushirikiano kati ya Serikali hizo mbili, imeandaliwa na inatarajiwa kusainiwa hivi karibuni; na

- Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam, vinavyohusu umuhimu wa kutumia sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kutoa Tuzo ya Wizara kwa wasichana ishirini (Kidato cha Nne wasichana kumi na moja na Kidato cha Sita wasichana tisa), waliofanya vizuri na kuongoza kwa upande wa wasichana katika masomo ya sayansi ya msingi (hisabati, kemia, fizikia na bailojia) katika mwaka wa 2004. Vilevile ilitoa tuzo hiyo kwa wasichana kumi na tatu waliofaulu mwaka wa kwanza wa 2003/2004 na kuongoza katika masomo ya sayansi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilifanya mkutano wa pamoja kuhusu uundwaji wa Kamati za Sayansi na Teknolojia katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kufikisha dhana ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, ilitekeleza yafuatayo:-

- Kufuatilia wabunifu na wagunduzi wenye vipaji maalum katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mwanza, Rukwa na Kagera na jumla ya vijana 26 walipatikana;

- Kuendelea kufadhili miradi ya utafiti kulingana na vipaumbele;

- Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa watafiti ili kuweza kutayarisha miradi ya utafiti inayokubalika kitaaluma;

- Kubuni jiko sanifu na kuwapatia mafunzo mafundi wadogo wadogo 52 katika Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma; jumla ya majiko 500 yamesambazwa mikoani;

- Kushirikiana na Shirika la Nyumbu kutengeneza trekta dogo linaloongozwa kwa mkono ambalo linafanyiwa majaribio;

- Kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Leseni za Biashara, Tume imeanzisha na kuisajili kampuni *IP - Forum* inayojumuisha wanataaluma, watafiti, wagunduzi na Wananchi kwa ujumla, kwa lengo la kulinda bunifu za wanasayansi na teknolojia;

- Kuendelea kukarabati jengo la Tume;

- Kukamilisha uanzishaji wa Masjala ya Taifa ya Utafiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa mbali mbali za utafiti kutoka ndani na nje ya nchi. Taarifa kamili ya Masjala hiyo inapatikana katika *http://www.research.or.tz;*

- Kuimarisha mtandao wa mawasiliano kwa kusambaza leseni za *software* za *Microsoft Office* kama vile za *Windows 2000* na *Microsoft Office XP,* ili kuwanusuru Watanzania kutumia *Microsoft* zisizo halali. Aidha, iliweza kununua kompyuta 1,000 kutoka kwa taasisi zisizo za Kiserikali kutoka nje ya nchi na kuzisambaza; na

- Kutoa mafunzo ya kompyuta kwa watumishi 300 kutoka Serikalini, wafanyabiashara, wanasiasa (Waheshimiwa Wabunge na Madiwani).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Tifa ya Nguvu za Atomiki, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 ilitekeleza yafuatayo:-

- Kutoa huduma ya upimaji wa mionzi *(Personnel Radiation Monitoring)* kwa wafanyakazi wa mionzi 1,000 kati ya 1,200 kutoka katika vituo 121 kati ya vituo 250. Aidha, ilikagua vituo 135 kati ya vituo 250 vya mionzi;

- Kufuatilia vituo 23 vilivyokuwa vimefungiwa ili kuhakikisha havikiuki agizo la kusimamisha huduma za *X-ray* ambapo vituo tisa vilirekebisha kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi na kuruhusiwa tena kuendelea na kutoa huduma za *X-ray;*

- Kufanya marejeo ya kanuni za kinga ya mionzi *(The Protection from Radiation (Code of Practice) Regulations 1990),* ambapo kanuni mpya, zinazoitwa *The Atomic Energy Protection from Ionizing Radiation Regulations 2004,* zimetayarishwa;

- Kutoa elimu ya kinga ya mionzi kwa njia za redio na vipindi vya televisheni. Aidha, Tume iliendesha semina nne, moja kati ya hizo zikiwa ni kwa watumiaji wa mionzi *(Radiographers)*, mbili kwa ajili ya wafanyakazi katika migodi na nyingine ya *power conditioning;*

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi minane; mradi wa kutokomeza mbung'o Mafia na Babati na ule wa kuendeleza mifugo, Zanzibar baada ya utokomezaji wa mbung'o, inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za *Atomic (IAEA)* inayotumia teknolojia ya mionzi hapa nchini. Miradi ambayo Taasisi husika zilipatiwa zaidi ya dola za Kimarekani 770,000 kama vifaa, mafunzo kwa wataalam wake na ushauri wa kitaalamu;

- Kutoa leseni ya kutumia mionzi kwa vituo 145;

- Kuanza kutumia jengo la kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi;

- Kukagua sampuli 2,800 za vyakula, mbolea na bidhaa nyingine za vyakula ili kudhibiti viwango vya mionzi katika vyakula viingizwavyo na viendavyo nje ya nchi *(Imports and Exports);*

- Kufanya matengenezo ya mashine 18 za *X-ray* na vifaa vingine vya nyuklia;

- Kuhakiki *(calibrate)* vifaa 28 vya kupima mionzi, ambapo vifaa 12 vikiwa vya hapa nchini na 16 kutoka nchi za Kenya, Uganda na Zambia;

- Kugharamia masomo ya Shahada ya Uzamili katika Sayansi *(Msc)* na Sheria *(LLM)* kwa wafanyakazi wawili wa Taasisi;

- Kuanzisha maabara ya *X-Ray (XRF) Fluorescence Spectroscopy* na *X-Ray Diffraction (XRD);*

- Kuanzisha maktaba ya kupatia taarifa za Kimataifa za Nyuklia *(International Nuclear Information System-INIS),* kupitia mradi wa *IAEA;*

- Kuimarisha usalama katika vituo vyenye vyanzo vya mionzi kwa kuweka vyombo vya kutoa tahadhari *(Security Alarm Systems* na *Radio Call)* katika Vituo vyake vilivyopo *Ocean Road Cancer Institute,* Tanga, *Central Radioactive Waste Management Facility* ya Tume iliyoko Njiro katika ofisi za Tume - Arusha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Hospital ya Taifa ya Muhimbili; na

- Kutangaza katika Gazeti la Serikali orodha ya watumiaji wa vyanzo vya mionzi ayonisha ambao walikidhi masharti ya usalama wa utumiaji wa vyanzo vya mionzi na kupata leseni kwa kipindi cha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/06, Idara ya Utawala na Utumishi inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudhamini watumishi 49 mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi;

- Kuendesha mafunzo ya kompyuta na mifumo ya habari *(IT),* kwa watumishi 150 katika sehemu za kazi *(In-house Training);*

- Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma zisizo rasmi katika Vyuo vya Ufundi Mbeya na Arusha hususan huduma za ulinzi, usafi na chakula;

- Kutekeleza mfumo wa uwazi wa upimaji utendaji kazi kwa watumishi *(Open Performance Review and Appraisal System);*

- Kuajiri watumishi 73 kwa ajili ya Makao Makuu ya Wizara, Vyuo vya Ufundi Mbeya na Arusha. Aidha, Wizara inatarajia kuajiri wanataaluma na watumishi wengine 405 kwa ajili ya Vyuo Vikuu na Taasisi zake, kwa lengo la kupunguza uhaba wa wafanyakazi;

- Kuendelea kuwaelimisha watumishi wa Wizara kuhusu mpango wa Serikali wa kuboresha utendaji kazi na huduma bora kwa umma;

- Kuhamasisha watumishi kupima afya zao na kutoa huduma kwa watakaojitokeza kwa hiari yao; na

- Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwaelimisha Wananchi na watumishi kupitia vyombo vya habari kuhusu taratibu za kupata huduma zitolewazo na Wizara kwa lengo la kupiga vita rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya *UNESCO,* katika kipindi cha mwaka 2005/2006, inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuandaa, kwa kushirikiana na asasi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, Programu na Bajeti ya *UNESCO* kwa kipindi cha 2006 - 2007;

- Kuratibu utekelezaji na kufanya tathmini ya miradi inayoendelea na ile itakayoidhinishwa kwa kipindi cha 2006 - 2007, kama itakavyoamuliwa na Kikao cha 33 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO*; na

- Kuifanyia mapitio Katiba ya Tume ya *UNESCO,* kwa lengo la kuipa Tume na Sekretarieti yake nguvu zaidi za kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuelimisha wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu nafasi za elimu ya juu nchini na nje ya nchi;

- Kukamilisha utayarishaji wa kanuni chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 na kusimamia utekelezaji wake;

- Kuelimisha wadau kuhusu upatikanaji wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundi;

- Kutathmini Sera ya Elimu ya Juu na kutoa mapendekezo ya kuiboresha;

- Kuratibu mafunzo kwa viongozi wa Serikali na mashirika ya umma wa ngazi ya kati na juu. Mafunzo hayo ambayo yatagharamiwa baina ya Serikali na Watendaji Wakuu wa mashirika mbalimbali, yanalenga kuboresha ufanisi ili kuimarisha mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa;

- Kushughulikia urejeshwaji wa utaratibu wa Serikali wa kudhamini wanafunzi nje ya nchi kwa baadhi ya fani muhimu Kitaifa ambazo hazipatikani nchini au nafasi zake ni finyu;

- Kuendeleza ushirikiano wa kielimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Madola, Ushirika wa Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika na nchi mbalimbali, zilizo na ushirikiano wa kielimu na Tanzania;

- Kuendelea kudhamini wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari. Kwa mwaka 2005/2006, Wizara itadhamini wanafunzi 1,427 (1,060 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili na 367 katika Vyuo Vikuu Binafsi); na

- Kudhamini wafanyakazi na wanataaluma 40 katika Shahada za Uzamili na Shahada za Juu za Falsafa. Kati yao 27 ni wa Shahada ya Uzamili na 13 ni wa Shahada ya Juu ya Falsafa. Hatua hii inachangia katika kuongeza idadi na uimarishaji wa wanataaluma katika vyuo vikuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 3,440 wa Shahada ya Kwanza na 420 wa Stashahada ya Ualimu;

- Kukamilisha ujenzi wa madarasa makubwa mawili yenye uwezo wa kila moja kukaliwa na wanafunzi 1,000;

- Kuendeleza sehemu ya Buyu iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

- Kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam;

- Kuanzisha programu za Stashahada na Shahada za Ualimu kwenye Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam;

- Kuboresha huduma ya maji kwenye Mabweni ya Mabibo;

- Kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanafunzi wengi chuoni;

- Kuanzisha ukarabati wa Chuo Kikuu cha Elimu cha Chang'ombe na Mkwawa;

- Kutoa mafunzo maalum kwa wadahiliwa wa kike kwenye fani za Sayansi, Teknolojia, Uchumi na Takwimu, kwa lengo la kuongeza wahitimu wa kike kwenye fani hizo;

- Kuchapisha na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau kupitia majarida mbalimbali ya ndani na nje ya nchi;

- Kushirikiana na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi katika kufanya utafiti; na

- Kuendelea kutoa elimu juu ya UKIMWI na ushauri nasaha kwa jumuiya ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kinatarajia kutekeleza yafuatayo: -

- Kuendelea na utayarishaji wa sera na programu katika kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa Chuo;

- Kuongeza udahili wa wanafunzi kufikia 350 sawa na ongezeko la asilimia 40;

- Kuendelea kurekebisha mitaala ili kuruhusu kozi nyingi za msingi na zingine zinazofanana zifundishwe kwa pamoja katika idara mbalimbali ili kuimarisha ufanisi wa utoaji mafunzo;

- Kuendeleza wafanyakazi wa Chuo kimasomo;

- Kuimarisha uwiano kati ya wanawake na wanaume kwa kukamilisha na kutekeleza Sera ya Jinsia itakayosimamia shughuli za jinsia;

- Kuimarisha mahusiano na taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa zinazohusiana na taaluma za makazi na mazingira;

- Kuimarisha na kuratibu matumizi ya teknolojia ya mawasilano katika shughuli za ufundishaji na uendeshaji wa Chuo;

- Kukarabati mabweni matatu, ofisi 13, vyoo 10 na nyumba 10 wanazoishi wafanyakazi wa Chuo; na

- Kujenga madarasa makubwa sita yenye uwezo wa wanafunzi 200 kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuendeleza ukarabati wa nyumba zilizonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya hosteli za wanafunzi zilizopo Barabara ya Chole, Dar es salaam;

- Kujenga kumbi kubwa mbili za kisasa za kufundishia, zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kila moja, ambazo pia zitakuwa na jumla ya vyumba 40 vya ofisi;
- Kuendelea na upanuzi wa maktaba, kuweza kuhudumia watumiaji 1,300 kwa wakati mmoja, ikilinganishwa na uwezo wa watumiaji 200 hivi sasa na kuanza kuendeleza ardhi ya Chuo iliyoko Kibamba/Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuongeza madarasa matano yenye uwezo wa kutumika na wanafunzi 480;

- Kudahili wanafunzi 100, kati yao 80 kwa udhamini wa Serikali 20 udhamini binafsi;

- Kuzungusha ukuta katika eneo la Taasisi ili kuimarisha usalama wa mali na vifaa vya taasisi;

- Kuendeleza tafiti mbalimbali na kutoa ushauri; na

- Kuimarisha Kituo cha Redio kwa kununua *Outside Broadcasting Van-OBVAN* na *transmitter (Radio Mlimani FM)* ili matangazo yake yaweze kusikika sehemu nyingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuendelea kushirikiana na wahisani, pamoja na Serikali katika kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji wa mali ya asili, misitu na ufugaji kwa wakulima na wafanyakazi;

- Kudahili wanafunzi 1,000 wa Shahada za Kwanza na wanafunzi 300 wa Shahada za Juu;

- Kuendeleza miradi ya utafiti kama miradi inayojumuisha utafiti na mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa wakulima;

- Kushirikiana na vyuo vingine vya nchi zilizoendelea na zinazoendelea katika utafiti na kutoa taarifa za utafiti ndani na nje ya nchi;

- Kuendeleza miradi ya maendeleo kama kuanza ujenzi wa mabweni 10 ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 3,000;
- Kukamilisha uwekaji wa Mtandao wa Kompyuta katika Kampasi ya Solomon Mahlangu;

- Kukarabati vyumba 25 na mtandao wa mabomba ya maji chuoni;

- Kuanza ujenzi wa vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa wanafunzi 500 kila moja;

- Kuboresha mazingira ya sehemu wanamoishi wanafunzi na wafanyakazi;

- Kuboresha mazingira ya kusomea na kufundishia;

- Kukamilisha ujenzi wa maabara ya *zoology;*

- Kukamilisha upanuzi wa maktaba iliyopo Solomon Mahlangu ili kuongeza uwezo wa kuhudumia watumiaji kutoka 300 hadi 1,000;

- Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Ujasiriamali na Biashara; na

- Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Patholojia ya Mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuboresha miundombinu kwa kuweka mtandao wa kisasa kwenye maktaba na kutengeneza upya mpango kabambe wa Chuo;

- Kuendeleza mafunzo ya walimu 10 ili wafikie kiwango cha Udaktari wa Falsafa;

- Kufanya tafiti ndogo 10 na kubwa nne;

- Kuchapisha makala *(three Journals of Co-operative Business, two Research Report Series, one Research Abstract Series and one Manual);*

- Kuboresha kiwango cha huduma za uelekezi na ushauri; na
- Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 721 kufikia 1,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuongeza idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kufikia 21,429 baada ya kuondoa waliohitimu ama kuondoka chuoni kwa sababu mbalimbali;

- Kuongeza uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kutoka asilimia ishirini na saba ya sasa kufikia asilimia thelathini;

- Kuanzisha programu mbili mpya; Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Kompyuta *(BSc Computer Science)* na Shahada ya Uzamili ya Sayansi za Mazingira *(MSc Environmental Studies);*

- Kuimarisha ofisi za kanda ama kwa kununua majengo au kushawishi mikoa kukipatia Chuo majengo ya kudumu ili kupunguza mzigo wa kodi ya pango na kuweka mazingira mazuri ya kusoma;

- Kuimarisha matumizi ya mawasiliano ya kompyuta *(ICT)* ili kuboresha mafunzo, mawasiliano na kumiliki takwimu. Katika hili Chuo kinatarajia kufanya yafuatayo: Kujenga maabara ya pili ya kompyuta Makao Makuu; kuimarisha matumizi ya kompyuta katika kuandaa nyaraka za taaluma *(Study Materials),* kumbukumbu za wanafunzi *(Student Records)* na utawala;

- Kushirikiana na *African Virtual University (AVU)* kuanzisha kituo cha kuratibu na kuendesha mafunzo kwa walimu kwa kutumia mitandao ya mawasiliano ya kompyuta kama sehemu ya mpango wa *NEPAD* wa kuboresha taaluma za Waalimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini;

- Kufungua maabara za kompyuta na kuweka mtandao wa ndani katika vituo vya mikoa kufikia 10;

- Kuunganisha mtandao mpana *(WAN)* kati ya Makao Makuu na vituo vya mikoa 10;

- Kuwa na jukwaa la elektroniki *(Electronic Teaching and Learning Platform)* la kuboresha kutoa na kupokea taaluma kutoka mbali;
- Kuongeza uzoefu na umahiri wa kutumia kompyuta kwa wafanyakazi na wanafunzi;

- Kuhamasisha uandishi wa vitabu vya masomo kwa kutumia wataalam wa hapa nchini;

- Kuboresha mazingira ya kazi na hasa ofisi za wafanyakazi Makao Makuu na katika mikoa; na

- Kukamilisha kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi ya Chuo *(Land Use Plan).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Mzumbe, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuanza ujenzi wa mabweni yatakayoweza kuchukua wanachuo 1,000, ofisi za waalimu 100 na ukumbi mmoja wa mihadhara;

- Kuendeleza ujenzi wa maktaba mpya ya Chuo;

- Kuweka samani na kuanza masomo kwenye kampasi ya Dar es Salaam;

- Kukarabati, kuweka samani na kuanza masomo kwenye kampasi yake ya Mbeya;

- Kusomesha Walimu saba katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa *(Ph.D)* na Walimu sita katika ngazi ya Uzamili; na

- Kudahili wanafunzi wa Shahada ya Kwanza 893, kati ya hao 250 ni kwa udhamini wa Serikali na 643 udhamini binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, katika mwaka wa fedha 2005/2006 linatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia mipango na taratibu mpya za kuanzisha, kusajili na kudhibiti Vyuo Vikuu, programu za masomo na udahili wa wanafunzi chini ya Vyuo Vikuu;
- Kukamilisha mpango mkakati wa kutekeleza Sheria mpya ya Vyuo Vikuu iliyounda Kamisheni ya Vyuo Vikuu;

- Kuendesha semina kwa wakuu wa vyuo vikuu na taasisi zao kuhusu uongozi bora wa taasisi hizo;

- Kuandaa na kuratibu maonyesho *(exhibition)* ya vyuo vikuu;

- Kukamilisha mfumo wa tuzo Kitaifa *(National Qualifications Framework)* kwa kushirikisha wadau wa ubora wa elimu na mafunzo nchini;

- Kukamilisha vigezo vya ubora *(standards)* wa majengo, vifaa na huduma katika vyuo vikuu na kuratibu uzingatiaji wa vigezo hivyo;

- Kuendelea kutoa machapisho ya kuelimisha umma kuhusu mipango na taratibu za kupata na kuthibiti ubora wa elimu katika vyuo vikuu;

- Kuanza ukarabati wa jengo la ofisi za kudumu za Baraza; na

- Kuendelea kuhamasisha wafanyakazi kuhusu ugonjwa hatari wa UKIMWI na magonjwa mengine, pamoja na mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2005/2006, inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wadau kuchangia na kuwekeza kwenye miradi ya elimu na kupanua wigo wa uchangiaji katika Mfuko wa Elimu kwa kushirikisha wadau katika ngazi ya Wilaya. Aidha, Mamlaka itaendelea kuishauri serikali juu ya kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Elimu;

- Kuingia na kKuimarisha mashirikiano na Mifuko ya Elimu ya Halmashauri za Wilaya ili kuchochea uchangiaji;

- Kuendelea kutoa ruzuku na mikopo, kwa vyuo na shule kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kuboresha elimu;

- Kuanzisha mashirikiano na jumuiya za wananchi, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya dini na asasi mbalimbali katika kuhamasisha wadau kuchangia Mfuko wa Elimu na kushirikiana kugharamia miradi ya elimu nchini; na

Kuboresha ufanisi na utoaji huduma kwa kutekeleza mpango mkakati wa mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu inakusudia kufanya yafuatayo katika elimu ya ufundi:-

- Kununua vitabu vya kiada na rejea kwa Chuo cha Ufundi Arusha;

- Kugharamia mafunzo maalum ya ualimu kwa walimu wahandisi watakaoajiriwa katika Chuo cha Ufundi Arusha;

- Kutoa mafunzo maalum kwa wasichana katika mpango maalum wa kujiunga na elimu ya ufundi katika Chuo cha Ufundi Arusha;

- Kukarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali kwa Chuo cha Ufundi Arusha;

- Kugharamia mafunzo ya watumishi tisa wa Chuo cha Ufundi Arusha na Makao Makuu katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa tatu, Shahada ya Uzamili moja, *Diploma* ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi tano;

- Kukamilisha kuhuisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo;

- Kukifufua Chuo cha *TANESCO* Kidatu kuwa Chuo cha Ufundi Morogoro; na

- Kuratibu matumizi ya mitaala mipya ya *National Technical Awards (NTA 4 - 6)* katika ngazi ya Ufundi Sanifu katika Vyuo na Taasisi za Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuanza mafunzo ya Uhandisi Migodi katika ngazi ya Ufundi Sanifu;

- Kuanza kutumia mitaala mipya inayozingatia umahiri na kutoa vyeti vya *National Technical Awards (NTA 4 - 6)* katika ngazi ya Ufundi Sanifu;
- Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Uhandisi wa Kompyuta *(Bachelor of Engineering in Computer Engineering);*

- Kukamilisha matayarisho ya mitaala na taratibu za kuanzisha programu ya mafunzo ya Shahada ya Uzamili juu ya Ukarabati *(Maintenance Management);*

- Kuendesha mashindano ya Ubunifu katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yaitwayo *"Tanzania ICT Challenge Award"* kwa msaada wa *TCRA, SIDA* na Kampuni ya *Erickson* ya Sweden.

- Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya Kimataifa sehemu mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Kuendeleza Mkataba na Serikali ya Watu wa China kwa kupeleka watumishi China kwa ajili ya mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)*;

- Kuendesha kozi ya Shahada ya Uzamili *(MSc in Facilities Management),* kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha *Leeds Metropolitan* (Uingereza) kwa udhamini wa *Association of Commonwealth Universities*;

- Kuendeleza Mkataba na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* wa kukuza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT);*

- Kuendeleza mradi wa utafiti juu ya taka ngumu *(Solid Waste Management)* chini ya udhamini wa *British Council;*

- Kuendeleza ushirikiano na *Cape University of Technology* kwa kupitia mikutano kati ya vyuo husika na kubadilishana watumishi kwa muda mfupi; na

- Kuendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, katika mwaka wa fedha 2005/2006, inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kununua na kufunga mashine na mitambo kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo;

- Kugharamia mafunzo maalum ya ualimu kwa walimu wahandisi watakaoajiriwa;

- Kununua vitabu vya kiada na rejea;

- Kugharamia mafunzo ya watumishi 24 katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa sita, Shahada ya Uzamili 10, *Diploma* ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi nane; na

- Kuendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, katika mwaka wa fedha 2005/2006, inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha mitaala mitatu ya Shahada ya Kwanza katika fani za Sayansi Jamii, Jinsia katika Maendeleo na Maendeleo ya Uchumi;

- Kupata hadhi ya ithibati kamili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi;

- Kudahili wanafunzi 250 katika kiwango cha Stashahada 210 na Cheti 40;

- Kuajiri wanataaluma 21 na watumishi wengine 20;

- Kukarabati jengo la utawala, madarasa manne na maktaba moja; na

- Kuanza kuendesha mafunzo katika Tawi la Taasisi - Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, kwa mwaka wa fedha 2005/2006, linakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kukagua na kutathmini kwa ajili ya ithibati uwezo wa uendeshaji na uhakiki wa ubora wa mafunzo katika taasisi 20 za ufundi;
- Kusajili vyuo 15 vyenye uwezo wa kutoa elimu na mafunzo ya ufundi;

- Kuandaa, kukuza na kuidhinisha mitaala ya programu za mafunzo 30 yenye kuzingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira;

- Kuweka viwango vya mafunzo *(Setting Standards of Training Programmes)* kwa ajili ya programu 20 za mafunzo;

- Kuratibu mitihani ya ufundi ya Kitaifa katika ngazi ya Ufundi Sanifu *(Full Technician Course)* na Stashahada ya Juu ya Uhandisi *(Advanced Diploma in Engineering),* kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mitihani *(NECTA);*

- Kusajili walimu wa ufundi na wataalamu wengine 1,000 katika vyuo vya ufundi;

- Kusimamia na kuhakiki ubora wa mafunzo *(Quality Control and Quality Assurance)* katika taasisi na vyuo vya ufundi;

- Kuweka mfumo wa uwekaji kumbukumbu za mitihani kwa njia ya kompyuta *(Examinations Database),* kwa ajili ya mitihani yote itakayotolewa na kuidhinishwa na Baraza kuhusiana na elimu na mafunzo ya ufundi; na

- Kuimarisha ushirikiano na baadhi ya taasisi za ndani na nje zilizo na majukumu yanayofanana na ya Baraza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo kwa upande wa Sayansi na Teknolojia:-

- Kuhuisha Sheria Na. 7 ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia;

- Kukamilisha mipango ya kuanzisha vituo vya sayansi *(Science Parks);*

- Kuanzisha Kituo cha *Millenium Science Initiative (MSI);*

- Kukamilisha mashirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuhusu Mradi wa Nishati ya Jua utakaotekelezwa katika Kijiji cha Mwasayi, Wilayani Maswa;

- Kukamilisha uanzishwaji wa kamati za sayansi na teknolojia nchini;

- Kuanzisha Taasisi ya kujenga uwezo wa maarifa na kuendeleza sayansi na teknolojia nchini itakayojulikana kwa jina la Taasisi ya Nelson Mandela Arusha;

- Kuendelea na maandalizi ya kutunga Sera ya Taifa ya Utafiti;

- Kuandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Bioteknolojia;

- Kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa makubaliano na mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa katika Sayansi na Teknolojia mfano ni Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Uswiss;

- Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Sayansi na Teknolojia nchini *(Outreach Projects);*

- Kutoa mapendekekezo ya kuweka utaratibu wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mashirikiano na kutoa mapendekezo ya kuboresha;

- Kuendelea kuandaa mwongozo na kutunga sera ya wabunifu, wagunduzi na wavumbuzi;

- Kuendelea kuelimisha jamii kupitia Redio na Televisheni kuhusu sayansi na teknolojia;

- Kuendelea kutoa msukumo kwa wasichana wachukue masomo ya sayansi na teknolojia kwa kutoa zawadi na kuwalipia karo; na

- Kuandaa nyaraka za kuridhia Mikataba iliyo chini ya *IAEA* kama ifuatavyo: *Joint Convention on the Safety of Spent Fuel Management and on the Safety of Radioactive Waste Management* na *African Nuclear Weapon Free (Pelindaba Treaty);*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza yafuatayo:-

- Kusambaza teknolojia ya matumizi ya makaa ya mawe yaliyoboreshwa kwa matumizi ya nyumbani kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* na watu binafsi;

- Kuhawilisha matumizi ya gesi ya samadi kwenye magereza, pamoja na jiko bora la mkaa kwenye wilaya sita za mikoa ya kati;

- Kuhawilisha teknolojia ya matumizi ya nishati ya jua na upepo kwa kuweka mtambo mmoja unaofanya kazi kutumia jua na upepo kwa pamoja huko *Olduvai Gorge (Mary Leakey's Camp);*

- Kuhawilisha teknolojia ya ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu;

- Kuunganisha ugunduzi wa pampu inayoendeshwa kwa mkono na nishati ya upepo ya gharama nafuu, kwa ajili ya kuvuta maji kutoka visima virefu mkoani Iringa;

- Kusimamia ufufuaji upya wa chama cha wagunduzi *(TAI)* na Chama cha Walimu wa Sayansi Tanzania *(STAURT);*

- Kuimarisha asasi mpya ya mambo ya asilia. *LINKS - Local/Indigenous Knowledge System Trust;*

- Kutoa mafunzo juu ya haki miliki na ubunifu kwa watafiti na wagunduzi;

- Kuendeleza masjala ya utafiti;

- Kuendelea kufadhili miradi ya utafiti na kutoa mafunzo kwa watafiti juu ya utayarishaji wa miradi ya utafiti; na

- Kusambaza matokeo ya tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Tume ya Taifa ya Mionzi itatekeleza yafuatayo:-

- Kufanya ukaguzi wa minara ya simu za mikononi, migodi na mazingira ili kubaini viwango vya mionzi na hali ya usalama;

- Kuendelea kutekeleza sheria ndogo ya kudhibiti viwango vya mionzi kwenye vyakula *(Protection from Radiation, Control of Radiation Contaminated Foodstuffs Regulations, 1998),* kwa kupima sampuli za vyakula viingiavyo na kutoka nje ya nchi;

- Kuratibu uanzishaji na usimamizi wa kituo cha kuthibiti majaribio ya silaha za nyuklia *(Comprehensive Test Ban Treaty of Nuclear Weapons-CTBT);*

- Kuratibu misaada ya zaidi ya *USD* 900,000 kwa Taasisi naneza Kitaifa kupitia miradi ya Kitaifa na Kikanda (Afrika) inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA);*

- Kutoa elimu ya kinga ya mionzi kwa wafanyakazi wanaohusika na kuendelea na utafiti wa madhara ya mionzi kwa nia ya kubuni mbinu nzuri ya matumizi salama ya mionzi katika vituo vyote na kutoa elimu ya kinga ya mionzi kwa umma kwa njia ya redio, televisheni na semina;

- Kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge, wafanyakazi wa mionzi na umma kuhusu shughuli za Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania *(Tanzania Atomic Energy Commssion-TAEC);*

- Kuimarisha huduma za matengenezo ya vifaa vya elektroniki na mashine za *X-ray;*

- Kukamilisha mpango wa kushughulikia dharura za mionzi Kitaifa *(Radiological Emergency Plan and Preparedness)* na usalama wa vyanzo vya mionzi *(Security of Radioactive Sources);* na

- Kuanzisha ofisi ndogo Zanzibar katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na Sheria ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kufikia mwaka 2025, ni kujenga jamii iliyoelimika yenye uwiano wa kijinsia na inayoweza kujiletea maendeleo kwa kutumia sayansi na teknolojia. Ili kufanikisha azma yake, Wizara katika mwaka wa fedha 2005/2006 inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu utekelezaji wa miradi inayoendelea na ile itakayoidhinishwa katika kipindi cha mwaka 2005/2006;
- Kuelimisha wanafunzi kuhusu nafasi za elimu ya juu nchini na nje ya nchi;

- Kuelimisha wadau kuhusu upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundi;

- Kutathmini na kuhuisha Sera ya Elimu ya Juu na kutoa mapendekezo ya kuboresha;

- Kuendeleza udhamini wa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari katika Vyuo Vikuu binafsi na wanafunzi wa udhamini binafsi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili. Kwa mwaka 2005/2006, Wizara itadhamini wanafunzi 424 (168 wa mwaka wa kwanza na 256 wanaoendelea);

- Kudhamini wafanyakazi na wanataaluma 209 katika Vyuo Vikuu kwa Shahada za Uzamili na Shahada za Juu za Falsafa;

- Kununua na kufunga mashine na mitambo katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MIST),* kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo;

- Kugharamia mafunzo ya watumishi 27 wa Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Makao Makuu katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa wanane, Shahada ya Uzamili 14, *Diploma* ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi watano;

- Kuratibu utekelezaji wa miradi inayoendelea na ile itakayoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa *UNESCO* Januari, 2006;

- Kukamilisha mipango ya kuanzisha vituo vya sayansi *(Science Parks);*

- Kukamilisha uanzishwaji wa Kamati za Sayansi na Teknolojia nchini;

- Kuanzisha Taasisi ya kujenga uwezo wa maarifa na kuendeleza sayansi na teknolojia nchini itakayojulikana kwa jina la Taasisi ya Nelson Mandela Arusha;

- Kuanzisha Kituo cha *Millenium Science Initiative (MSI);*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani na wadau mbalimbali kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika Wizara yangu. Ni dhahiri kuwa msaada walioutoa na wanaoendelea kutoa hususan katika kuboresha sayansi na teknolojia, elimu ya juu na ufundi, katika vyuo na taasisi, umesaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia pale ambapo Serikali imekuwa ikishindwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Nchi hizo ni pamoja na Norway, Sweden, Uholanzi, Japan, Ubelgiji, Canada, Jamhuri ya Korea, Jamhuri ya watu wa China na Umoja wa Nchi za Ulaya.

Aidha, mashirika ni pamoja na Benki ya Dunia, *UNESCO* na Shirika la Maendeleo la Sweden *Sida/SAREC, Carnegie Foundation* na *DANIDA.* Naomba waendelee na moyo huo, nasi tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2005/2006, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 138,058,526,400/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 111,113,449,700/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 26,945,076,700/= ni kwa matumizi ya maendeleo.

Mwisho kabisa, nachukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutimiza masharti yaliyomokwenye kanuni ya 81 (1), toleo la 2004 ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii, uliyoipa jukumu la kuchambua taarifa za utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2004/2005 na kupitia malengo ya makadirio ya Wizara hiyo kwa mwaka wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii, ilichambua na kujadili maeneo yafuatayo: Dira na majukumu ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu; utekelezaji wa maagizo na mapendekezo ya Kamati iliyochambua bajeti ya Wizara mwaka 2004/2005 na malengo yaliyopangwa kutekelezwa na makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kujadili na kuchambua vipengele vilivyotajwa hapo juu, Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, pamoja na Naibu wake, wakisaidiwa na Timu ya Wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara, walijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati kwa ukamilifu na hivyo, Kamati inaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu Juu, iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu ili lijadili na kuidhinisha bajeti ya Wizara yake kwa mwaka wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu , Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Serikali kupitia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kamati inaunga mkono lengo la kuwezesha utoaji wa elimu iliyo bora na yenye uwiano bora wa kijinsia katika nyanja za Ufundi na Elimu ya Juu, kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mafunzo na utafiti, kuwaajiri wataalamu wenye sifa, kuweka na kudumisha kiwango cha juu cha ubora katika utekelezaji kwa kuwa na wataalamu wanaohitajika katika Taasisi kulingana na mahitaji ya jamii ya Tanzania na ulimwengu wa utandawazi.

Kamati inaipongeza Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa juhudi zinazofanywa za kujenga mazingira bora kwa ajili ya sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma za Elimu ya Juu, Ufundi, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azma ya Serikali kutekeleza sera ya kuinua maendeleo ya uzalishaji kwa kutumia sayansi nateknolojia, Kamati inayo mapendekezo na ushauri ufuatao:-

Kwamba, kiasi cha shilingi milioni 30 kilichotengwa katika bajeti ya 2005/2006 kwa ajili ya Masjala ya Taifa ya Utafiti *(National Research Registry)* ni kidogo na hivyo Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya Masjala hii katika bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii katika uhai wa miaka yote mitano sasa imekuwa ikihimiza Serikali itenge asilimia moja ya Pato la Taifa kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza utafiti na maendeleo ili kufikia lengo la kuleta mafanikio katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika Dira ya Taifa. Kulingana na Takwimu za sasa za ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 5.6, mahitaji ya fedha za utafiti kufikia lengo la asilimia moja ni karibu shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kutenga walau shilingi milioni 600 kwenye bajeti hii ya 2005/2006, ongezeko hilo ni asilimia 100 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi milioni 300 kilichotengwa mwaka 2004. Hata hivyo, mchango huu bado ni mdogo na hivyo tunashauri Wizara nyingine ziongeze mchango kwenye eneo la utafiti katika kukuza uchumi ili tufikie lengo la kutumia asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa, kauli ya Mheshimiwa Rais Mkapa kwenye uzinduzi wa Taasisi ya Sayansi Tanzania, iliyofanyika hapa Dodoma kuhusu Jumuiya ya Kimataifa kusaidia na kuzipa uhai Taasisi za Elimu ya Juu za Afrika na Vituo vya Elimu ya Sayansi na Teknolojia za Afrika ni mtazamo mpya wa Serikali katika kuongeza bajeti kwa ajili ya utafiti na maendeleo katika hatua katika kufikia matumizi ya asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine inayoonesha msukumo wa kuimarisha utafiti na maendeleo, Kamati inawapongeza Waanzilishi 25 wa Taasisi ya Sayansi Tanzania, waliotunukiwa vyeti wakiongozwa na Mheshimiwa Dr. Pius

Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kutunukiwa hadhi ya kuwa Mwanachama wa Heshima wa Taasisi ya Sayansi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inampongeza kwa dhati Profesa Mathew Luhanga, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa Rais wa Taasisi ya Sayansi Tanzania. Tunashauri Kauli ya Mheshimiwa Rais ya kugeuza hali ya *Brain Drain into Brain Gain,* ifanyiwe kazi na kila Wizara ili Taifa lifikie walau kutumia asilimia moja ya pato lake kwenye maendeleo ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mfuko wa Elimu kaunzishwa Tanzania, Kamati ilibaini upungufu katika sheria kwa kutokuweka kiwango cha chini cha Serikali kuchangia Mfuko huu kila mwaka, Kamati imeendelea kuishauri Serikali kufanya marekebisho lakini hadi sasa hakuna marekebisho yaliyotolewa pamoja na kwamba, Wizara tayari imewasilisha Waraka wa Mapendekezo ya marekebisho haya kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri tangu Machi, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Mfuko huu hauhitaji kueleza zaidi katika kuimarisha Sekta ya Elimu. Kwa kuweka kiwango cha asilimia mbili ya Pato la Taifa baada ya kuondoa deni la Taifa, kiasi ambacho kingetegemewa kupatikana kisingepungua shilingi bilioni 43 mwaka huu wa fedha wa 2005/2006, lakini fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 6.8 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kwa mara nyingine inashauri Serikali ifikie maamuzi ya kurekebisha sheria hii kama kweli ina nia ya dhati ya kuwekeza kwenye Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijadili vilevile maendeleo ya Elimu ya Juu hapa nchini katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali iko katika hatua mbalimbali za kuboresha na kupanua Elimu ya Sekondari nchini kwa kuongeza idadi ya shule za sekondari na ubora wa elimu inayotolewa. Hali hii kwa vyovyote vile itaongeza idadi ya wanafunzi watakaokuwa na sifa ya kuingia vyuo vikuu nchini katika mwaka huu wa 2005/2006 wanafunzi wenye sifa za kuingia vyuo vikuu 22,992 kwa vyuo vikuu vya umma na vya binafsi nchini, kwa pamoja. Vyote hivi vina uwezo wa kudahili wanafunzi 16,660 ambayo ni asilimia 72.5 ya wanafunzi wenye sifa za kuingia vyuo vikuu. Hivyo, wanafunzi zaidi ya 6,000 ambao ni kama asilimia 27.5 ya wenye sifa hawatadahiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa takwimu hizi zinaonesha kuwa, Serikali imepiga hatua kubwa katika suala zima la udahili, pamoja na mafanikio haya kutokana na mpango wa elimu wa shule za Sekondari (MMES), kutakuwa na idadi kubwa ya wahitimu wa shule za sekondari hivyo ni vema Serikali ikaendelea kuongeza na kuboresha Vyuo Vikuu vyake na kujenga mazingira mazuri kwa vyuo vikuu binafsi ili kupanua wigo wa udahili wa wahitimu wa Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yanayojitokeza sasa katika Vyuo Vikuu vya Umma, hivi karibuni viongozi wa wanafunzi wa vyuo vikuu vya umma walikutana kujadili matatizo yanayowabili katika vyuo vya umma. Viongozi hao wamewasilisha kwa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na kwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, waraka mfupi unaoeleza matatizo yafuatayo:-

Kwanza, mfumo mzima wa Bodi ya Mikopo *(Loan Board),* haueleweki jinsi utakavyofanya kazi, ikiwa ni pamoja na utoaji *form,* uwakilishi wa Vyuo ndani ya Bodi hiyo, Idadi ya wanafunzi watakaopata mikopo na vigezo vitakavyotumika kuwapata wanafunzi watakaostahili mikopo hiyo. Hata hivyo, jana niliona Bodi ya Mikopo ikiwa imetoa matangazo kwenye magazeti.

Pili, wanachuo kushindwa kumudu gharama za kuishi wanapokuwa vyuoni na wanapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo nje ya vyuo vyao kutokana na viwango vya sasa shilingi 2,500 vya tangu 2001 kuwa vidogo kwa vile vimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama zinazokaribia hali halisi kwa siku kwa ajili ya kifungua kinywa, chakula cha mchana, jioni na usafiri kwa wanafunzi wanaoishi nje ya chuo ni wastani wa shilingi 5,000 kwa siku kwa maelezo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na hoja kuwa viwango vya posho hizo vimepitwa na wakati, kwani viliwekwa mwaka 2001, hivyo viangaliwe upya ili wanachuo waweze kukabiliana na gharama zilizopanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi, ikutane na Viongozi wa Vyuo Vikuu vya Umma, kwa lengo la kuelimishana kuhusu Sheria ya Bodi ya Mikopo na taratibu zake. Aidha, tunapendekeza wanachuo wa vyuo vyote nchini, waelimishwe juu ya utaratibu huo. Tunashauri jambo hili litekelezwe kabla ya mihula ya Vyuo Vikuu kuanza ili walengwa waweze kukamilisha taratibu zinazotakiwa na kuepuka usumbufu. Vilevile tunashauri Serikali ikamilishe uteuzi wa mwakilishi kutoka Vyuo Vikuu katika Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri vilevile Waraka wa Viongozi wa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania kuhusu matatizo na mapendekezo kwa Serikali ni vema ufanyiwe kazi mapema iwezekanavyo. Hapa namsikia Mheshimiwa Waziri akisema tayari ameshafanya uteuzi wa mwakilishi kutoka Vyuo Vikuu kwenye Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine Morogoro *(SUA),* Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe utoaji wa hati miliki kwa eneo la Mazimbu ili mikakati ya kuendeleza miundombinu ya eneo hilo isipate kipingamizi chochote cha kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Hospitali ya Taifa Muhimbili kutenganishwa na Chuo Kikuu kishiriki cha Sayansi za Afya cha Muhimbili ni vema Serikali ikaangalia mgawanyo sahihi wa mali zilizokuwa zikimilikiwa kwa pamoja na Taasisi hizo mbili,

ikiwemo hati za kumiliki ardhi katika maeneo hayo. Pia ni vizuri zoezi hili likamalizika mapema kwa faida ya maendeleoya kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro uliojitokeza Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT),* hivi karibuni na Kamati ilipokea maelezo kutoka kwa wanafunzi na uongozi wa Taasisi kuhusu chanzo cha mgogoro. Sote tunafahamu kuwa migogoro inavuruga mambo mengi ikiwa ni pamoja na bajeti ya Serikali, muda wa mafunzo na vilevile migogoro inaondoa ufanisi katika vyuo, hivyo, Kamati imeona ni vema sasa migogoro imalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha mgogoro wa wanafunzi *DIT,* tunanukuu maelezo ya wanafunzi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuona pande zote. Nukuu ya maelezo ya wanafunzi inasema hivi: "Ukiukwaji wa Sheria ya *DIT* Namba 6 ya 1997 na Mitaala ya Taasisi. Sehemu ya pili kifungu cha 4 (1) (g) cha sheria kinaipa mamlaka Taasisi kujitungia mitihani yake yenyewe na kutoa tuzo zake yenyewe. Badala yake *DIT* imekuwa haifanyi hivyo na kuendelea kutegemea mitihani toka Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA),* ambapo mitihani hiyo imekuwa na matatizo na mapungufu mengi kwa mfano, wanatoa mwaka huu wanafunzi wa *FTC* mwaka wa pili *Civil Engineering* waliletewa na kulazimishwa kufanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu baadala ya Mtihani wa *FTC*. Aidha, vyeti vitolewavyo na *NECTA* havina hadhi ya Elimu ya Juu kwani havioneshi masomo, alama za kufaulu wala daraja la cheti".

Katika nukuu ya pili, wanazungumzia Tasnifu *(Final Projects)* kwamba: "Mitaala ya Stashahada ya Juu Uhandisi inaeleza wazi kwamba, Tasnifu, yaani *Final Projects* itafanyika Muhula wa Nne unaojitegemea wa mwaka wa Tatu wa Masomo, badala yake Taasisi imeondoa muhula wa nne kwa kufanya Tasnifu na imekuwa ikilazimisha Tasnifu hiyo kufanyika ndani ya mihula mitatu ya masomo ya nadharia".

Pili wanaeleza ukiukwaji wa mikataba baina ya wanafunzi na Mdhamini au mfadhiri wao. Wanafunzi wamekuwa wakipewa fedha zao za mikopo kiwango pungufu na kile kinachoainishwa kwenye Mikataba kwa mfano, Juni, 2004, wanafunzi wote wa *FTC* na *ADE,* kwa pamoja walikatwa zaidi ya shilingi milioni 29 za mafunzo viwandani *(Industrial Practical Training - IPT)* bila maelezo yoyote, baada ya mgomo wa wanafunzi wa siku tatu walirejeshewa fedha hiyo.

Wanafunzi wa mwaka wa tatu wamekuwa wakilipwa posho zao za chakula na malazi pungufu na kiwango cha kwenye Mkataba. Mwaka huu wanafunzi wa Shahada ya Uhandisi wamepunguziwa muda wao wa mafunzo viwandani tofauti na mkataba wao.

Tatu, wanaeleza migomo isiyoisha. Menejimenti ya Taasisi imekuwa haitekelezi majukumu yake ipasavyo mpaka kunapotokea migomo kwa mfano, kuanzia Januari, 2004 hadi Mei, 2005 kumetokea migomo isiyopungua saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa Taasisi umekuwa hautoi ushirikiano wa kutosha kwa wanafunzi hasa kwenye mambo muhimu yanayowahusu, wanafunzi wamekuwa hawashirikishwi kwenye vikao muhimu vya ndani na nje ya Taasisi, kwa

mfano, Mwakilishi wa Wanafunzi hakualikwa kwenye Baraza la Taasisi katika vikao viwili vya tarehe 13 Mei, 2005 na tarehe 27 Mei, 2005 vilivyokuwa vikihusu mgogoro huo.

Mapendekezo ya Wanafunzi, kwa kuwa *DIT* imepata usajili, imepata Ithibati na ina mfumo wa kudhibiti ubora wa mafunzo na uendeshaji wa mitihani na utoaji wa tuzo unaokubalika na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na kwa kuwa Sheria ya *DIT* Namba 6 ya 1997 na ile ya *NACTE* ya mwaka 1997, hazina uhusiano wowote wa Sheria ya *NECTA* ya mwaka 1973, hivyo basi, Taasisi itoe tuzo kwa wahitimu wa *FTC* na *ADE* kutokana na mitihani yake yenyewe kama ilivyoainishwa kwenye Sheria na mitaala ya *DIT* na pia Tasnifu kufanyika kama ilivyoainishwa kwenye mitaala.

Kuhusu migogoro ya mara kwa mara, kwa kuwa uongozi wa Taasisi umeshindwa kutekeleza Sheria ya *DIT* kuzingatia mitaala yake yenyewe kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu na kadhalika na hivyo kupelekea migogoro isiyoisha ndani ya Taasisi. Tunaiomba Serikali ifanye mabadiliko ya uongozi mapema iwezekanavyo ili kudumisha hali ya amani na utulivu ndani ya Taasisi na hivyo kuboresha utoaji wa elimu kwa maslahi ya Taifa.

Tatu, wanafunzi wanasema tunaiomba Serikali itoe ufafanuzi juu ya Programu za *Full Technician Certificate (FTC)* na *Advanced Diploma in Engineering (ADE),* kwani kwa mujibu wa *NACTE*,programu hizi siyo zao na wala si za *DIT,* badala yake taarifa za upotoshaji zinatolewa kwa Umma na Taasisi kuwa, wanafunzi wa *ADE* wanataka Shahada ya Uhandisi, jambo ambalo si la kweli.

Nne, wanasema wanaiomba Serikali iwaite chuoni wanafunzi wote mapema iwezekanavyo, kwa mujibu wa makubaliano ya tarehe 19 Mei, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Taasisi ya *DIT* yanasema hivi: "Sheria iliyoanzisha *DIT Act No. 6* ya 1997, *Part II ( 4)(g),* inatoa mamlaka kwa Taasisi kutunga mitihani na kutoa tuzo pale tu idhini ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *NACTE* inapotolewa".

Pili, ili Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* liweze kutoa idhini ya kutunga mitihani na kutoa tuzo kulingana na Sheria Namba 9 ya mwaka 1997 vifungu vya 5 (a) na (e) na 11, inabidi Taasisi iwe imepata usajili, ithibati na iwe na mfumo wa kudhibiti ubora wa mafunzo na mfumo wa uendeshaji mitihani na utoaji tuzo unaokubalika na Baraza la Mitihani na utoaji wa tuzo unaokubalika na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* iwe na mitaala inayozingatia umahiri *(Competence Based),* iliyoidhinishwa na *NACTE,* iwe na idara zenye kutoa mafunzo kwa kuzingatia sifa za walimu na vifaa vya kutosha vya kufundishia.

Tatu, mitihani na tuzo za stashahada ya juu ya Uhandisi viko chini ya Baraza la Mitihani ya Tanzania *(NECTA)*, kulingana na Sheria Namba 21 ya *NECTA.*

Nne, ili chuo kiweze kutekeleza masharti ya utungaji mitihani na utoaji tuzo, ilibidi pawe na matayarisho ya kutosha kujenga uwezo wa kutunga mitihani.

Tano, Taasisi ilipewa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Septemba, 2004 baada ya kutimiza masharti muhimu ya ithibati na hivyo kuruhusiwa kuanzisha mafunzo ya Shahada ya Uhandisi *(Bachelor of Engineering),* kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na kuendelea na programu za zamani za Stashahada ya Juu ya Uhandisi.

Sita, Mitihani na Tuzo za Stashahada ya juu ya Uhandisi imeendelea kutolewa na Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, Sheria za *DIT* na *NACTE* hazikufuta jukumu la kutunga na kutoa tuzo hizo kutoka *NECTA.*

Pili, imechukua muda mrefu kwa *DIT* kujenga uwezo wa kutunga mitihani na kutoa tuzo zake.

Tatu, hata baada ya *DIT* kujenga uwezo wa kutunga mitihani na kutoa tuzo zake, bado imonekana kuwa kitaaluma si busara kuhamisha mitihani na tuzo za programu hizo kutoka *NECTA,* ambao wamekuwa wanazisimamia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa migogoro mingi katika Taasisi hiyo ni dhahiri kuwa kuna matatizo yanayotakiwa kuangaliwa kwa kina na ngazi zote zinazohusika na Taasisi hiyo. Kamati inampongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuunda Tume ya kushughulikia matatizo ya *DIT* na hivyo, tunashauri Jumuiya ya *DIT* sasa ifahamu matokeo yake na hatua zichukuliwe kumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wizara itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ili Taasisi hii iweze kufikia hadhi iliyokusudiwa. Kipindi cha Mpito cha kubadilisha hadhi ya *DIT* ni lazima kabisa kifuate kwa ukamilifu, urekebishwaji wa Sheria Namba 9 ya 1997 ili *DIT* iwe na uwezo wa utoaji wa taaluma na tuzo zinazokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa katika kipindi cha mpito, ikamilishe yote yanayotakiwa kisheria ili wale waliodahiliwa kwa mafunzo rasmi ya Shahada ya Uhandisi, waweze kupewa tuzo hiyo watakapomaliza masomo yao. Serikali sasa iepuke kuanzisha Taasisi zozote kabla ya kufanya matayarisho muhimu hasa yanayohitaji mabadiliko ya Sheria hii, itaondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha utandawazi, Serikali isimamie kwa ukaribu Elimu ya Juu katika utoaji wa mafunzo na tuzo zinazokubalika kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi ili kuweza kuukabili ushindani wa soko la ajira kwa wahitimu wa Taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafsi hii na pia Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu,

Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Zabein Mhita, ambao kwa mujibu wa kanuni ya 87 kifungu cha kwanza, walikuwa ni Wajumbe wa Kamati yangu, wakati wa kujadili na kuchambua utekelezaji wa Wizara yao kwa mwaka 2004/2005, pia tunawashukuru kwa ushirikiano wao tulioupata wakati tunachambua bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2005/2006. Aidha, nawashukuru wataalam wote wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Ruth Molel, kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujibu hoja na maswali wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa umakini na ushirikiano wao mkubwa wakati wa kujadili fungu hili na sasa naomba niwatambue kwa majina. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, pamoja nami, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya pekee, niwashukuru kwa dhati Wananchi wa Jimbo la Babati Mashariki, ambao walinipa ridhaa ya kuwatumikia katika kipindi kinachomalizika sasa. Kwa kuwa makazi ya sasa yameangukia kwenye Jimbo jipya la Babati Mjini, ni imani yangu kuwa wana-CCM na Wananchi wa Jimbo jipya la Babati Mjini, nao watanipa ridhaa ya kuwa mtumishi wao kwa kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Katibu wa Bunge na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Theonest Ruhilabake, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. Mwisho, nachukua fursa hii, kukupongeza wewe, pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kutuongoza vizuri katika kipindi chote cha miaka mitano na tunawatakia afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ningependa tu kwa ajili ya kujiandaa, tunao wachangiaji 13 na wa mwanzo watatu ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa. Hawa wajiandae ndiyo wataanza kuchangia. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na

Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la 2004.

Kwa kuwa leo ni mara yangu ya pili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni katika Mkutano huo wa 20 na nilikwishapata nafasi ya kutoa salamu za rambirambi, kwa familia na jamaa za Waheshimiwa Wabunge, walioiaga dunia kabla ya Mkutano huu wa 20 kuanza, leo ningependa kutoa salamu za rambirambi kwa familia na jamaa za Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyeaga dunia wakati Mkutano huu wa 20 wa Bunge ukiendelea. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikwishatoa salamu za pongezi kwa wanachama wa vyama vya siasa walioteuliwa na vyama vyao kuviwakilisha katika kinyang’anyiro cha Urais na Umakamu wa Rais katika Uchaguzi Mkuu wa 2005. Kwa sababu hiyo, sasa nichukue nafasi niwapongeze Mheshimiwa Dr. Pius Ng’wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Viongozi wote wa Wizara, pamoja na Makamu wa Wakuu wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu, kwa kazi zao nzuri wanazozifanya katika mazingira magumu kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzungumzia matatizo na mafanikio ya Wizara hii, hasa kwa upande wa Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu, nitajaribu kuikumbusha Wizara na Serikali, maoni na ushauri tuliokwisha kuutoa kwa Wizara katika hotuba nne za bajeti za miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/2005, nilizungumzia juu ya Programu na Mipango Kabambe au *Master Plan* ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu na wanafunzi wake kwa awamu ya miaka mitano mitano. Japo, Mheshimiwa Dr. Pius Ng’wandu, alikwishasema kuwa, Wizara yake ilikwishaandaa programu hiyo kwa miaka mitatu iliyopita, inasikitisha kuwa mpaka Bunge litakapovunjwa tarehe 29 Julai, 2005, hakuna hata Mbunge mmoja ambaye amewahi kuiona programu hiyo, wala hakuna semina yoyote iliyowahi kutolewa na Wizara kuhusu programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kwa mwaka wa fedha 2004/2005, tuliishauri Wizara na Serikali kuanza mara moja kuweka maandalizi ya kupanua Vyuo Vikuu kwa kutumia matarajio na matokeo ya Mpango wa Maendeleo ya Shule za Msingi - MMEM na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari - MMES, kwani tulitarajia kuwa, kwa kutumia takwimu za idadi ya wanafunzi wanaoingia shule za msingi na wale wanaotarajia kuingia na kumaliza Shule za Sekondari za Kati na za juu, Serikali ingekuwa imeshaanza kuweka rasilimali fedha na rasilimali watu, zinazotakiwa katika kuendeleza Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Makadirio ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kuwa kutakuwa na wanafunzi 2,000,000 katika shule za sekondari ifikapo mwaka 2010 na wahitimu wa sekondari wasiopungua 500,000 kila mwaka, bila shaka katika shule za sekondari za juu kutakuwa na wahitimu 250,000 kila mwaka. Hivyo, kutokana na

takwimu za Wizara ya Elimu na Utamaduni katika kitabu chao cha *Basic Statistics in Education 1995 - 2004,* kwa matokeo ya mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2003, asilimia za ushindi kwa *division one* 16.5 na *division two* 30.8 hivyo, kama hali ikiendelea hivyo ni dhahiri kuwa, kati ya wanafunzi 250,000 watakaomaliza Kidato cha IV zaidi ya 125,000 watakuwa wanapaswa kuingia Vyuo Vikuu kila mwaka. Idadi hiyo itakuwa kubwa na hivyo kuthibitisha uhalali na ukweli wa kuwa na Chuo Kikuu kila Mkoa wa Tanzania Bara, kwani ikiwa kufikia mwaka 2014, kutakuwa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu 500,000 nchini Tanzania, tukiwa na Vyuo Vikuu 21 na kila Chuo kikawa na wastani wa wanachuo 20,000, litakuwa jambo linalowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizo hapo juu, pamoja na mafunzo tuliyoyapata kutokana na maandalizi hafifu ya mipango ya MMEM na MMES, kama nitakavyoyataja hapo chini, ili kufanikisha Mpango wa Maendeleo wa Vyuo vya Elimu ya Juu ni lazima tuanze mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa kufanya mambo katika dakika za mwisho za majeruhi yafuatayo yamejitokeza: Uhaba wa walimu kwa shule za msingi na walimu wapya kusomea ualimu kwa mwaka mmoja badala ya miaka miwili na uhaba wa walimu kwa shule za sekondari, ambapo Wizara imeamua kuwapa kozi ya wiki tatu vijana waliomaliza kidato cha sita ili kufundisha Sekondari!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tutakapoanza kuingiza wanafunzi wengi wa Vyuo Vikuu, je, Wahadhiri nao watakuwa wanachukuliwa wahitimu wa shahada ya kwanza na kupewa mafunzo ya miezi sita ili sasa wawe *Senior Lecturers?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu alizozitoa Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, katika hotuba yake ya bajeti ya 2005/2006 katika Kiambatanisho kinachosomeka "Piramidi Bora ya Elimu 2010", anaonesha kuwa asilimia 12.5 ya wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Sita, wanaokaribia 250,000 watakuwa wanaingia Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna miaka mitano tu kutoka sasa hadi 2010 na suala la Elimu ya Juu haliwezi kuchukuliwa kama lile la Shule za Msingi na Sekondari kwa sababu Serikali ilipotaka walimu wa Shule za Msingi, wengi walikuwepo kwenye mfumo kwa vile ajira ilikuwa imesitishwa, wanafunzi wa kwenda kwenye vyuo vya ualimu kwa mwaka mmoja walikuwepo wengi, waliokuwa wamemaliza Kidato cha Nne na hata wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita wataochukua kozi ya wiki tatu wapo wengi. Swali je, walimu wa kufundisha katika Vyuo Vikuu nao wako wengi kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na masuala haya, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuharakisha utekelezaji wa mambo ambayo ni ya muhimu kabla ya wakati uliotegemewa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo Aprili, 2004, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *The Higher Education Students' Loans Board,* kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, mwaka mmoja sasa umepita tangu sheria hiyo

ilipopitishwa na Bunge, lakini imechukua muda mrefu kwa Wizara kutunga kanuni za kuendesha Mfuko huo kwa kiasi kwamba, yafuatayo yamejitokeza: Wanafunzi wanaotegemewa kuanza masomo ya Vyuo Vikuu Agosti 2005, hawajui utaratibu wa kukopa na wala fomu za mikopo hazijatolewa; Serikali haijatangaza kwenye vyombo vya habari kuhusu taratibu, masharti, wahusika na namna mikopo hiyo itakavyotolewa na pia Serikali haijawahakikishia wanafunzi na Wananchi kwa ujumla, kiasi cha fedha na uwezo wa idadi ya wanafunzi wanaoweza kuhudumiwa na Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba, wakati naandaa hotuba hii kuna matangazo yalikuwa hayajatolewa. Kwa hiyo, kuna maendeleo ambayo kufikia hivi sasa ninavyozungumza yametoka na kwa hiyo namshukuru Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kutoka kwa wawakilishi wa wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Umma nchini, waliotaka kujua kama wako wanafunzi waliokuwa chini ya udhamini wa Serikali kwa Mkataba na Serikali, je, wangekatisha Mkataba huo? Nakumbuka Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, alisema kuwa, Mkataba wao utaendelea kama ulivyo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, aweke mambo haya bayana kupitia vyombo vya habari, kuliko kuwanyima wanafunzi taarifa na kuja kutoa taarifa baada ya wanafunzi kugoma. Tunashukuru tu kwamba, taarifa hii imetolewa wakati Mwenyekiti wa Kamati akisoma maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Umma, Serikali ilipitisha viwango vya posho ya chakula Sh. 2,500/=, posho ya usafiri Sh. 500/= na posho ya Malazi Sh. 600/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa, posho hizo zilipitishwa tangu mwaka 2001 na tangu wakati huo, Serikali imefanya marekebisho kadhaa kwa watumishi wa Serikali, kuanzia posho za vikao, posho za kujikimu kwa safari ndani ya nchi na vilevile marekebisho kwa watumishi wa Serikali wanaosafiri kwenda nchi za nje yamefanyika na kuboreshwa katika posho ya kujikimu nje ya nchi, posho ya mavazi *(Outfit Allowance)* kwa kiwango cha kuridhisha. Sasa katika zama hizi za uwazi na ukweli na usawa, kwa nini Serikali haiwezi kufanya marekebisho katika posho za wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Kwanza, hata hivyo posho hizo wanazopewa wanafunzi ni mkopo na watazirejesha. Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa, Wizara na siyo Serikali kwa ujumla wake, inayo mapendekezo yaliyotolewa hivi karibuni na wanafunzi wa Vyuo Vikuu, tunaiomba Serikali iyapokee na kuyakubali ili kuwawekea mazingira mazuri wanafunzi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya Umma kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vinayo malalamiko kuwa Serikali inachelewesha utekelezaji wa mpango wa gharama halisi za mafunzo kwa kila mwanafunzi wa Chuo Kikuu. Ikumbukwe kuwa hata kwa Shule za Msingi sasa Serikali inatoa dola 10 kwa kila kichwa cha mwanafunzi kwa ajili ya *capitation grant,* tunaomba Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ifuate utaratibu huu na kutoa fedha kulingana na idadi ya wanafunzi walioko katika kila Chuo Kikuu cha Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka kuwa, hivi karibuni kumekuwa na migomo na migogoro katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam. Chanzo cha migogoro ni kutotekelezwa kwa Sheria ya Na.6 ya 1997, kuhusu Chuo kutunga mitihani yake. Hii ni kutokana na Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* kutumia sheria iliyolianzisha mwaka 1973, kuendelea kuhodhi madaraka ya kutunga mitihani ya *DIT*. Kufuatana na mkanganyiko huo kumekuwa na utata wa nani anapaswa kutunga mtihani wa Chuo cha *DIT;* nani anapaswa kutoa vyeti vya *DIT* naVyeti vinavyotolewa vitambulike namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupuuzwa matakwa ya Sheria ya *DIT* ya 1997, *NACTE* wamekuwa wakijiita *Autonomous Body,* aidha kumekuwepo na uzembe kwa viongozi wa *DIT* na Wizara katika kuhakikisha kuwa *DIT* wanapata Ithibati *(Accreditation).* Kitendo ambacho kingehalalisha *DIT* kutunga mitihani yao wenyewe na kutoa vyeti vyao wenyewe. Kwa hali hiyo, sasa ni miaka minane tangu Sheria ya *DIT* ya 1997 imetungwa bila kufanyiwa kazi kikamilifu. Wanafunzi siyo watendaji na hawakuwajibika kusimamia utekelezwaji wa vifungu vya sheria hiyo. Hivyo, hawawezi kulaumiwa kwa kudai haki zao zilizomo ndani ya Sheria Na. 6 ya mwaka 1997 ya *DIT. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na vurugu hizo mfano tarehe 9 Mei, 2005, wanafunzi wa mwaka wa tatu wa *Civil Department* wa *DIT,* waliletewa mtihani wa somo la *Soil Mechanics and Foundation,* ambao ni kwa ajili ya wanafunzi wa *diploma* ya ualimu badala ya mtihani wa *Soil Mechanics,* ambao ndio wanapaswa kufanya wanafunzi wa Chuo hicho. Katika mtihani huo kulionekana maelezo yaliyoonesha kuwa, mtihani ulikuwa na sehemu mbili (a) na (b), kumbe kwa ndani ulikuwa na sehemu moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inazo taarifa kuwa hata Walimu wa *DIT* wanayo malalamiko ya kutopandishwa madaraja na kutolipwa baadhi ya posho zao kwa kipindi cha miaka kumi sasa. Tunaiomba Serikali, iyafanyie uchunguzi malalamiko hayo na kuyaondoa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa nne, Kambi ya Upinzani ikiendelea kuishauri Serikali kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Sayansi na Teknolojia hasa katika kutoa pesa za kutosha katika utafiti na maendeleo *(Research and Development),* lakini ushauri wote huu umekuwa ukiangukia kwenye masikio kiziwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelezwa kwenye Dira ya Taifa kuwa kufikia mwaka 2025, Tanzania itakuwa imejenga jamii iliyoelimika na ya kisasa katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia ili kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kujinukuu mara mbili,wakati nikitoa mawazo ya Kambi ya Upinzani hapa Bungeni katika bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, nilisema hivi: “Lakini Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na udhati, dhamira na uwezo wa Serikali yetu wa kuweka matendoni, yale yote yaliyoainishwa katika Dira hii na hii inatokana na ufinyu wa fedha zinazotolewa kwa

Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hasa fedha za utafiti na maendeleo; tafsiri finyu ya Wizara hii, kwa dhana ya kuiangalia katika muktadha wa Elimu ya Juu tu na leo naongeza jambo lingine ambalo ni ukosefu wa utashi wa kisiasa wa kutoa rasilimali na fedha za kutosha kwa ajili ya Utafiti, Sayansi na Teknolojia".

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuwepo kwa maarifa katika sayansi, iwe sayansi ya jamii au asilia, kumekuwepo na kanuni za kufanyia kazi ili kutimiza malengo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zilizoendelea katika kupanga vipaumbele vya shughuli zao za kijamii na kiuchumi wanakuwa na kanuni ya kutumia ili kupanga bajeti zao. Mfano uko Marekani, Ulaya, Japan, Uchina, India, wanazo kanuni za kujua kuwa katika Pato la Taifa ni asilimia ngapi itumike katika masuala ya Utafiti na Maendeleo.

(i) Hivi sasa inaeleweka wazi kuwa nchi zinazoendelea zinatoa 20% ya fedha zote zinazotumika katika Utafiti na Maendeleo na huku nchi zilizoendelea zikichangia 80% katika katika shughuli za Utafiti na Maendeleo Duniani; Kanda ya Amerika Kaskazini inatoa asilimia 37.7, Kanda ya Ulaya inatoa asilimia 27.2, Kanda ya Asia inatoa asilimia 30.5, Kanda ya *Latin America* na *Carribean* asilimia 2.9 na Kanda ya Afrika asilimia 0.6. Kwa kuzingatia idadi ya watafiti duniani, nchi zinazoendelea zilichangia asilimia 28 na nchi zilizoendelea zilichangia asilimia 72 , hii ni kwa takwimu ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni inayotumiwa na nchi nyingi ya kupanga fedha za utafiti na maendeleo *(Gross Expenditure on Research and Development of the GDP),* uwiano wa matumizi katika utafiti na maendeleo kutokana na Pato la Taifa inatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ushahidi uko wazi kuwa, kadri nchi inavyotoa pesa nyingi katika eneo la utafiti na maendeleo, ndivyo inavyopata mafanikio makubwa ya kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi na kijamii. Mfano, mwaka 1997, Pato la Taifa la China lilikuwa *$PPP* 3.543 bilioni na ilikuwa imewekeza katika Utafiti na Maendeleo kiasi cha *$PPP* 21 Bilioni, ilipoongeza uwekezaji kufikia *$PPP* 50 bilioni, Pato la Taifa la China liliongezeka na kufikia *$PPP* 5,029 bilioni kwa mwaka 2000. Hii inajionesha pia katika nchi kama Japan, Marekani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kwa sasa kiashiria *(indicator),* kinachotumika sana sana katika kulinganisha Mataifa na kuelezea Sera ya Sayansi na Teknolojia ni uwiano kati ya matumizi ya fedha za utafiti na maendeleo na Pato la Taifa (*The Ratio Between GERD and GDP).* Hivi sasa nchi za Ulaya zimeamua kutumia mpaka asilimia tatu ya Pato la Taifa kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo. Israel inatumia asilimai 4.4, Sweden inatumia asilimai 3.8, India imepanga kutumia asilimia 2 ifikapo mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania, ilipitisha katika Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia 1996 kutumia asilimia moja ya Pato la Taifa. Kitu cha ajabu ni kuwa, Serikali imetenga shilingi milioni 600 tu kwa ajili ya Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH).*

Mheshimiwa Naibu Spika,Tanzania inazo Taasisi na vyombo mbalimbali vya kufanya utafiti wa Kisayansi na Kiteknolojia kama vile *Tanzania Industrial Research and Development Organization (TIRDO); Tanzania Engineering and Mechanical Design Company (TEMDO); Tanzania Automotive Technology Centre (TACT); Technology Development and Transfer Centre (TDTC); Commission for Science and Technology (COSTECH)* na *Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (CAMARTEC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wakati *The Mwalimu Nyerere Academy,* wanalalamika kwa kupewa shilingi milioni 100 ili kukarabati majengo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, imelalamikia kitendo cha Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kutenga shilingi milioni 140 kununua magari mawili ya watumishi wa Wizara hiyo na Baraza la Mawaziri liliidhinisha hivyo, wakati huo huo Wananchi wakielezwa kuwa, Serikali haina fedha za kuzipatia Taasisi za Utafiti, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linaloendana na hilo ni fedha kwa ajili ya Taasisi za Sayansi,Teknolojia na Utafiti ni idadi na maslahi ya wanasayansi watafiti. Tukitumia kigezo cha idadi ya watafiti kwa kila watu 1,000,000 kwa takwimu za mwaka 2000 katika nchi nyingine hali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ya Japan kwa kila watu 1,000,000 kuna idadi ya wanasayansi na watafiti 5,206. Marekani kwa watu 1,000,000 kuna watafiti na wanasayansi 4,006, Ulaya kwa watu 1,000,000 kuna watafiti 2,458, Uchina kwa watu 1,000,000 kuna watafiti 554, Afrika Kusini kwa watu 1,000,000 kuna watafiti 309, Afrika kwa ujumla wake kwa kila watu 1,000,000 kuna watafiti 78, Afrika chini ya Sahara kwa watu milioni 1,000,000 kuna watafiti 51, Tanzania kwa watu 1,000,000 haijulikani inawezekana wako watafiti wanne au watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutokuwa na takwimu za wanasayansi watafiti kwa Tanzania, ni jambo la busara Serikali ikaanza kuweka sensa na takwimu ya wanasayansi wake watafiti, kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kujua wako wanasayansi watafiti wangapi; mahitaji yao na idadi inayohitajika kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili wataalam au watafiti kumekuwepo na uhamiaji wa wataalam hawa kwenda nchi za nje, kama ambavyo hapa Tanzania, Serikali haina idadi ya wanasayansi wake, waliopo na waliohama, hata mimi sina idadi hiyo. Ila hoja hapa ni kuwa, wanahama kwenda kutafuta marisho ya kijani *(Green Pasture).* Mfano, imekadiriwa kuwa kati ya asilimia 40 hadi 60 ya wanasayansi watafiti wa Argentina, Chile, Colombia, Peru, walikuwa wamehamia na kufanya kazi katika nchi zenye viwanda. Lakini kinachosababisha hali hiyo ya kuhama kwa wataalam hao ni

mishahara midogo ya wataalam; mishahara midogo ya wasaidizi wao; ukosefu wa vifaa na zana za kufanyia kazi zao na mazingira magumu ya kufanyia kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matatizo katika kuunganisha Taasisi /Vyuo vya Utafiti na wenye viwanda; uhaba wa fedha za kuzalisha kwa wingi zana zinazotokana na utafiti wa wagunduzi na wavumbuzi na Wananchi watumiaji kutopata taarifa za zana zilizozalishwa, zinazoweza kuwasaidia katika kurahisisha kazi zao na kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu kuhuisha upya shughuli za Taasisi za Sayansi na Teknolojia, Serikali ifanye yafuatayo: Iunde Tume kufanya upembuzi yakinifu juu ya umuhimu, namna bora navyanzo vya fedha kwa ajili ya kuzifufua taasisi hizo; uwezekano wa kuziunganisha chini ya chombo kimoja taasisi zote za Utafiti Sayansi na Teknolojia kuliko ilivyo sasa ambavyo ziko kwenye Wizara tofauti tofauti; Serikali kutoa Waraka kwa kiasi kinachopaswa kutengwa kila bajeti kwa shughuli za Utafiti na Maendeleo na namna ya kuboresha maslahi na vifaa kwa watafiti.

Kama Serikali haiwezi kuitenga Wizara ya Sayansi na Teknolojia ikawa moja, vilevile kukawa na Wizara ya Elimu ya Juu, basi Serikali ifanye kama inavyofanya kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambavyo Jeshi la Magereza lina kasma yake. Hivyo, Idara ya Sayansi na Teknolojia iwe na kasma yake na nusu ya Bajeti ya Wizara hii iende kwa Idara hiyo ya Sayansi na Teknolojia.

Serikali kufuatia Sera yake ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, basi ilete Muswada wa Sheria ili kufanikisha utekelezwaji wa Sera hiyo. Kwa mfano, mwaka huu, kama sheria hiyo ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa ingekuwa inatumika, Idara ya Sayansi na Teknolojia ingepata zaidi ya shilingi bilioni 98 bila kuweka fedha zinazokwenda kwenye Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa tukumbuke kuwa, changamoto nyingi zinazotukabili sisi Watanzania katika maeneo ya maendeleo, uchumi, afya, elimu na kilimo endelevu, haya yote yanaweza kuwekwa katika *denominator* moja, kuwa na jamii iliyoelimika na uchumi unaotumia ujuzi, maarifa, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni siku yangu ya mwisho kuchangia katika Wizara hii, kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Masuala ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ninawashukuru kwa dhati, wapiga kura na Wananchi wote wa Jimbo la Kyerwa, kwa imani yao kubwa waliyonipa kuwawakilisha hapa Bungeni. Kama nimewawakilisha vizuri ni jukumu la Watanzania wote na Wanakyerwa kutoa uamuzi. Ninawashukuru sana kwani kwa nafasi waliyonipa, nimeona mengi, nimejifunza mengi na nimefanya mengi. Namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru tena viongozi wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hususan Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na ninamtakia

afya njema kwa vile ameamua kustaafu na tunamkaribisha katika maeneo mengine anapoweza kuitumikia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza wachangiaji wakubwa. Kwa hiyo, sasa nitawaita wale watatu wa kwanza, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Mheshimiwa Musa Lupatu pia ajiandae. Sasa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani za dhati kwa kunipa nafasi hii leo kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza na huu ukiwa ni Mkutano wa mwisho katika Bunge hili, ningependa nitoe salamu za rambirambi kwa marehemu wote, ambao katika kipindi hiki cha awamu hii wamefariki dunia na hasa wa mwisho ambaye ni Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana na kuwaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu awape nusura ili awalaze mahali pema peponi. *Amin*.

Kwa wale wote ambao ni jamii na jamaa, pamoja na sisi tuweze kuwa na subira kwa yote hayo ambayo yalijitokeza kwa vile hili ni jambo la lazima na hatujui ni kina nani watakaofuata leo na kesho. Mwenyezi Mungu atunusuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda nimshukuru sana Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa ulezi wake ambao katika muda wote nimekuwa naye katika Kamati ya Huduma za Jamii na akanifunza mengi mpaka nilipofika kuwa Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako huko kwa kushirikiana pamoja na Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tumeweza kuwa pamoja na tukachangia suala hili kwa kikamilifu kabisa mpaka hii leo amefikia kiwango cha kuwasilisha hotuba ya bajeti katika Bunge lako hili Tukufu. Kwa hiyo, namtakia kila la kheri na mafanikio katika maisha yake ya baadaye na sisi ambao tuna tamaa ya kuja tena, atuombee ili turudi tuweze kuliendesha Baraza hilo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwapongeze wafanyakazi wote kwa ujumla, pamoja na wafanyakazi wa Vyuo Vikuu vyote vya Tanzania, kwa juhudi zao ambazo wamezichukua katika muda huu katika hali ngumu ambayo imetufikisha Tanzania kuweza kuendelea kwa kiasi fulani katika Sekta hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Niwapongeze sana hasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo kwa muda wote nimeshuhudia yaliyotendeka kwa jinsi walivyosaidia kwa kushirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kuona kwamba, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea na kuwa na Vyuo Vikuu vingi zaidi kuliko ilivyokuwa navyo hivi sasa. Kwa hiyo, niipongeze tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa juhudi yake ya kuweza kufuatana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na kuona kwamba, tunaenda sambamba katika kutekeleza masuala ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe wito zaidi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hasa kufuatana na kuanzishwa kwa Chuo cha Taasisi za Sayansi za Baharini. Katika muda wote huu ambapo tumekuwepo katika Bunge, tumejitahidi kushirikiana nao na kuona kwamba, tunafikia muafaka kabisa wa kuanzisha shughuli zinazofuatana na ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Baharini kule Zanzibar sehemu ya Buyu. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali ya Zanzibar katika muda huu ambao tumebakia nao, kukamilisha shughuli zote na matatizo yote ambayo yanakikabili chuo hicho ili kuona kwamba, hatimiliki ile pamoja na madai yote ambayo sasa hivi yamekuwa ni utata kidogo, yaweze kumalizwa na taratibu za ujenzi ziweze kuendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hili ni Bunge la mwisho, ningependa vilevile nitumie fursa hii, niwashukuru Wanakikao wote wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Bunge hili, pamoja na Wajumbe wa Bunge hili, ambao wao ndiyo walionichagua kuwepo kule kwa kunipa kila ushirikiano wa kuona ninatekeleza majukumu ya Bunge hili mpaka kufikia leo tukawa tuko pamoja, natumai tutaendelea mpaka hapo tutakapomaliza kabisa na kufunga shughuli hizi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusiana na masuala ya fedha kidogo ambazo huwa zinapatikana kwa Vyuo vile. Ningeishauri sana Serikali kwamba, tunaelewa wazi kwamba, shughuli za Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ndiyo ufunguo wa kuendeleza nchi zetu hizi. Kwa hiyo, kuna kila haja ya kuona kwamba, katika bajeti zao tunapanga. Lakini wakati mwingine kunakuwa na matatizo kwamba, utoaji wa fedha unakuwa hauendi sambamba kama tulivyopanga na vilevile kuchelewa kupatikana fedha. Ningeiomba sana Serikali ilione suala hili na kuona kwamba, kuna umuhimu zaidi wa kuweza kufanikisha na kutoa fedha hizo zinazopangwa katika bajeti kwa wakati na vilevile kama ilivyoshauriwa na Vyuo mbalimbali katika nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanafunzi kuanzia mwaka huu Serikali ilikuwa na agizo au dhamira ya kuendesha masomo kwa kujumuisha wanafunzi ambao wamemaliza mwaka 2004, pamoja na wale ambao wamemaliza katika muhula huu. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba, mpaka tunafikia hatua hii, sasa hivi bado hakujawa na taarifa kamili na jambo hili linawasumbua sana wanavyuo hawaelewi waanzie wapi au wafanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaishauri sana Serikali kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, katika muda huu mfupi tuliokuwa nao, kuweza kulitafutia ufumbuzi suala hili na kuona kwamba, ikiwa bado utaratibu huu upo, walifanyie kazi suala hili. Kwa sababu vijana wanasumbuka na wanatuuliza sana suala hili linakwenda vipi na tunashindwa kutoa jawabu kufuatana na hali halisi ya mambo yanavyokwenda. Ningeomba kama kutakuwa na suala kama hili, Serikali ikiwa inalielewa mapema, ipange mipango yake mapema sana ili inapofika wakati tena kusiwe

na mvutano wa suala hili, halafu mwisho yakaja yakatufikia kwamba tunaanza kujiingiza katika suala la migomo na migongano ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni kuhusu masuala ya utafiti. Kuna msemaji hapa aliyenitangulia, alitoa takwimu za watafiti katika dunia nzima alipoona. Lakini cha kusikitisha ni kwamba, alipofika Tanzania akasema kwamba, labda Tanzania haikutajwa kwa sababu inaweza ikawa na watafiti wawili, watatu. Nataka nimfahamishe au nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania tuna watafiti wengi.

Suala lililokuwepo ni kwamba, sasa hivi Serikali tuwe na mkazo wa makusudi kuweza kutoa nyenzo kwa ajili ya kuwapa fursa watafiti hawa na kuweza kuendeleza shughuli nyingine za utafiti ambazo ndiyo ufunguo wa maendeleo katika nchi hii ya Tanzania, pamoja na Taifa zima naa Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, ningeomba tena nitumie fursa hii, niwapongeze tena Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wakuu wa Vyuo vyote vya Tanzania na kuwatakia kila la kheri na mafanikio katika maisha ili tuweze kuendeleza Taifa letu hili kwa usalama na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mawazo yangu katika Wizara hii muhimu.

Kabla sijafanya hivyo, ningependa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kutoa rambirambi kwa wenzetu wote ambao wametutangulia mbele ya haki na rambirambi hizi pia ziwafikie ndugu zao, jamaa, pamoja na wapiga kura katika majimbo mbalimbali. Naomba vilevile nitoe rambi rambi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kupotelewa na Mkuu wao wa Chuo, Marehemu Mheshimiwa Bomani, Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa ili niunge mkono hii hoja, sikuwa na jinsi kwa sababu mambo mengi ambayo tuliishauri Serikali katika vipindi vya nyuma yanafanyika takwimu zenyewe zinajionesha. Ningependa nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Yesabasi Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Tekonolojia na Elimu ya Juu na Msaidizi wake wa karibu, Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri, pamoja na timu nzima. Sijawasahau Viongozi wa Vyuo Vikuu, baadhi yao wapo hapa, hao ndio majemadari wanafanya kazi nzito na nzuri. Ningependa niwapongeze. *(Makofi)*

Ningependa nitambue kuwepo kwa Mkuu wa Chuo cha Mzumbe, Mheshimiwa Ibrahim Kaduma. Vilevile kuna Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Professa Babu, naye yupo pale amekuja kujumuika nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa uchumi hapa duniani siku hizi umebadilika. Huko tulikotoka utajiri wa nchi ulihesabika kwa wingi wa *physical capital,* yaani nchi gani ina mali nyingi sana. Sasa hivi nguzo kubwa ya uchumi ni utajiri wa elimu hususan elimu ya sayansi na ufundi. Dunia imeshatambua hivyo na umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini unaendana na jinsi Elimu ya Juu ilivyo katika nchi husika. Kwa maana hiyo basi, nchi zetu zinahitaji vijana wengi wapatiwe elimu ya juu. Sasa hivi sifa ya msingi katika kazi zinazohitaji stadi ni shahada na hii ni muhimu sana katika wakati huu wa utandawazi ambapo tunagombania nafasi ambazo ni chache, kupata nafasi hizo usipokuwa na shahada ni ndoto ya mchana. Kwa hiyo, tuna changamoto hapa kwamba, Elimu ya Juu ipatikane katika ubora unaotambulika Kimataifa na vilevile iwafikie vijana wetu wengi. Naishukuru Serikali kwa jitihada zake katika mambo mengi na katika kitabu hiki kuna mifano mingi ya juhudi ambazo zimefanyika na Serikali na hii ni hatua *in the right direction.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 1980, Serikali nyingi hapa duniani na hasa katika nchi zinazoendelea na vilevile wahisani, waliweka msisitizo katika Elimu ya Msingi na Elimu za Sekondari na hata hapa Tanzania ndivyo ilivyokuwa. Tumejionea kwamba, uwekezaji na bajeti kubwa ilielekezwa zaidi katika Elimu ya Msingi. Elimu ya Juu kwa muda mrefu haijapewa kipaumbele hata kidogo. Nashukuru kwamba, ukiangalia bajeti katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imezinduka na tunaona pesa na uwekezaji katika Elimu ya Juu unasogeasogea ili ukidhi mahitaji angalau kwa asilimia ndogo. Yote hayo yanatokana na dhana iliyokuwa inanadi kwamba, ukiwekeza katika Vyuo Vikuu, manufaa ni hafifu katika kuendeleza uchumi ukilinganisha na kuwekeza katika Elimu ya Msingi. Ningependa kutamka hapa kwamba, dhana hii ni potofu na imepitwa na wakati. Matokeo ya dhana hii ni kwamba, bajeti imeendelea kuwa finyu ingawa mahitaji yanaongezeka. Walimu wetu ni wachache na wachache tulionao wengi wanakimbia kwenda kutafuta maslahi mahali pengine kwa sababu mafao yao hapa nchini ni duni. Hali katika kila Chuo ni kwamba, vyumba na vifaa vya kufundishia ni haba, kwa maana hiyo mafunzo yanaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Dunia na *UNESCO,* waliunda Kamati *(Task Force),* ambayo ilichambua nafasi ya Elimu ya Juu katika kuleta maendeleo ya nchi za Kusini. Ni viongozi mahiri waliochaguliwa walikuwa 14 *(14 academicians)* na huo utafiti ulifanyika katika nchi hizi. Majadiliano yalifanyika kwa muda wa miaka miwili na mwaka 2000 walitoa ripoti. Mambo mengi waliyoyapata. Lakini labda niseme tu kwamba, lile ambalo lilinivutia ni kwamba, walisema kwamba, bila kupanua na kuboresha Elimu ya Juu, nchi zinazoendelea hazitaweza kuhimili ushindani katika uchumi wa kisasa unaotegemea elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, juhudi nyingi zimeonekana katika kuboresha na kupanua Elimu ya Msingi na Elimu za Sekondari. Jana tulikuwa na bajeti ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, tuliona hayo na tukampongeza.

Lakini kwa upande wa Elimu ya Juu, naweza kusema, tusipoweka mikakati madhubuti na ya makusudi ya kupanua na kuboresha Elimu ya Juu sasa, Tanzania itabaki kisiwa kitakachoachwa nyuma kimaendeleo katika karne hii ya sayansi, teknolojia na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano tu kwamba, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, kuna vijana wetu 6,320 ambao waliomba kujiunga na Chuo hicho na walikuwa na sifa zinazokidhi lakini nafasi zilizopo ni kama 945 tu ambayo ni asilimia 14. Ningeweza kutoa mifano ya vyuo vingine tarakimu zinaendana hivyo hivyo. Vilevile niliwahi kutoa mfano hapa ambao si vibaya nikaurudia kwamba, kulikuwa na utafiti uliofanywa na *Economic and Social Research Foundation* katika nchi 13 za Afrika katika eneo letu. Walichambua ni wahitimu wangapi wa Vyuo Vikuu kwa kila mwaka kwa kila laki ya Wananchi katika nchi husika. Nitaje tu matokeo ya nchi chache ambazo tunaweza tukajilinganisha. Mozambique walikuwa 10, Uganda 19, Zimbabwe 29, Kenya 41, Namibia 141 na Afrika Kusini 244.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata kigugumizi kutamka kuwa, Tanzania ni wahitimu saba tu. Sasa nadhani hapo sina haja ya kuiomba Serikali kwamba, wenzetu wakitembea sisi hatuna budi kukimbia. Hata hivyo, naipongeza Serikali kwamba, sasa hivi inawekeza katika elimu. Tunaona vyuo vingi Serikali inavipanua, usaili katika vyuo vingi binafsi unapanuliwa, ningeomba tuendelee na hiyo nguvu mpya na ari mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wote nilipokuwepo hapa Bungeni, nimechangia kuhusu Sheria ya Vyuo Vikuu. Wote tunakumbuka kwamba, katika Mkutano wa Tisa, Mheshimiwa Waziri alileta Muswada na namshukuru sana. Lakini nikumbushe tu kuwa huko tulikoanza ilikuwa Muswada huo uunganishe Vyuo Vikuu na Vyuo vya Teknolojia, lakini vyuo vya teknolojia iliondolewa katika Muswada huo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tano, ametuambia kuwa mwaka 1995 tulikuwa na vyuo 23 vya teknolojia na sasa hivi tunavyo 43. Kwa hiyo, ningeomba kwamba, suala hili liangaliwe ili Muswada utayarishwe na kuletwa hapa Bungeni ili utungiwe sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumefanya mambo mengi ambayo sisi wenyewe hatujisifu. Tunasifiwa kwa uchumi, tunasifiwa vilevile kwa mfumo tuliojiwekea wa kuangalia mapesa ya Serikali, yaani *Intergrated Financial Management Systems* na wenzetu majirani wanakuja kujifunza kutoka kwetu. Sasa tunapoichagiza Serikali kuongeza idadi ya vijana wanaoingia Chuo Kikuu, tusi-*compromise quality.* Nilitaka kukumbusha Baraza letu la Ithibati ya Elimu ya Juu kwamba, imepewa majukumu mengi ikiwa ni pamoja na kuweka, kuviangalia, kuvitunza na kuvienzi viwango vya elimu katika programu zote.

Taratibu ziwekwe kuangalia *quality, assurance, auditing* na *coordination* ya *courses* na natarajia kwamba, kozi zinazofanana katika vyuo ziwe na ubora sawa. Sioni sababu kwa nini ubora wa programu utofautiane na wahitimu wetu wawe na ujuzi karibu wa aina moja. Kwa sababu ya utandawazi tuna vijana wetu wengi baada ya kuhitimu wanakwenda nje ya nchi yetu kufanya kazi. Botswana tuna Madaktari wengi, vilevile Lesotho, sasa kama tutakuwa na viwango tofauti vya wahitimu wetu, mtu akienda nchi ya

nje akaboronga watasema wahitimu wa Tanzania sio wazuri.  Ndio maana niliona kwamba, hiyo *quality assurance* ifanyike ili programu ifananefanane na ikiwezekana hata mitaala iwe sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, wiki mbili zilizopita Wizara ilizindua *Tanzania Academy of Sciences,* ambayo ina waasisi 25.  Nilitaka kumwomba Waziri kwamba, vigezo vya kuingia katika taasisi viwekwe wazi.  Nina imani kuwa Wananchi wengi wangependa kujiunga na hii *academy* lakini  ilianza na kuzinduliwa kinyemela, wengine tulikuwa hatuna habari.  Kwa hiyo, tungependa tujue namna ya kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa niwashukuru Wananchi wa Rungwe, kwa heshima waliyonipa ya kuwatumikia kama Mbunge wao.  Tumefanya mengi kwa pamoja, tumeweka misingi mingi kwa hiyo huko tunakokwenda tuangalie kwamba ni lazima tuongeze matofali kwenye hiyo misingi.  Nawatakia uchaguzi mwema, wachague mtu ambaye ataendeleza mafanikio tuliyofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo na namaliza kama nilivyoanza kuiunga hoja mkono.  Ahsante sana.  *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.  Kwanza na mimi napenda nianze mchango wangu kwa kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, ambaye amefariki.  Sisi wengine hatukuwepo, tulipata habari zake tukiwa safarini.  Hatuelewi wenzetu mlishtuka namna gani lakini sisi wenyewe tulipigwa butwaa pale hotelini, siku nzima tulishindwa cha kuongea kwa sababu tulimwacha mzima, lakini kazi ya Mungu haina makosa.  Tunaomba tu Mungu amrehemu na aifariji familia yake.  *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kwanza nimpongeze Mwalimu wangu Mheshimiwa Dr. Pius Ng’wandu kwamba, ameingia pale Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, amefanya mambo makubwa, mageuzi makubwa sana tumeyashuhudia. Kwa kweli anastahili pongezi yeye na Naibu wake Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, pamoja na Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamishna wote na wataalamu, wamefanya kazi kubwa walau tunaanza kuona Vyuo Vikuu badala ya Chuo Kikuu kimoja au viwili tulivyozoea kuvisikia, lakini sasa tumekuwa na Vyuo Vikuu vingi vya Serikali vinakuja pamoja na vya watu binafsi.  Kwa hiyo, tunapenda tumpongeze sana.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Waiziri, ametushirikisha sana sisi wenzake hapa ndani katika mipango yake yote ya Elimu ya Juu.  Amekuwa mvumilivu sana kwetu na nachukua nafasi hii kusema haya kwa sababu yeye alitangaza kwamba, hawezi kugombea.  Mimi ni mwanafunzi wake, kwa hiyo, nimefaidika sana na mchango wake katika maisha yangu binafsi.  Basi tumtakie kheri kama ataishi maisha ya kawaida mapya, lakini awe tayari kutoa mchango wowote ambao Serikali au nchi itamhitaji kuutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nililalamika sana juu ya chuo chetu cha Mbeya, hakikuweza kufanikiwa kuitwa Chuo Kikuu kwa maana ya Chuo Kikuu wakati

yeye mwenyewe Waziri, mwalimu wangum akiwa ni Waziri wa Wizara hiyo. Lakini alinijibu vizuri na ameacha amesha-*set standard*,kwa hiyo, najua Waziri atakayekuja atahakikisha Chuo Kikuu cha Mbeya kinafunguliwa kama Chuo Kikuu sio Taasisi. Nina hakika na yeye atatusaidia kusukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili; moja amelizungumza kaka yangu, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa sasa hivi ni kwamba, tunahitaji Vyuo Vikuu vingi visambae katika nchi, kwa mtandao mzuri, kwa kuangalia maeneo mbalimbali bila kupendelea upande mmoja. Tunaomba hili lizingatiwe na Serikali. Tuna imani na Serikali inayokuja itazingatia hayo kwa ari moja na nguvu moja na kasi moja mpya. Lakini pamoja na kusambaza hivyo Vyuo Vikuu ombi ni kwamba, lazima ubora *(quality)* ya elimu, maana yake sasa hivi kuna *academies* nyingi sana.

Katika nchi unakuta watu wameandika katika jengo la kawaida hapa *academy* fulani, hapa ni *academy* fulani. Nashangaa hii elimu inatoka wapi! Nafikiri lazima kuwe na ufuatiliaji sana pale Wizarani kutoa *qualification* gani kitu kiitwe *academy* au Chuo Kikuu ili kusudi elimu itakayotolewa pale iweze kuwa ni elimu ambayo inauzika mahali popote duniani. Hilo ndilo ombi langu, sio wingi tu lakini *quantity* pamoja na *quality* vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo ambalo mimi naliona kwamba, Serikali imejitolea sana kusomesha vijana tena nafikiri ni bure kwa sababu wote wanakopa kwenye Serikali na huo mpango ulianza zamani lakini umeboreshwa sana na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu. Hatuna matatizo tena vijana wanasoma, wanaotoka familia maskini na kwingine wote wanasoma, watoto wa matajiri wanasoma kwa mikopo mikubwa ya Serikali. Sasa huwa najiuliza, hawa hawapati ajira sasa watalipaje au tugeuze tuseme ionekane wazi kwamba, Tanzania ni nchi mojawapo katika ulimwengu ambayo inatoa Elimu ya Juu bure. Hiyo ingetuletea sifa kubwa zaidi, kwa sababu tunasema tunawakopesha lakini hawana ajira.

Ukiwauliza wenyewe wahitimu wako wapi huoni wako wapi, hawa *graduates* wanaomaliza wako wapi? Tunajua wanakwenda wapi? Hatuwezi kutumia fedha nyingi za Serikali namna hii halafu hatuwezi kuwapa kazi, hatuwezi kuajiri halafu tunajua hawawezi kurudisha zile fedha. Sasa ikijulikana kwamba tunasomesha bure, hiyo itasaidia pengine. Tutaeleweka kwamba ni nchi ambayo inatoa elimu hiyo bure. Kwa sababu hatujui wako wapi kwa hiyo ni kama mnyama mmoja anaitwa nini sijui, wengine wanafahamu lakini wanachimba shimo refu sana. Halafu anachimba tu *the whole day* sijui anakuwa anakula minyoo na nini halafu anaondoka. Sasa ngiri ndio nyumba yake, lakini mnyama yule sijui ndio muhanga, anachimba shimo refu lakini ngiri ndiyo anayekaa ndani.

Sasa tunaweza tukasomesha watoto kwa gharama kubwa ya fedha ya Tanzania, lakini elimu ile wanafaidi nchi nyingine. Hilo naona ni hatari kabisa. Hatuwezi kutumia fedha na watoto hatuwezi kuwaajiri na nafasi zingine zipo ila kuna ukiritimba kidogo.

Mimi nafurahia Wizara ya Elimu na Utamaduni, walishasema Mwalimu *Grade C* hawezi kuwa Mwalimu Mkuu, kwa hiyo, wamewaondoa wamebakiza wa *Diploma* na *Grade A* wazuri wazuri ndio wameshika nafasi zile. Hivi leo bado unakuta kuna watu wenye digrii wengi sana lakini *DEOs* ni wale wa zamani wengine ni wale wenye *diploma* tu au hawana kitu chochote. Mimi nafikiri ziko nafasi nyingine ambazo vijana wanaohitimu Chuo Kikuu wapewe jamani.

Hatuwezi kuwa na ving'ang'anizi tu, watu wameng'ang'ana nafasi nzito miaka nenda rudi na wala hawa-*qualify* lakini wako pale, kwa nini hatuwezi kuwapa vijana wetu wakamate nafasi zile sasa mwisho wanakosa ajira na kwa hiyo hawawezi kurudisha fedha, kwa hiyo, tunatumia fedha za Serikali kuwaelimisha bure. Mimi nafikiri Serikali hili jambo ilione.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho sielewi Vyuo Vikuu wanapangaje mafao yao, sijui mishahara, *allowances* mbalimbali, lakini sisi tunaokaa na watu ambao wanafanya kazi huko tunakerwa sana. Kwa sababu imeonekana pale wale watawala sijui wataalamu ambao wengine ni *Form Four* tu wanapanga mishahara yao mikubwa sana lakini mwalimu anayehangaika ana *Masters, PhD* anapata mshahara mdogo kuliko mtu wa kawaida tu ambaye anafanya kazi ofisini. Unashangaa sana nani anayepanga vitu hivyo.

Mtu amesota amesoma *first degree, diploma, second degree, PhD* anapata fedha kidogo, mtu tu wa kawaida pale anafanya kazi ofisini mshahara mara mbili ya mtu aliye na *masters* na aliye na *PhD*. Nadhani *Open University* wana tatizo, halafu wanajipangia tu. Wanapolalamika huyu anaweza kupata *house allowance* huyu hana, wamejirundikia wao wenyewe sijui Serikali ziko ngapi katika nchi hii.

Nafikiri kama *University of Dar es Salaam* wanapata kiasi fulani, basi Sokoine, Mzumbe, nadhani kuna utaratibu ambao aliyesoma sana apewe sana, hakusoma basi bahati mbaya atapata kulingana na kusoma kwake. Ni aibu kumpa mtumishi wa kawaida shilingi laki tisa halafu mtu ana *PhD* zake anapata shilingi laki tano, maana yake nini. Nchi gani hii? Nadhani *there is a problem there?*

Matokeo yake Vyuo Vikuu haviwapi mafao mazuri, haviwajali, vinajali watumishi tu wa kawaida posho kubwa, mishahara mikubwa wengi wanatoroka. Profesa amesema pale wengi wamekwenda Gaborone.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi, juzi nilikuwa nikikutambulisha kwa Profesa Matibo pale Johannesburg, yule ni mwalimu wa *linguistics* na katika nchi hii watu wa aina yake hawawezi kuzidi wawili. Ile ni digrii ngumu sana kuisoma na anajua *French* na Kiingereza vizuri. Lakini katika maongezi yetu walikuwa tena vilevile na Profesa Kezilahabi. Kezilahabi wote mnamfahamu kwa vitabu alivyoandika vya mambo ya fasihi. Wote wamekimbia nchini wako Gaborone kule.

Tumepanda ndege moja nikamwuliza mwalimu vipi huji kusaidia nchi, akasema nasikitika sana vilugha vyote vya nchi ile nimeandikia vitabu. Inanisikitisha

nimeshindwa kukaa Tanzania niandike vitabu kwa lugha zote za nchi yangu akasema eti naumia kama mzalendo lakini katika *green pasture* siumii.

Katika mafao siumii lakini kama mzalendo katika nchi yangu, sijafanya kazi ninayofanya Botswana, naumia. Aliniambia bahati nzuri Naibu Spika, tulikuwa wote pale, nikimtambulisha. Ndiyo aliyenifundisha mimi yule mwalimu.

Kisa hakuna mswahili wa kawaida yuko pale ofisini marupurupu mengi, yule Profesa kidogo, sasa mnataka tufukuze Maprofesa wote. Sisi tunayo habari tunaangalia mshahara. Watu wamekuwa watawala wale wa kawaida wana nguvu kuliko *lectures?*

Wanapendelewa kuliko *lecturers,* hii inakera sana. Mtu ukasote namna hiyo, mwingine alikimbia umande, wewe unasota unasoma unaandika *thesis,* Mswahili amekaa katika deski anapangia wataalamu wasomi mshahara.

Kuna tatizo pale *Open University* hata *University of Dar es Salaam.* Msipofanya hivyo, tutajua la kufanya sisi. Maana tuna madaraka na mamlaka tumepewa na Wananchi wetu, lazima watu wasomi wawe *retained, to be comfortable in order to be retained* ili wafanye kazi kwa nchi yetu, hakuna kupendeleana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nisema hayo, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nichukue nafasi hii, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hotuba hii ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Kabla sijafanya hivyo, nitoe pole kwa familia ya mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, ambaye ametutoka hivi karibuni, pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, ambao wamempoteza Mbunge wao wa Viti Maalum. Naomba Mwenyezi Mungu, aiweke pema roho yake. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Naibu wake, Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu, wataalamu wote, pamoja na Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii nasema ni mpya, kwa maana ni Wizara ambayo imeundwa miaka ya 1990. Lakini kwa muda huu mfupi, Wizara imeonesha kasi kubwa ya mabadiliko hasa katika nyanja za Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, imefanya vizuri kwa muda mfupi na napenda niendelee kuwapongeza kwa kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo mazuri ya Waziri na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, juu ya ufafanuzi wa masuala mbalimbali, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo machache sana, kwa maana ya ufafanuzi na kutoa hoja hapa na pale ili wenzetu waweze kupokea ushauri mbalimbali.

Kwanza nianze na maandalizi ya Vyuo vya Elimu ya Juu, kupokea mabadiliko yaliyotokea kwenye mpango wa MMEM na mpango wa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka hii minne, tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya ongezeko la Shule za Sekondari, ongezeko la Shule za Msingi, ongezeko la wanafunzi wanaoingia na kumaliza Shule za Msingi pamoja na Sekondari. Vilevile, tumeshuhudia matokeo mazuri ya mitihani katika Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Sasa matokeo haya mazuri yanahitaji maandalizi makubwa kwa Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu ili viweze kupokea matokeo haya mazuri ambayo yanapatikana kutokana na mpango huu mzuri.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kujua tu kwamba Serikali imejiandaa kwa kiwango gani kupokea mabadiliko haya ya ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofanya vizuri katika Darasa la Saba, Darasa la Kumi na Mbili na Darasa la Kumi na Nne? Maana wao kwa kufaulu zaidi lazima wawe na sehemu ya kwenda. Nitatoa mfano ambao umetolewa jana na Waziri wa Elimu na Utamaduni. Ukitazama mabadiliko haya ya ongezeko la wanafunzi mwaka 2000 waliotahiniwa Kidato cha Nne walikuwa 47,397. Lakini waliotahiniwa mwaka 2004 ni 63,370 ambalo ni ongezeko la wanafunzi zaidi ya 16,000. Sasa ongezeko hilo linahitaji maandalizi ya kuwapokea vijana hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yako mabadiliko yanayoonekana pia dhahiri katika kufaulu mtihani. Kidato cha Nne hicho hicho wanafunzi ambao wamefaulu kwa kiwango cha Daraja la Kwanza mpaka la tatu mwaka 2000 ni 12,237. Waliofaulu kiwango cha Daraja la Kwanza mpaka la Tatu mwaka 2004 ni 23,929, mara mbili zaidi katika miaka minne. Hii inadhihirisha kwamba tunahitaji maandalizi makubwa ya kuwapokea kwenye *High Schools* na Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, bado nataka kujua wenzetu Serikali wamejianda vipi kupokea mwitiko huu mkubwa ambao umetokea kwa vijana wetu pamoja na wananchi.

Pili, haya ni maandalizi *physical,* lakini yako maandalizi mengine kupokea wanafunzi wa mitaala mipya ya Sekondari. Tumeelezwa hapa katika kijitabu cha Wizara ya Elimu na Utamaduni tulichopewa jana, kinachozungumzia marekebisho ya mtaala wa Sekondari Toleo la Juni, 2005, ukurasa wa sita na ukurasa wa saba. Hapa yamezungumzwa mengi, lakini *interest* yangu hapa ni kuzungumzia juu ya mchakato ambao umetumika kurekebisha mtaala wa Sekondari.

Mchakato ule nadhani ni mfano wa kuigwa, kwamba umekuwa ni mchakato shirikishi ambao umeshirikisha wadau wengi wa maeneo yote kuja na mtaala ambao unaoneka sasa ndiyo mtaala utakaofaa Shule zetu za Sekondari katika karne ya 21. Nawapongeza sana. Lakini la pili, katika maelezo yao wanasema ulikuwepo udhaifu ama upo udhaifu katika mtaala wa sasa na hii ndiyo *interest* ambayo nataka kueleza kwamba

moja ya tatizo ama udhaifu ulioonekana ni kwamba yalikuwepo ama yapo masomo 13 ya lazima ambayo yanaonekana ni mengi sana. Hivyo, yametokea marekebisho.

Lakini lingine katika mtaala wa sasa, unatilia msisitizo ambao umelenga kwenye maarifa, kutoa maarifa tu bila kujali stadi muhimu za kufikiri, stadi za maisha, stadi za ujuzi, stadi za vitendo na ubunifu kwa wanafunzi wenyewe. Kwa hiyo, mtaala huu uliorekebishwa maana yake unataka kuondoa tatizo hili la kujali maarifa peke yake ili mtaala ambao umebuniwa sasa uweze kuwapa stadi za maisha watoto wetu wanapomaliza Shule, uweze kuwapa njia muhimu za kufikiri, uweze kuwapa ujuzi na uweze kuwaandaa kwa vitendo pindi wanapomaliza.

Kwa hiyo, najiuliza sasa hapa, Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu, vimejiaandajae kupokea mtaala huu mpya? Vyenyewe vinafanya marekebisho gani ili viweze kupokea kwa usahihi kabisa mabadiliko haya mapya? Je, Walimu wetu katika Vyuo vya Elimu ya Juu, wanaandaliwa vipi katika kupokea mabadiliko haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nieleze matatizo ambayo yanatokea Chuo Kikuu pamoja na Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu. Katika maelezo ya Kamati tulielezwa kwamba ipo migomo. Imetokea migomo karibu saba kule Dar es Salaam *Institute of Technology* na migomo hii imeundiwa Kamati ili iweze kuangalia tatizo ni nini.

Naipongeza sana Kamati kwa ushauri na Wizara kwa kuunda hiyo Kamati. Kwa hiyo, ninaomba sasa Serikali ifanye bidii na haraka ili Kamati hii ikamilishe mapendekezo yake tuondoe migomo hii.

Lakini nasikitika kwamba tunangojea migomo kila wakati. Serikali isingoje migomo. Katika Vyuo vya Elimu ya Juu, ziko Idara za Utafiti na Idara za Mipango. Idara hizi ni muhimu sana sio kwa kupanga tu mambo yatakayofanyika, lakini pia kwa kutazama wanafunzi wanasema nini sasa, wafanyakazi wanasema nini, kuna tatizo gani ambalo linafukuta kwamba kama halikufanyiwa kazi mapema litaleta matatizo? Kwa hiyo, naiomba kabisa Serikali, Idara zile pamoja na Idara nyingine ambazo ni muhimu zifanye kazi ya ziada kuangalia nini kinatokea ili kisiweze kufikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya matatizo ambayo nayaona yanayoleta migomo na matatizo mengine ni matatizo ambayo yako toka mwanzo hasa kwenye hivi Vyuo vya Elimu ya Juu. Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu vinao Walimu, lakini jambo la kwanza Walimu walioko kwenye Vyuo Vikuu mara nyingi ni Walimu ambao hawana *teaching methodology.* Ni walimu wanaofundisha kwa uzoefu, wemefaulu, wamepata shahada nzuri, wakabaki ma- *tutorial* wakaendelea kufundisha. Kwa hiyo, ile saikolojia ya watu wazima ya kuwafundisha na kuwaelewa, kwa kweli inahitajika sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba pengine tungeangalia upya jinsi ya kuwasaidia Walimu wetu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, waweze kupata dozi kidogo ya mafunzo ya saikolojia na *teaching methodology* ili waweze kuwajua tu wanafunzi wao.

Pili, mafunzo ya utawala kwa Viongozi yanahitajika sana kwa sababu huwezi ku-*manage institution* kama huna mafunzo rasmi ya Utawala na Uongozi. Kwa hiyo, ni vizuri Viongozi wakapata mafunzo ya aina hiyo katika Vyuo vyetu.

Tatu, ni mafunzo ya uzoefu wa vitendo katika fani zao. Walimu wetu mara nyingi wanafundisha kwa mazoea, lakini tunasema tunaingia karne ya 21 ya sayansi na tekinolojia, karne ambayo ni ya ushindani wa soko ambayo lazima watu washindane kwa kufanya kazi nzuri za vitendo. Kwa hiyo, ili iwezekane, Walimu wetu ni lazima wafanye kazi za nadharia pamoja na vitendo hasa halisi kwenye maeneo ya *professional* zao.

La mwisho, nawaomba Vyuo vya Elimu ya Juu wawe na mabadiliko ya mtazamo. Katika hili mimi najikumbusha, nilipokuwa Chuo Kikuu, mara yangu ya kwanza nimeingia Chuo Kikuu jambo moja nililojifunza ni kwamba Maprofesa hawakuwa na nia kubwa ya kutaka wanafunzi wafaulu, walikuwa na nia kubwa ya kutaka wengi wafeli ndivyo nilivyojifunza *(Makofi)*

Wako walimu ambao sitawataja majina, Maprofesa wangu wanne ninaowakumbuka. Mmoja siku ya kwanza alisema kwa Kingereza*, My name is Professor Enye, I am going to teach you in plant physiology and for those who survive this year I will continue with you next year. Signal* ile inaonyesha kabisa kwamba hawahimizi wanafunzi kufaulu. Kwa hiyo, nawaomba tubadili mtazamo, Vyuo Vikuu viwe ni sehemu ambayo mwanafunzi akiingia afikirie kufanya vizuri, tumu-*encourage* afanye vizuri ili aweze kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nimalizie kwa kusema kwamba mfumo huu wa ongezeko la kufaulu watoto na *infrastructure* za elimu, basi uendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika mfumo wa soko huru kwa maana ya kupokewa na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja muhimu sana ya Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu na nianze kwa kumpongeza sana kwa hotuba yake nzuri na kwa kutueleza mipango mingi mizuri ambayo yeye na wataalamu wake na Serikali kwa ujumla wamefanya kwa kipindi cha miaka karibu kumi. Ninawapongeza sana kwa kazi nzuri hizo na kwa ujumla kwa Sekta ya Elimu. Tunawapongeza sana wenzetu waliofanya kazi na hasa katika Serikali hii ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ambayo Mwenyekiti ametueleza mambo mengi mazuri jinsi alivyoweza kushauri Wizara namna ya kufanya mambo mbalimbali na mapendekezo ambayo ameyaweka mbele yetu. Kwa ujumla narudia kusema, naipongeza sana Serikali kwa kushughulika na Sekta ya Elimu kwa jinsi walivyoshughulika nayo.

Mheshiumiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba sababu mojawapo iliyonifanya nigombee Urais, nilikuwa natafuta uteuzi wa Chama changu cha Mapinduzi ili kutaka kubadili mtiririko huu na kuimarisha Sekta ya Elimu, lakini vile vile kubadili mfumo wa Bunge*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nimependa kwamba Sekta kama hii ya Elimu ilikuwa inafaa tuijadili kwa siku hazipungui nne au tano ili tuelewane hasa hatima ya elimu ya watoto wetu itakuwaje. Alivyochangia sasa hivi Mheshimiwa Lupatu amenigusa sana kwamba hivi vijana wetu wanapokuwa Shuleni, Walimu tunataka washinde au washindwe. Sasa sababu hizo mimi naona sitoshelezwi kabisa na kuwa unajadili dakika 15 au 20, Bunge unamaliza mwaka mzima unakuwa bado hujafika mahali pa kutafuta wenzako wakuelewe na nyie wote kwa ujumla kama Watanzania na baadaye Waafrika meelewane, mnataka hasa kupata kitu gani katika kipindi fulani tuseme hiki cha karne ya 21 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipata bahati wa kuwa Waziri wa kwanza wa Wizara hii ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu na wakati huo tulipoianzisha Wizara hii, Katibu Mkuu wangu akiwa Dr. Mohamed Bilal tulipambana na mambo magumu, lakini tuliweza kuweka misingi mizuri ambayo ndugu zetu wamekuja kuiendeleza. Napenda nishukuru sana kwa kuindeleza misingi hiyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Wizara hii ni kwamba eneo hilo la sayansi na teknolojia lilikuwa lipanuliwe na liimarishwe liende mpaka Vijijini. Wizara hii kwa kweli ni Wizara ambayo ina maana ya kujumuisha shughuli karibu za Wizara zote, kwa sababu kama unatafuta kuimarisha dhana ya sayansi na teknolojia, unagusa kila Sekta, unagusa kila eneo na unapenda maeneo haya yaimarishwe kuanzia Vijijini. Mathalan, tuna maeneo mengi sana ya viwanda vidogo vidogo yanaguswa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo mengi ya miundombinu yanaguswa na Wizara hii. Tuna maeneo mengi katika maeneo ya kilimo yanaguswa na Wizara hii, huduma za jamii, maji, hata elimu yenyewe. Ukiangalia vielelezo vinavyotumika katika kufundisha watoto wetu katika Shule za Msingi katika maeneo ya sayansi, baolojia, fizikia, utakuta hakuna kabisa sehemu ambazo unaweza ukafundishia fizikia katika maeneo ya Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa teknolojia hii na sayansi hii tunaiimarisha namna gani kuanzia maeneo hayo ya Vijijini kuanzia na Elimu yetu ya Msingi? Bado tuna swali kubwa na tunadhani hata wakati ule mwaka 1990 na kuendelea tulidhani tungeweza kuwa na Kamati za Wilaya za Sayansi na Teknolojia na mimi pendekezo hilo nililifikisha mpaka kwa Wakuu wa Wilaya zote na Wakuu wa Mikoa walifahamu. Sijui kwanini eneo hilo lilififishwa na mpaka sasa Wizara hii inaonekana kama Wizara ya watu waliosoma sana huko juu, lakini Vijijini hawaguswi na dhana nzima hii ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda nijenge hoja kwamba Wizara hii inatakiwa ianze kujipanua iguse kabisa maeneo ambayo wananchi, katika maisha yao ya kawaida ya Vijijini wanatakiwa wajue kwamba kuna matumizi ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilikuwa napenda nilizungumzie, ni katika suala zima la Elimu ya Juu na Elimu kwa ujumla. Tunakubali kabisa kwamba tunaendelea kupanua na kuongeza nafasi za Shule za Msingi na Sekondari. Ambacho inafaa tukubaliane vile vile ni viwango. *Quality* ni ubora wa elimu hii; je, huyu

Mtanzania anapomaliza Sekondari anaweza kujieleza vizuri hata kwa kuandika barua ya Kiswahili au ana matatizo? Je, mtanzania huyu anapomaliza Elimu ya Sekondari anaweza akaandkia barua nzuri kwa lugha ya Kiingereza au ana matatizo? Kwa sababu kama atakuwa ana matatizo, kuandika barua maana yake hata kutafuta kazi itakuwa shida. Atashindana namna gani na Mganda na Mkenya ambao wamekuja Tanzania kutafuta kazi ili waweze kushindana na huyu? Atawezaje?

Kumbe ni vyema hilo tukajiuliza na tukaelewana kwamba kuna tatizo la ubora na viwango vya elimu yetu na tufanye nini sasa ili kusudi vijana wetu hawa tuweze kuwapa zana za kutosha katika ubora wa elimu hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile najiuliza, tumekuwa tukiendelea kufundisha na kuwasaidia vijana wetu katika kupata elimu yao. Lakini je, hili eneo la uchapa kazi, elimu, ikiwa pamoja na kujitegemea tumeliacha au bado tunalo? Hivi Mtanzania anayemaliza katika kiwango cha Sekondari au kiwango cha Vyuo na hata Vyuo Vikuu anakuwa na zana za kuweza kujitegemea, kwa Kiingereza tunaita *work ethic*, anakuwa na utashi wa kutafuta kujitegemea au anatafuta kutegemea?

*Work ethics,* Mataifa mengine kama Ujerumani yametumia sana kwamba mtoto anakuwa hapiti tu Shule, lakini anafundishwa umuhimu wa kujitegemea, *the work ethics* yaani akiingia kazini kama mfanyakazi wako wa Tanzania anakuwa mwenye bidii, anakuwa mwenye unadhifu anakuwa ni mwenye dhima kubwa ya kuweza kutekeleza kazi yake. W*ork ethic* hii tunaitoa katika Tanzania au tumewaachia tu vijana waweze kusoma na kumaliza madarasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naliuliza vilevile lina ambatana na kwamba je, tunaelimisha watoto wetu, hivi wanapomaliza masomo wanakuwa hawashawishiki na rushwa au wanashawishika na rushwa zaidi? Kuna nini kinachotokea mtu amemaliza masomo halafu anakuwa anatamani kiasi kwamba atumie hata rushwa kuweza kupata mali au mapato mengine? Suala la elimu na rushwa hivi tunalitoaje? Tunalijengaje katika msingi wetu wa elimu? Kwa nini rushwa inaonekana inaongezeka wakati vijana tunaowatoa katika Vyuo vyetu ndiyo tunawatoa sisi ambao tunawatayarisha katika Taasisi za Elimu? Hilo suala linatakiwa liwepo au somo hilo liwepo, suala la elimu na uaminifu ili liende sambamba katika kudhibiti rushwa na mwananchi aweze kujisikia vizuri katika kutumikia Taifa lake na katika kujenga Utanzania na Uafrika wa maana zaidi katika siku zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linaambatana na lile alilosema mwenzangu, elimu na malezi. Tunapokuwa tunafundisha na mimi ni Mwalimu, nina *Diploma* ya Ualimu ya Chang'ombe na katika Ualimu, unafundishwa kumlea mwanafunzi au mwenzako aweze kwanza kupata uwezo katika somo au masomo fulani. Lakini vile vile aweze kupata uwezo wa kutafuta kusaidia hata watu wengine.

Sasa kama wewe Mwalimu unaonekana humsaidii mwanafunzi, yeye moja kwa moja naye atatoka akiwa anajua kumbe kumsaidia mtu mwingine haina maana. Wasomi wengine wanaita *deontologists* ni Kiingereza kinachoonyesha kwamba wewe unatakiwa

kuwa na moyo wa kusaidia wengine sio kutafuta faida. Ukitafuta faida, basi itafikia mahali utamnyang'anya mtu hata nguo zake kwa sababu una nafasi hiyo, kumbe elimu inatakiwa iende sambamba katika malezi yetu na kuhakikisha kwamba unamjali mtu mwingine na hasa huyu mtu mwingine ni Mtanzania mwenzako, ni Mwafrika mwenzako au ni mtu mwingne ambaye anatakiwa kupata haki za msingi za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunapokuwa na migogoro tuisimamie vizuri kuanzia Walimu na Viongozi tunapokuwa na matatizo, tuwasikilize ambao wanaweza kuwa wamesababisha matatizo, tuyasimamie vizuri na huyu mtoto katika kumfundisha tumfundishe kwa kumwelekeza. Walimu wote kabisa nchini na wengi wanafanya, tunaomba wawasimamie wanafunzi vizuri ili elimu yao iambatane na kujua kwamba kumbe kupata elimu si kuelekea kumwonea mtu mwingine. Hilo ni suala muhimu sana kwa sababu tunasikia mambo mbalimbali katika Vyuo Vikuu, baadhi ya wanafunzi wanaonewa sana hawawezi kushinda mpaka akurupushwe kwa namna fulani kisaikolojia ambayo inakuwa ni balaa kwake katika kusoma. *(Makofi)*

Watoto wa kike wananyanyaswa sana katika Sekta za Elimu ya Juu, wanatafuta wengine wafanye mambo si ya kawaida ili waweze kufaulu mitihani. *(Makofi)*

Walimu Watanzania tukiwa namna hii hatuwezi kujenga Taifa imara na Afrika imara na mtoto wa Afrika kuanzia ambapo mababu zetu waliachwa kwenye utumwa huko, sasa anatakiwa atendewe vizuri, awe na akili nzuri, awe na moyo mzuri wa kuhakikisha kwamba baadaye anaimarisha eneo letu hili la uafrika na anajenga msimamo anajenga uwezo ambao Waafrika tunaweza tukajivunia katika siku zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nayasema haya baada ya kuona kwa mfano yameelezwa na wenzangu wasomi wengi tu wanakimbia nchini kwa sababu ya mambo ya kunyanyasana tu. Madaktari wetu walipogoma pale kumbe waligoma kwa msingi kabisa, lakini wakaachwa achwa tu siku kadhaa, tulidhani walikuwa na makosa kumbe walikuwa sahihi. Wale Madaktari kwa sababu posho ilipunguzwa ghafla sasa hata mimi ukinipunguzia posho ghafla leo tutafuatana mpaka Ofisini. *(Makofi)*

Mambo ya kupunguziana mapato, hizo ni haki za msingi na wale tulidhani ilikuwa vizuri sana tukawajali. Lilifanyika baadaye na Serikali, lilikuwa zuri, tumeshalisikia tunapongeza. Lakini vitu vya namna hii havitakiwi kutokea, vinatakiwa kuanzia mwanzo mnaelewa tatizo ndiyo maana ya usomi, uelewe tatizo ili uliendee vizuri ushirikiane na wenzio na uweze kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge la Afrika ya Elimu, Utamaduni, Utalii pamoja na Rasilimali Watu na hivi kwanza ndiyo tumeanza katika Bunge la Afrika kuangalia eneo zima hili la Elimu ya Afrika katika mfumo wake na mwelekeo wake, tunaelekea vipi ili tuweze kuimarika katika umoja wetu na ushirikiano wetu. Tunaangalia kwa Kiingereza tunasema: "*Education for African integration.*" Sasa hivi Marais wetu wememaliza kuweka msimamo jinsi ambavyo wanataka Viti viwili vya Baraza la Usalama. Sasa kuelewana huko kumetupa faraja kwamba angalau katika Afrika tunajenga uwezo wa kuelewana na kushirikiana.

Mimi naomba sana, tutumie yale yale ambayo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa aliyoeleza kwamba, Afrika kuijenga ikawa imara lazima tushirikiane na sisi tutasaidiana na wenzetu hata kama sio mimi wale watakaokuwepo ili eneo hili la elimu kwa ajili ya ushirikiano na umoja wa Afrika iweze kuimarika katika siku zinazokuja. Bila ya kuwa pamoja na bila ya kuwa imara, Waafrika tutaendelea kusambaratishwa na Waafrika, tutaendelea kudharauliwa.

Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu pamoja na Naibu Waziri Zabein Mhita na Katibu Mkuu Lucy Mollel na ndugu zangu wengine kwa jinsi ambavyo wemafanya kazi vizuri. Tunawapongeza, hongereni sana kwa kazi nzuri ambapo tunawatakiwa kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa hotuba yake nzuri na nimpongeze Naibu wake kwa kazi nzuri na Watendaji wote wa Wizara hii. Pia, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kazi nzuri na hususan katika kuangalia matatizo ya wanajumuiya za Vyuo Vikuu, wametoa mapendekezo na mapendekezo hayo ninaamini kabisa yatatiliwa mkazo na viongozi wote wanaohusika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonisukuma sana nizungumze, ni kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Bunge lako Tukufu kuniteua mimi kwa miaka mitano iliyopita pamoja na wenzangu wawili kuwa mwakilishi wenu katika Baraza la Chuo Kikuu Huria. Nafasi hii tuliomba watu wengi, lakini sisi watatu mlituchagua, Mheshimiwa Benson Mpesya, mimi pamoja na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh tuwawakilishe katika uongozi wa Baraza la Chuo Kikuu Huria.

Leo nitajielekeza zaidi katika kuzungumzia Chuo hiki kwa sababu nimekaa nacho miaka mitano, naelewa matatizo yake na uwakilishi wangu kwa kweli utakuwa hauna faida kama sitakizungumzia kwa undani.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, Chuo Kikuu Huria ndiyo kokoro lililo na chujo katika kuelemisha Taifa hili hasa katika Elimu ya Juu. Ninasema hivi, hili ndiyo kokoro lililo na chujo kwa sababu kokoro mara nyingi linasomba vitu visivyotakiwa kusombwa. Lakini Chuo hiki kina mchujo mzuri na ukiangalia udahili ambao unategemewa kwa mwaka huu, wanafunzi 21,000. Hiyo ni idadi ya zaidi ya Vyuo vingine vyote ambavyo ni *convectional,* utaona kabisa kwamba kwa idadi hiyo kama tukifaulu kuwadahili wanafunzi hao ina maana nchi hii itakuwa imekwenda mbali na kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo kielimu ya juu.

Sasa kwa bahati mbaya, niliyojifunza kwa kipindi cha miaka hiyo mitano, la kwanza, Chuo hiki hakijapata kwa kweli msukumo unaotakiwa kama Chuo Kikuu Huria. Kutokana na udahili wa wanafunzi wengi, Chuo hiki kwa mfano kwa sasa kinapewa

fedha za matumizi ya wanafunzi kupitia *other charges*. Ambapo ukiangalia wanafunzi 21,000 kama wakidahiliwa wote, kwa kuwapa matumizi yao kwa *other charges* ina maana wanapunjwa sana. Lakini wangepewa kwa *direct student cost*, wangepata fedha nyingi mara mbili zaidi ya Vyuo vingi. *(Makofi)*

Sasa tunawabebesha mzigo mkubwa sana Viongozi wa Chuo hiki. Kwa kusema hili, ningependa nitoe shukrani zangu za dhati kabisa, kwanza kwa Mkuu wa Chuo ambaye ni Dr. Samwel Malecela, kwa Uongozi wake ambao haukuyumba na Uongozi ambao ni imara. Lakini nitambue pia uongozi mzuri sana, uongozi wa mtu ambaye ni jasiri, mtu ambaye kwa kweli ameridhika na chochote unachompa na unachomwambia, Prof. Geoffrey Mmari. Tumekaa naye kwa miaka mitano, ni mwadilifu, ni mtu mwenye kuelewa wajibu wake, ambaye amejitoa mhanga katika kuvitumikia Vyuo vyetu Vikuu vingi hapa nchini.

Lakini nitambue pia uongozi wa sasa wa Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Tolly Mbwette. Ni kijana, kwa muda mfupi ambao tumekaa naye pale, mimi ni Kikao changu kimoja tu nimehudhuria akiwa Makamu Mkuu wa Chuo. Ni kweli tafsiri ya nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya pale sasa inatafsiriwa. Ameanza kuonyesha mabadiliko makubwa sana katika kipindi kifupi na kwa ujana wake ninaamini ana safari nzuri, ndefu ya kujiendeleza kuvisaidia Vyuo vyetu. Tunamtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie matatizo makubwa ambayo kwa kweli kama tukiyatatua, Chuo hiki kitakuwa Chuo kilichotarajiwa na kitatekeleza matarajio yake. Tatizo kubwa kama nilivyosema, Chuo hiki hakipati fedha za kutosha kutoka fungu la Serikali. Lakini kubwa zaidi ni kwamba Chuo hiki kimesahaulika katika majengo. Hiki Chuo ni Chuo ambacho sasa hivi kinaendeshwa katika majengo yaliyoko Kinondoni ambayo kwa kweli tunaishukuru Serikali, maana majengo hayo yamenunuliwa kutoka Benki ya Biashara ya Taifa. Lakini bado majengo yale hayatoshi, ukarabati mkubwa unatakiwa na majengo mengi yanapaswa kuongezeka.

Lakini kubwa zaidi ambalo mimi ningeomba ili Chuo hiki kitekeleze matakwa yake na kwa kweli dhamira ya kuundwa kwake kwa sababu Chuo hiki siyo kwa ajili ya Dar es salaam peke yake, siyo *convectional*, majengo yake yametawanyika nchi nzima. Napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Mikoa hasa mitatu ambayo kwa kweli yenyewe imekwishatoa uamuzi wa kukipa Chuo hiki majengo. Mikoa hiyo ni wenzetu wa Mbeya, wenzetu wa Ruvuma na Singida. Hatua za juu sana zimeanza kuchukuliwa na Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Viongozi wa Mikoa hii ndiyo wametambua umuhimu na kwa kweli umuhimu wa kuwaelimisha watu wao. Ninaomba kupitia Wizara yako ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, litolewe agizo. Serikali iwaagize Wakuu wa Mikoa kuangalia majengo yale ambayo yanaweza kutolewa kwa ajili ya matumizi ya Elimu Huria katika Mikoa yote na ikiwezekana mpaka ngazi ya Wilaya.

Mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa kwa Sera ya sasa, kwa kugawa maeneo ambayo hayatumiki vizuri ili yaanzishwe Vyuo Vikuu. Amegawa Chuo cha *TANESCO* Morogoro kwa Jumuiya ya Waislam; amegawa majengo ya Chuo cha Benki Iringa kwa Tumaini *University*. Nimwombe sasa Mheshimiwa Rais kabla hajastaafu, katika kuwasaidia wanyonge ambao wamesambaa nchi nzima, atoe tamko

kabisa kwamba kwa kweli kila Mkoa utenge majengo na kama yako majengo ambayo yalikuwa yanatumiwa na vyombo vyetu vya Umma na yako katika Mikoa yote, majengo hayo yatolewe na si kwa kulipa, yatolewe bure kwa Chuo Kikuu Huria. *(Makofi)*

Mimi nafikiri Rais Mkapa atakuwa anastaafu kweli kwa tabia yake ya kuwajua wanyonge na kuwatetea, atakuwa amemaliza kazi yake vizuri. Hakuna zawadi nzuri ambayo ataitoa kwa Watanzania kwa kweli zaidi ya hii ya kuangalia Elimu kwa watu ambao kwa bahati mbaya walikwishakata tamaa kwamba hawataonja Chuo Kikuu, wako makazini ambako wananyanyaswa na ufinyu wa Elimu yao na wanataka wajiendeleze ili waendelee wapate haki. Mimi nafikiri itakuwa ni zawadi kubwa. Mfano mzuri ni Waziri wa Sayansi na Teknolojia, mimi kama kaka yangu napenda kutangaza kwamba katika watu ambao wamepanda ngazi ya kwenda Chuo Kikuu bila kupitia katika hivi Vyuo ambavyo tunaviona, ukakae darasani *conventional* ni pamoja na yeye. Ameonyesha mfano mpaka sasa hivi ana *degree* sijui tatu. Lakini angekata tamaa na asingepata upenyo asingefika huko aliko. *(Makofi)*

Sasa kwa Watanzania ambao uwezo wao ni mdogo, kwa kweli tutawapatia upenyo kwa kuhakikisha kwamba wanapewa fursa za kwenda kusoma Chuo Kikuu Huria na ndiyo pekee ambako Taifa linaweza kutoa mchango wake. Kwa hiyo, mimi nasisitiza sana kwa ile Mikoa na Wilaya ambazo hazijaonyesha umuhimu wa kutoa majengo kwa ajili ya Vyuo hivi kuwasaidia Watanzania ambao bado hawajakuwa tayari na wamekwishakata tamaa, kuwafikia katika ngazi ya Wilaya, basi majengo yatolewe.

Kwa hiyo, mimi ninaomba hilo na ninaomba sana na nimelizungumza kwa kirefu kwa sababu najua ndiyo pigo kubwa kwa Chuo hiki. Kikipata majengo, kitaelimisha, kikipewa fedha kitaelimisha. Kuwa na udahili na kuwa na wanafunzi 21,000 kwa mwaka, mimi nafikiri hilo ndiyo jibu sahihi. Hivi Vyuo vingine ni kweli tunavihitaji, lakini hatuwezi ku-*turn round* kupata wanafunzi wengi wanaofaulu na kupata Vyeti vya Vyuo Vikuu kama ambavyo tungeweza kufanikiwa kama tukitumia fursa zote za Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuishukuru Serikali, kwanza kwa kukubali kuundwa kwa Chuo hili. Naomba niiombe Serikali iendelee kutochoka kukilea Chuo hiki, ibebe mzigo huu ambao ni mkubwa.  Kwa bahati mbaya, katika watoto ambao wanaweza kuonekana kwamba hawako karibu na baba, ni Chuo hiki, maana hawako mahali wanaweza kupiga kelele wakasikika. Hawa walioko katika Vyuo ambavyo vina mabweni wanaweza kukusanyika kwa haraka wakaungana, wakaandamana, wakasikika. Hawa waliotawanyika nje, nchi nzima kama hatutawasemea sisi Wabunge, hawa watakuwa hawana msemaji.

Kwa hiyo ninawaomba Wabunge wenzangu kwamba kwa kweli kila mmoja anapoamka anawakilisha watu katika Jimbo lake ambao hawajafika Chuo Kikuu. Tukifika hapo kila mmoja akatetea hivyo, mimi nina uhakika Chuo hiki kitaongezewa fedha, kitapewa majengo na kitatekeleza shabaha ya kuundwa kwake. Baada ya kusema hivi, napenda kumaliza kwa kushukuru na kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa siku mbili mfululizo kwa sababu nilikuwa sijachangia chochote, nilikuwa nimeacha sehemu ambazo kidogo nina upeo nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, napenda kuipongeza Wizara chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu; Naibu Waziri, Mama Zubein Muhaji Mhita; Katibu Mkuu, Mama Ruth Mollel; Wakurugenzi Wakuu wa Vyuo na Taasisi mbali mbali na Watendaji ambao walikuwa au wako chini ya Wizara hii kwa kutuandalia hotuba nzuri na kwa kutekeleza majukumu yao kwa uwezo mkubwa waliokuwanao kwa miaka mitano ambayo mimi nilikuwa nao kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii. Kwa hiyo, kwa miaka mitano nilikuwa nao, nimeona jitihada zao na kwa kweli kazi inaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kila penye kazi nzuri hapakosi kuwa na matatizo madogo madogo na wakati mwingine hata na makubwa ambayo tulishirikiana kwa pamoja tunaweza kuelekezana kuona tukafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingine ziwaendee Waasisi 25 walioanzisha Taasisi ya Sayansi Tanzania. Wote wale mimi nilivyowafahamu au ninavyowafahamu, ni Watanzania waliobobea kwenye masuala ya Sayansi. Kwa hiyo, ninaamini Taasisi hii itakuwa ndiyo chemchem ya ushauri wa masuala yanayohusu Sayansi na Teknolojia ndani ya nchi yetu. Niwatakie kheri tu kwamba Taasisi iweze kukomaa na waweze kutusaidia kwa yaliyo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, niunganishe tu mchango wangu wa mawazo na yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Henry D. Shekiffu aliyekaa sasa hivi, sijui kwa nini! Mimi kwenye mchango wangu nilianza *point number one*; Chuo Kikuu Huria sijui kabisa ni kwa nini! Ninadhani ni katika hali hiyo hiyo kwamba Chuo hiki bwana ndiyo kumbakumba kwa wengi waliokosa nafasi ya Shule ya kwenda kwenye mstari ule wa moja kwa moja, unaanza Darasa la Kwanza mpaka moja kwa moja *PhD*. Hii inatoa nafasi kwa wafanyakazi, popote unapoona kwamba unajaribu unaweza kwenda kusoma, basi unaingia.

Pamoja na matatizo aliyotusaidia kutufafanulia, mwenzetu Mwakilishi aliyekuwa ndani ya chungu hiki, mimi napongeza sana kazi inayofanywa na Chuo hiki pamoja na matatizo yake kwa sababu ni cha nchi nzima kama alivyosema, kokoro lisilo na nini sijui. Nimefurahia sana usemi ule. Ninafahamu ndani ya Chuo hiki kwa sababu ni kokoro linalozoa kila kitu. Jamii ya watu wenye Ulemavu hapa ndiyo mkombozi wao mkubwa. Kwa wale wawili, watatu ambao wamejisukuma, wakafika na *Form Six* wakapata na vibarua vya uongo na kweli, hapa ndiyo mkombozi wao, kwamba wana nafasi ya kwenda kusoma moja kwa moja kwa sababu ya mazingira kwamba atabaki kule kule kwake nyumbani. Anatwanga, sijui anafanya nini lakini anasoma.

Tofauti na Vyuo vingine ambavyo itabaidi apande ngazi sijui afanye nini, kwanza hata *structure* ya majengo yenyewe niliyoyaona pale, sana nadhani wamefikiriwa fikiriwa sana tu, wako chini chini huku. Sana hapa nishukuru kwamba Chuo kimekuwa

na kitengo maalum kabisa cha Wanachuo Wasioona kwamba kuna kompyuta maalum ziko pale, kuna na sehemu za kurekodi *modules* zao.

Lakini ninachokiomba, pamoja na matatizo yote, udahili umeongezeka na ninaamini hawa wenzetu wasioona ndiyo wana bahati kweli ya kusoma hata Chuo Kikuu hata Vyuo Vingine. Wasioona wako wengi. Kwa hiyo, hata hapa nategemea watakuwa wengi tu hata kwa mwaka huu. Kati ya hawa 21,000 hawa tunaweza kuambulia hata 200 wakaenda kusoma kwa maana kwamba wanaongezeka.

Ninachokiomba katika kitengo hicho cha *recording,* basi kiboreshwe na kuimarishwa zaidi ili kupunguza msongamano wa wanachuo wanapohitaji kurekodi *module* zao mbali mbali katika masomo wanayosoma. Hata sasa hivi kuna matatizo, kwa hiyo, kwa sababu udahili unaongezeka, ninaamini wataongezeka. Hebu hilo lionwe mapema.

Pia, katika Chuo hiki kulikuwa na kompyuta maalum kwa wanachuo wasioona. Ningependa tu kufahamu; je, kuna mpango gani basi wa kujaribu kuongeza kompyuta hizi kwa sababu kama nilivyosema, hawa natarajia wataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani na pongezi kwa uongozi na utendaji wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Chuo hiki pamoja na matatizo yake, pamoja na udhaifu wake wa hapa na pale lakini kimeonyesha jitihada na dhamira ya dhati kabisa kuweza kuboresha mazingira na miundombinu kwa ajili ya kukidhi haja ya Wanachuo wenye Ulemavu; Wasioona na wa Viungo. Kuna kitengo maalum kabisa, kuna waajiriwa kabisa ndani ya kitengo kile licha ya Walimu ambao ni *specialist* wa mambo ya *brain*, wako pale wanalipwa na Chuo kuweza kuwahudumia Wanachuo wenye ulemavu kuwarekodia, kuwatafsiria na kuwasomea. Kwa kweli wanafanya vizuri kwa sababu wanawezeshwa.

Kuna jitihada ya kurekebisha miundombinu ambayo nimeona. Wanachuo walemavu wa viungo baadhi ya majengo mengi yamerekebishwa. Wametengewa hata na mabweni maalum ambayo angalau wanaweza wakajisukuma nayo kuweza kusoma kwa raha mustarehe. Chuo kimekuwa hata na mpango wa kuweza kuwanunulia hata vifaa vya kujimudu. Kwa kweli ni mfano mzuri. Mtu akitenda jema, mshukuru. *(Makofi)*

**Mheshimiwa Naibu Spika, sasa iwe ni tabia na desturi kwa Vyuo vingine vyote vya Umma vinavyoumuka. Kuna Mtwara inakuja, kuna Mkwawa inakuja, sijui kuna nini inakuja na watu wenye ulemavu wengi wanamudu. Niseme, kwa hali zao wanamudu zaidi kazi za Ualimu. Sasa kuna Vyuo hivi vinaumuka vingi vingi, hivi vitakuwa vya Ualimu. Hebu na hivyo viweze kuzingatiwa kusudi na wao waweze kupata kibarua kilichokomaa katika Elimu.**

Mheshimiwa Naibu Spika, nishirikiane na Kamati kwa sababu ni mdau. Mengi yale yaliyosemwa tulishiriki pamoja na tumeafikiana. Tunadhani Wizara itaendelea kuyatekeleza, lakini ningeomba kukazia, Bajeti ya Utafiti iongezwe. Hata babu zetu walifanya tafiti. Moto haukuwepo, lakini walitafuta, wakapekecha miti, moto ukatoka.

Waligonganisha mawe, ndiyo utafiti wenyewe huo. Hawana vitabu, lakini wali-*develop* kwamba ukifanya hivi kinaweza kikawa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ni msingi wa maendeleo ya maisha. Kwa hiyo, fedha hizi ziongezwe. Kwa sababu kama ndugu zetu huko walijua wakafanya na ndiyo haya yametuletea hata *electricity* kwa sababu *through* mawe waliyokuja watafiti wakatoa nini ndiyo mwendelezo wa mambo. Tujitahidi kabisa kwa nchi maskini kama sisi, utafiti ni msingi ambao unaweza ukakuza teknolojia zetu, teknolojia ambayo inaweza ikatusogeza mbele. Kwa hiyo, ninaomba, hili nalikazia, kwa kweli ni la msingi sana.

Ninachoweza kuongeza hapa, matokeo ya tafiti mbalimbali ambayo yapo na yatakuwepo, basi matokeo haya yawafikie wadau mpaka ngazi za chini kule. Kama alivyosema Mjumbe mmoja hapa, labda hata Kamati zile za Sayansi na Teknolojia za Wilayani huko zikatupiwa haya matokeo, ndiyo matokeo yatafika kwa wananchi huko chini wakaweza kujikwamua kwa yale na lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na kilichosemwa kuhusu migogoro ya *DMT*. La! Kwa kweli haipendezi. Haipendezi na kama Wanachuo na Mheshimiwa Waziri pia asingekuwa na Saikolojia ya Ualimu, Vyuo vingine navyo vilikuwa vinataka kama vinatukutakuta vile, halafu sijui inakuwaje! Kikianza Chuo kimoja, baada ya siku mbili, kingine! Sio inakuwaje, siku hizi si *hallow hallow* tu, *internet*, wanapelekeana simu sisi huku tumefanya hivi. Kwa hiyo, nayo maendeleo ya Sayansi na teknolojia hayo tunashukuru, wanapeana taarifa. Wakiwa na matatizo yaliyo sawa na wao wana-*lay strategies* na kugoma na nini.

Lakini kwa *DMT* kama Kamati ilivyosema kwa kweli mambo haya yalizidi. Inasikitisha mpaka Kamati kushauri kwamba labda uongozi huo ubadilishwe, maana ni kinyaa kitupu. Inasikitisha, lakini sasa penye ukweli mtu unafanyaje? Pamoja na yaliyozungumzwa na Mheshimiwa mwenzangu alishazungumza kwamba labda Viongozi waweze kupewa *education* ya *management* labda na *psychology* na vitu kama hivyo. Lakini ajira za siku hizi najua ni za ushindani, watu wana-*apply* wanafanyiwa usaili halafu anaye-*qualify*, mimi ninaomba hao wanao-*qualify* kwamba mimi ndiyo Mkuu wa Chuo gani, sijui kitu gani, waweze kufundishwa, waweze kupewa msasa wa Utawala Bora katika Taasisi zao ili mambo kama haya yasiweze kutokea tena. Haipendezi! Inaonyesha ulegevu na wakati mwingine mambo ni ya uonezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufahamu kwamba wanafunzi wetu siyo kwamba hawaelewi mambo yanavyokwenda, hata kidogo! *Sometimes they are far than we think*. Si teknolojia, wanajua zaidi wakati mwingine! Kwa kweli, wanajua! Kwa upande wa Walimu, mimi ni Mwalimu, siku hizi lazima kujisomea sana maana unaweza ukaingia Darasani, mtoto akakuuliza kitu alichokiona kwenye *Internet* na wewe hata *Internet* hujui. Kwa hiyo, kwa kweli tusidhani kwamba hawafahamu. Cha msingi ni kukaa nao, kuelimishana na kuweza kuwa na msimamo unaoeleweka na ndivyo tunavyowafundisha kukomaa kushika madaraka ya nchi hii kuliko kuwabishiabishia wakati mwingine. Wenzangu wameyasema na mimi kama mzazi yananiuma wakati mwingine watoto hawa wanapokukurushwa bila utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Wizara hii ione uwezekano chini ya Serikali *of course* wa kuweka mazingira muafaka kwa ajili ya kuwawezesha Viziwi kusoma Vyuo Vikuu. Ni gharama sana najua, basi tutenge angalau Chuo Kikuu kimoja tu nchini hapa kitakachoweza ku-*accommodate* Wanachuo Viziwi kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko katika tembea zangu, hakuna hata kimoja. Waliobahatika wanasoma sijui Amerika, sijui wapi. Wakati umefika na wao waweze kusoma ndani ya nchi yao. Tuchukue hivyo vifaa vinavyohusu huko, tuingize angalau kwenye Chuo Kikuu kimoja tu kwa sababu nao najua hawatakuwa wengi, lakini watafarijika kusoma ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Sponsorship* nje si rahisi na *these people* wanaoweza kupata nafasi. Wana akili kweli ya *Computer Science*, sijui kwa nini. Wana *concentration* ya kuona, hawaghasiwi na kusikiasikia nje, ni mahodari kweli kwa utafiti mdogo niliioufanya. Kwa hiyo, kwa kweli hili ninaliomba, Viziwi hawana Chuo hapa ambacho wanaweza wakaenda kubabaisha kusoma Chuo Kikuu chochote kile hata hicho Huria cha makokoro, hawawezi. Kwa hiyo, hilo ni ombi maalum kusudi angalau na wao waweze kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahishwa na mtindo huu wa kuwasaidia watoto wa kike kusoma kidogo kwanza ili kuweza ku-*qualify* kuingia Chuo Kikuu. Leo nimesikia Sokoine *University* wame-*qualify* kama 44, ndiyo nyongeza hiyo kwa jitihada ya ku-*balance* uwiano wa wanachuo kijinsia kati ya wanaume na wanawake. Sasa ilianza hii kitu na Chuo Kikuu cha Dar es salaam, nadhani Sokoine.

Wito wangu ni kwamba, Vyuo vyote vinavyozuka hapa, hii iwe kama *a must* ya namna fulani, iwe ni Kanuni. Iwe ni Kanuni ili hii *balance* iweze kufikiwa kwa sababu matatizo ya *inequalities* tunazijua. Kwa hiyo, iwe ni kitu kama Kanuni kwamba Vyuo vya Umma huu mtindo uwepo, vya watu binafsi hatuwezi kulazimisha kwa sababu kule nako ndiyo hivyo, mtu anataka biashara yake iende vizuri, lakini vya Umma basi naomba hiki kiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana sana tu na yaliyozungumzwa kuhusu Mfuko wa Mikopo kwa wanachuo. Lakini ninachokiomba basi, taratibu zitakapomalizika fedha hizi wanachuo wapewe kwa wakati muafaka. Kucheleweshewa kunachosha. Wakati mwingine tunawaona Mabenki, kule kuna siku wanalundikana wengi kwa pamoja, masomo kule yanakwenda, huku wanang'ang'ania kale ka-*cheque*.

Kwa hiyo, kuna *delays* za namna fulani. Ombi ni kwamba waweze kuletewa kwa wakati muafaka ili waweze kujipanga wenyewe wangapi wangapi wa kwenda hata kuzichukua kuliko hali halisi ambayo inajitokeza.

Baada ya kusema haya, mimi niendelee tu kutoa pongezi kwa Wizara. Nishukuru, nimekuwa nao kwa muda wa miaka mitano. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kabisa

kwamba anang'atuka. Nimpongeze ameonyesha njia kwamba unapoona kwamba umeshahudumia Taifa kwa wakati fulani vya kutosha, pisha njia ili basi na wengine waendelee kujifunza. Baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Kwa shughuli za kipindi cha asubuhi tunamalizia hapo. Tutakapokutana jioni ataanzia Mheshimiwa Bernard K. Membe. Kwa hiyo, ujiandae na orodha itawekwa kule. Sasa kufika hapo nasisitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.54 mchana Bunge lilifungwa mpakaSaa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niungane na Wabunge wenzangu katika kumpongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa hotuba nzuri aliyoitoa asubuhi na ningependa bila kucheleweshа nimwambie ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kutoa pole kwa wenzetu ambao nadhani wanakaribia 11, walioaga dunia katika kipindi cha miaka mitano ambacho nimekuwa Mbunge katika Bunge hili kuanzia mwaka 2000 hadi sasa. Tunaomba roho za Marehemu hao wote zipumzike kwa amani huko mbinguni. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchana nilipata habari kwamba Jimbo langu limekamilisha uchaguzi wa Madiwani jana usiku na ningependa nitumie nafasi hii kuwapongeza Madiwani wote wa Jimbo la Mtama waliochaguliwa kwa kishindo jana jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nije kwenye mjadala wa suala la Elimu ya Juu. Nitajadili mambo mawili tu. Kwanza, ni suala la wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita kushindwa kupata nafasi ya kujiunga na Chuo Kikuu, lakini la pili ni suala la Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa Kidato cha Sita waliofaulu mwaka huu na waliostahili kwenda kwenye Vyuo Vikuu tumeambiwa ni 22,992 na kati ya hao ni 16,660 ndiyo waliopata nafasi ya kudahiliwa au kuwa *registered* kwenda Chuo Kikuu. Wanafunzi 6,332 tumeambiwa leo asubuhi wamepata bahati mbaya au hawataweza kwenda Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo ambalo linahitaji mjadala wa Bunge. Ni tatizo kwa sababu hawa ni wanafunzi ambao wamefaulu vizuri na kwa kweli wanafunzi wote kila mwaka wanaofaulu *First Division* na *Second Division* ni *materials* za kwenda Chuo Kikuu. Tunapopata wanafunzi 6,332 ambao wanashindwa kupata nafasi ya

kuendelea kwenye Vyuo Vikuu ni lazima tujadili ili tupate majibu ya namna gani tunaweza kuwasaidia wanafunzi hawa kwa sababu tusipofanya hivyo tunajenga *pool* ya wanafunzi watakaokuwa na hasira, lakini pia tunajenga *pool* ya vijana ambao hawawezi kupata ajira.

Njia moja ya kupunguza ajira ni ya kuhakikisha kwamba vijana wanaomaliza Darasa la 14 na waliofaulu kwa *Division* ya kwanza na ya pili kama inavyofanyika kwenye nchi za wenzetu wengine, wanapata nafasi ya kwenda kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yanatolewa kwamba, sababu inayofanya washindwe kupata uwezo huo wa kwenda kwenye Vyuo Vikuu ni Vyuo Vikuu vyenyewe kuwa vichache. Tumeambiwa kwenye taarifa na hotuba ya Waziri kwamba, Vyuo Vikuu vinavyoweza ku-*accommodate* wanafunzi hawa ni 43, lakini vingine vimesailiwa na vingine bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani imefika wakati turudi nyuma na tujiulize kule nyuma tulikuwa tunafanya nini ili kuhakikisha wanafunzi wote waliokuwa wanafaulu kwa kiwango cha *University* walikuwa wanapata nafasi za masomo. Ningependa nikumbushe kwamba, kulikuwa na utaratibu mzuri sana wa wanafunzi hawa wanapomaliza Vyuo Vikuu. Serikali ilikuwa inawa-*sponsor* baadhi ya wanafunzi hawa kwenda kusoma kwenye Vyuo Vikuu vya nje na walipokuwa kule ama Serikali iliwasomesha ama *foundations* mbalimbali ziliwa-*sponsor* ili mradi wanafunzi wengi waliweza kwenda kusoma nje na nafasi ya ndani ilijazwa na wanafunzi wengine pia ambao walistahili kusoma kwenye fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni yangu kwamba, yaelekea utaratibu ule upo holela, hatujawa na mpango madhubuti wa kuziomba nchi marafiki au nchi tunazoshirikiana nazo au *foundations* mbalimbali kuweza kulinusuru Taifa letu kutokana na tatizo hili la kushindwa kupata Shule za wanafunzi wanaostahili kuingia Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nimejionea mwenyewe miaka ya tisini kwamba nje, nchi ya Uingereza, Marekani na Cuba tulikuwa na wanafunzi wasiopungua 900 hadi 1200; Canada peke yake tulikuwa na wanafunzi waliokuwa *sponsored* na Serikali 211; Cuba tulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa wamesajiliwa na kulipiwa na Serikali hii wasiopungua 69 na Marekani kwa maana ya *United States of America,* nadhani kulikuwa na wanafunzi wasiopungua 300. Lakini ilipofika mwaka 1996/97 mpango wa kusomesha wanafunzi nje ukafutwa. Matokeo yake wanafunzi wale waliokuwa wanasoma kule nje wengine waliamua kubaki huko huko, lakini pia tukawa na shida ya kuwajua tu kwamba ni wanafunzi gani wataalam mbalimbali waliohitimu nje ya nchi wa kurudi huku. Maelezo yaliyotolewa ni kwamba nchi ilikuwa na hali mbaya ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashuhudia kwamba nchi nyingine za *SADC*, nchi nyingine za Afrika Mashariki, Kenya na Uganda na nchi nyingine za Afrika bado zinaendelea kupeleka wanafunzi wake nchi za nje na bado *foundations* mbalimbali kama *The Ford Foundation, The Commonwealth Secretariat* na *Full Bright* bado zinaendelea

ku-*sponsor* wanafunzi hawa kwenda kusoma nchi za nje. Ninaiomba Serikali kwamba wakati umefika wa kuomba *Bilateral Countries,* kuomba *International Organization* hasa *Funding Countries,* ziweze kutusaidia kubeba mzigo wa wanafunzi kwani wanayo haki ya kusoma na wanayo haki ya kusomeshwa. Hatuwezi kuwa na maelfu ya wanafunzi katika nchi hii ambao wanakosa ajira, eti pia wanakosa Shule, *it's a disgrace. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda peke yake, *enrolment* ya mwaka 2004/2005 ni wanafunzi 58,000. Nilikwenda pale mwezi Februari mwaka huu 2005, wanafunzi 58,000 ni *Makerere University* peke yake. Sijapata *statistics* za *Kenyatta University,* lakini kwa kweli ni lazima tuwe na *program* nzuri ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu hasa hawa wanaomaliza *Form Six* wanapata nafasi za kujiunga katika Vyuo Vikuu. Ni aibu kwetu kuwa na *Secondary Schools* ambazo tunazipanua na kuhimiza kwamba kila Kata tuwe na *Secondary School.* Leo wakati tukiwa na *Secondary Schools* ambazo hazipo katika kila Kata, tuna *stranded students* 6,332. Hali itakuwaje baada ya miaka miwili/mitatu kama hatutakuwa na mpango madhubuti wa kuongeza *Universities* na bado kuwa-*sponsor* wanafunzi wetu nchi za nje? Hakuna aibu na ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hawa wanahitaji pia Walimu wazuri. Walimu wazuri wa kwenye Vyuo Vikuu vyetu ambao kwa bahati katika nchi hii tunao Walimu wazuri sana, wamesoma vizuri kweli na wengine wako nje, lakini tunayo matatizo mawili ambayo pia ni vyema tukayasema. Tatizo la kwanza ni kwamba, wengi wa Walimu wetu wanaowafundisha vijana hawa hawalipwi vizuri.

Mwalimu wa Chuo Kikuu anapomwona mwanafunzi wake analipwa kule Benki Kuu Sh.800,000/= hadi Sh.1,000,000/= lakini yeye analipwa Sh.200,000/= hadi Sh.300,000/= au Sh.400,000/= hapati motisha ya kuwafundisha wanafunzi hao na kinachotokea ni kwamba tunapoteza Walimu, kwani wanakwenda kwenye Shule za *SADC countries* ambako kuna mishahara mizuri zaidi. Japokuwa anaipenda sana nchi yake, analazimika kukimbia nchi kwenda kufundisha nje. Siyo kwa sababu anaichukia nchi, lakini kama binadamu ana mahitaji na kama binadamu anayo haki ya kutafuta soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka *program* maalum ya kurudisha wataalam na Walimu wetu waliopo nchi za nje na hasa nchi jirani warudi wapate marupurupu na mishahara mizuri inayolingana kwa *standard* za *SADC* na Afrika Mashariki ili waje watufundishie wanafunzi wetu kwa sababu hatimaye *education* lazima iwe ni *investment* itakayoendeleza nchi hii. *Investment* yoyote ina gharama na kwa vyovyote vile tunastahili kuwaomba wataalam wetu kote waliko warudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo la pili ni kwamba, sina hakika kama tunayo *Human Resource Development Bank* au sina hakika kule Utumishi kwenye *National High Level Manpower Location Committee* kama wanajua wataalam wote walioko nje ya nchi yetu ambao ni Watanzania wenye vipaji, wenye utaalam, wenye uwezo wa kufundisha vitu hivi, tunakosa kitu hicho. Ninaiomba tena Serikali, huu ndiyo wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba nchi hii inakuwa na *data-bank* yake ya kujua

Watanzania wake walioko nchi za nje kwa elimu zote ili tunapowahitaji na tutakapotoa *incentive* tuweze kuwaita. Watanzania wengi niliozungumza nao wanayo ari na nia na kwa kweli nguvu ya kutaka kurudi nchini ili kuja kufundisha na kuja kushiriki katika nyanja mbalimbali za utaalam huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa uchungu kwa sababu Watanzania waliopata elimu na waliosomeshwa na nchi hii ni wengi sana. Tumefika wakati tuwatambue, tuwapatie marupurupu yanayohitajika na tu-*invest* katika *education* kwa sababu *investment* ya *education* ni *expensive*. Lakini Waziri mwenyewe alituambia mwaka juzi 2003 kwamba: "Kama unadhani *education* ni *cheap, try ignorance." Ignorance* inakuwa *more expensive* kuliko *education* na maana yake ni kwamba ni lazima tu-*invest heavily* kwenye *education* na ni lazima tujisikie aibu kuwa na wanafunzi waliomaliza Vidato vya Sita katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu/minne iliyopita hadi sasa ambao wanakosa kwenda kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie kwa kuziomba nchi za wenzetu, tuziombe nchi marafiki na turudishe utaratibu kabambe wa *full sponsorship* na *partial sponsorship* na tuzitafute hizi kutoka kwenye *foundations* zote ili angalau tuweze kupeleka wanafunzi kama wanavyofanya nchi za wenzetu. Ninaisemea Angola kama mfano, inayopeleka Cuba kila mwaka wanafunzi 300 na wanakwenda kuchukuliwa na *Boeing* yao *747* kwenda Havana Cuba kupeleka wanafunzi likizo na kuwarudisha. Hatutaweza kufanya hivyo, lakini tuone nchi za wenzetu kama Angola zinavyo-*invest in education,* zinavyo-*invest* katika *human resource capital* kuwaelimisha watu wake kwa sababu ni lazima tu-*invest*. Nchi hii tunazo fedha na tunaweza kutafuta fedha, tunaweza kutafuta wafadhili wa kuweza kuwafadhili wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nizungumzie suala la kilio cha wazazi kuhusu elimu na hasa watoto wanaoshindwa kwenda Vyuo Vikuu na *argument* yangu ni kwamba, wale wote wenye *Division* ya Kwanza na *Division* ya Pili bila *cut-off* walistahili na bado wanastahili kwenda *Universities* za ndani na za nje na hiyo iwe *challenge* ya Serikali hii. Ahsante na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana huu ili kuchangia hoja ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Kwa vile nimeshatoa rambirambi kwa wenzetu waliotutangulia huko kuzimu, lakini nilikuwa bado sijatoa rambirambi kwa Marehemu Margareth Bwana, wale ndugu pamoja na marafiki wa Marehemu Margareth Bwana, namwomba Mwenyezi Mungu awafariji na ailaze mahali pema roho yake. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuunganisha pale alipoishia Mheshimiwa Bernard Membe kuhusu masuala kwanza ya kuwaenzi wasomi wa Elimu ya Juu. Kusema kweli tatizo hili katika nchi hii kama tusipoliangalia tutapiga *mark-time* hapo hapo, hata maendeleo tunayodhani na tunafikiri kwamba tunatamani yaje, yatakuja pengine 1/5 au inawezekana ikawa hata chini ya hapo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumsifu Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba waliyotoa, lakini nataka nitoe hayo mwishoni baada ya kutoa dukuduku langu.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano hai. Nilikuwa na Walimu wenzangu Watanzania pale *Nairobi University* watatu/wanne, mmoja akiwa ni Profesa Kaniki. Tulikuwa tunazungumzia masuala ya Maendeleo ya Taaluma Tanzania na hasa hasa wale walioko nje kurudi nchini. Mimi baada ya kumaliza *Edinburgh University* ilikuwa niende kule Australia, nilikuwa na matatizo yangu binafsi, ilibidi nirudi Tanzania. Bahati mbaya wakati ule katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikuwa na Idara ya Falsafa, kwa hiyo, nikalazimika niende Nairobi.

Basi niliyokuwa nayapata kwa wenzangu waliokuwa wamenitangulia pale ni kwamba, Tanzania wataalam hawaenziwi na kila juhudi wanayoifanya inaonekana kama wanacheza mchezo usiokuwa na maana yoyote! Baada ya mwaka mmoja/miwili nikamkosa mwenzangu Profesa Kaniki, akaenda Kusini huko Botswana na sasa hivi sijui yuko *South Africa* au yuko Namibia, sielewi. Lakini tatizo kubwa ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa asubuhi Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alisema ile *brain drain* sasa inageuzwa kuwa *brain gain,* mimi hiyo kasi ya *brain gain* siioni. Mwenyewe anasema maneno hayo ni ya Mheshimiwa Rais na siyo yake yeye.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, tatizo ni hilo na ninaomba Mheshimiwa Waziri anisikilize sana, kama tusipoangalia masuala ya kuwaenzi hawa ambao wanafundisha, tutakosa Walimu. Wanafundisha vijana ambao wanakwenda katika Taasisi mbalimbali, Benki na kadhalika, wanapata mishahara mikubwa zaidi kama Sh.1,500,000/=, Sh.1,200,000/= au Sh.2,000,000/= na kadhalika, wao amepata sana Mwalimu pengine Sh.450,000/= au Sh.500,000/=, amekwenda sana Sh.550,000/= mpaka Sh.600,000/=. Hivi unategemea huyu atakuwa anapika tu chakula kinaliwa na wengine! Huyu mpishi siku moja atakula chakula kile, atakaa chini ale. Yeye mwenyewe anataka kula, wewe unataka apike tu wengine wale! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isingekuwa kugombea Ubunge mwaka 1995 nisingerudi ndugu zangu na nikimaliza kipindi hiki naondoka. Eeh, ndiyo! Natafuta nini kukaa hapa!

**MBUNGE FULANI:** Hutaki *Umufti*?

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Hata *Umufti* siutaki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hali halisi! Hivi mnategemea nifanyeje? Huo ndiyo ukweli na ninadhani wakati muafaka umefika, bila ya kuwaenzi hawa, hiyo *brain gain is not in reality.* Kweli kabisa, hilo mlijue wazee wangu, ndugu zangu na Waheshimiwa Wabunge hapa, bila ya kufanya hivyo hakuna njia nyingine wale wataondoka wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia *statistics* za *Higher Education*, nimeona Maprofesa jinsi wanavyopungua. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale wamepungua mpaka sasa hivi wamebakia kama 32 katoka karibu 65 au 66. Ni lazima watu waende katika malisho ambayo ni ya kijani kibichi. Unaendelea unasema *globalization.* Hii maana yake ni kwamba, wale watu mafukara wawe mafukara zaidi na wale matajiri watajirike zaidi, haiwezekani! Ninaomba suala hili ni lazima tuliivie macho, vinginevyo tutakuwa tunazungumza hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukuza vipaji maalum vya Sayansi na Teknolojia, ninaishukuru Serikali hasa wale waanzilishi 25 walioanzisha Taasisi ya Sayansi Tanzania. Ninaishukuru Serikali kwa kuwaenzi kwa kuwapa vyeti pamoja na kutambua shughuli zao, lakini pamoja na hivyo, hiyo bado haitoshi, itabidi iwe ni lazima kukuza vipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapozungumza pale katika ibara ya 30 ukurasa wa 25 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia katika mambo iliyofanya 2004/2005, moja ni kufuatilia wabunifu na Wagunduzi wenye vipaji maalum katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mwanza, Rukwa na Kagera na jumla ya vijana 26 walipatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Pwani, katika Jimbo langu kulikuwa na watu wawili ambao walikuwa Wagunduzi, tena wamefanya kazi nzuri ya kugundua mashine mbalimbali nyingine ni *manual* za kuendesha kwa mkono na nyingine kwa kuendesha kwa betri ndogo ndogo tu. Ninamsema mtu mmoja hapa anaitwa Malimwengu. Yule Ndugu Malimwengu amegundua mashine nyingi za kufanyia kazi, kurahisisha kazi Vijijini kama za kuvunia pamba, kuvunia mpunga, kumwagilia mikorosho na kadhalika. Lakini bahati mbaya tena kwa masikitiko makubwa mashine zile zikachukuliwa wakasema: "Tunakwenda kuziangalia huko Kibaha Makao Makuu ya Mkoa." Baada ya kwenda kuangaliwa Kibaha, yule bwana akatiwa msukosuko, baada ya kutiwa msukosuko sijui alifungwa au nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo mashine hizo hatujui zilipokwenda na hakuna chochote! Amekatishwa tamaa, nini maana yake? Mimi Mbunge wake nimekuwa nikipiga kelele, lakini sikupiga kelele katika njia ya kulia, hapana, nilikuwa ninakwenda huku na kule, lakini mwisho sikuujua. Yule mtu badala ya kupewa ari ili aweze kuendelea zaidi akakatishwa tamaa na ameacha shughuli hizo sasa. Hivi Mheshimiwa Waziri halioni hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wenye vipaji maalum ingawa Mheshimiwa Waziri anasema hapa kwamba walienziwa, mimi sioni wale watu wangu wawili kwani wamekatishwa tamaa kabisa. Ni kwa nini hawa walio na vipaji maalum wasiendelezwe? Wasitafutiwe njia/mbinu na kupewa uwezo zaidi pamoja na nyenzo ili wafanye vizuri zaidi? Kuna tatizo gani? Kuna wivu gani? Ni kitu gani ambacho nchi hii itapata hasara ikiwa hawa wataenziwa na kuendelezwa vipaji vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya Elimu ya Juu maana yake ni kwamba na Vijijini huko tuendelee. Kama Vijiji haviendelei na watu kule Vijijini hawafaidiki na Elimu ya Juu, maana yake Elimu ya Juu haina maana yoyote, itabakia ni kitu cha kuzungumzwa tu katika vitabu pamoja na *Alf Lela Ulela.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwamba, kama kweli tunataka tuendelee, basi wale wenye vipaji maalum, wale Wagunduzi ni lazima tuwashike kweli kweli na kuwasaidia na kuwapa nyenzo ili waendelee zaidi, siyo kuwakatisha tamaa. Hivyo ndiyo walivyofanya wenzetu Japan, wamefanya wenzetu India na kwingineko. Japan walichukuliwa vijana wa wakulima wakaenda kusoma, *within 25 years* wakarudi nyumbani, wakaenda kule Vijijini wakapindua maisha yote yale ya kilimo kama kilimo cha mpunga na kadhalika, wakapindua mashamba yale yakageuka kuwa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka namna hiyo, siyo tunazungumza tu kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha kufa na kupona, hizo ndiyo sifa za kilimo. Tunapindua kwa kupeleka watoto wasome Elimu ya Juu, warudi wafanye kazi. Ikiwa tunawakatisha tamaa hakuna njia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Membe alisema kwamba, wanafunzi 58,000 wako Chuo Kikuu cha Makerere. *Kenyatta pamoja Nairobi* walichukua wanafunzi 70,000 katika Chuo Kikuu. Wenzetu kule wana mpango wa *eight, four, four.* Miaka minane ya *Primary*, miaka minne ya Sekondari na miaka minne ya Chuo Kikuu na huo mradi unaanza mimi niko pale na wamefanikiwa vizuri sana. Mwanzo walisema sijui huu mpango wa *eight, four, four* hautafaulu. Umefaulu vizuri kabisa! Sasa nasema hayo ndiyo mapinduzi tunayoyataka. Sisi tunachukua wanafunzi 22,000, tunashindwa kuchukua wale 9,000 tu! Wanakaa nje, watafanya nini? Hii maana yake nini? *(Makofi)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kengele ya kwanza imelia, nasema kwamba ninaisifu Wizara kwani inafanya kazi nzuri, lakini waongeze kasi kwa sababu mahitaji yetu sasa kwa Tanzania ili kwenda mbele zaidi ya Kenya na Uganda ni makubwa. Wenzetu wale wako mbele, soko la ajira lile la Afrika Mashariki likija, ile *free movement* ya *labour* tayari tumekwisha. Vijana wetu siyo watakuwa vijiweni tu, bali watakuwa katika virago au katika sehemu gani, sijui! Wao watakuwa maboi wa kufyagia tu, lakini kazi nzuri zote zitachukuliwa na vijana wa kutoka Kenya na kutoka Uganda kwa sababu wao ndiyo wanaosomesha, sisi tunafanya mchezo, tunasuasua.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti, namsifu rafiki yangu, Dr. Pius Ng'wandu, tulikuwa wote katika Taasisi ya Elimu. Mimi nilikuwa katika Baraza lake, yeye akiwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima wakati ule wa miaka ya sabini.**

**Kwa hiyo, namjua ni mchapakazi mzuri sana. Pia, Mheshimiwa Zabein Mhita namjua tangu akiwa pale Wizara ya Elimu, amechapa kazi kweli kweli akiwa Mkurugenzi wa Shule za Msingi. Nisimsahau Mama Mollel, anafanya kazi nzuri.**

**Lakini nasema mwongeze kasi ili tuweze kuwawahi wenzetu wale wa Kenya na Uganda au la sivyo vijana wetu hawa wataishia Mitaani na tutaongeza balaa zaidi. Nawashukuru sana kwa kazi mliyoifanya na sasa hivi maendeleo yanaonekana na mfanye juhudi zaidi ili mambo yawe mazuri zaidi.** ***(Makofi)***

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote niliyozungumza, ninaunga mkono hoja na ninaomba yatiliwe mkazo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa. Sijui kama *Hansard* imechukua *krkrkrrr.* Kama watakuwa wamechukua, watakuwa wamejitahidi kweli watu wa *Hansard*. *(Kicheko)*

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na moja kwa moja niungane na wenzangu kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo asubuhi. Mimi imenifurahisha sana na ninasema ninaiunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa, kila nchi inahitaji kuwa na Kitengo cha Sayansi na Teknolojia kama vile ambavyo tunacho sisi wenyewe. Lakini sisi kama nchi nyingine nyingi ambazo zinaheshimu maendeleo, tuna Wizara hasa ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Katika dunia ya leo Sayansi na Teknolojia hasa upande wa '*R' and 'D'* yaani utafiti na maendeleo, ndiyo hasa ni ncha ya mkuki ambayo inaongoza maendeleo ya nchi na ukitazama nchi za nje maendeleo yao yote, macho yao yote yapo katika Vyuo Vikuu.

Vyuo Vikuu ndiyo wakombozi wa maendeleo yao na ustaarabu wa *modern world* kama ilivyo hivi sasa. Ni kweli kabisa kwa sisi hapa Tanzania tunazalisha *graduates* wengi, hatuna idadi yao ambao wako nje kama alivyoeleza Mheshimiwa Membe na ni vyema tukajua idadi yao ilivyo.

Lakini ningependa nizungumzie hasa juu ya *R &D* katika mambo ya utafiti, *scientific research* nataka ni-*concentrate* katika hilo. Leo baada ya miaka 45 kuzungumzia jiko sanifu la mkaa, kwa kweli ni aibu kabisa. Gerezani kuna watu pale hawajakwenda Shule kabisa. Sweden wanatengeneza *welding machine* ambayo inaaminika sana. Lakini *welding machine* inayotoka Sweden haiwezi kufanya kazi kwa masaa matatu mfululizo.

Gerezani unakuta vijana wabunifu wanakutengenezea ile *machine* ambayo inaweza kwenda kwa masaa tisa bila ya kupumzika. Wamekuwa wabunifu kujua ya kuwa kitu ambacho kinapooza mashine ile ni yale mafuta ambayo yanatoka kwenye *transformer*. Si jambo zuri kweli lakini huo ni ubunifu ambao tunauhitaji utoke kwenye *Universities* zetu. Kusema ya kuwa umaskini ni hoja au ndiyo sababu, kwa nini hatuna fedha nyingi ambazo zinaingia katika utafiti huo kwa hakika siyo sababu, kwa sababu nchi ambazo zilipata uhuru baada ya sisi nchi za Asia kama vile Indonesia, Malaysia,

Korea na nchi kama hizi zote zimetumia ubunifu wao wenyewe na wameweka fedha katika *R &D* ndiyo maana wamefika hapa walipo hivi leo. *(Makofi)*

Sasa mimi najiuliza, tatizo letu hasa ni nini? Ukosefu wa fedha, ushawishi mdogo upande wa Serikali kwa wataalam wetu au ni dharau tu kwa upande wa Serikali? Bado sijajua. Lakini ukweli ni kuwa fedha kiasi kidogo mno ndicho ambacho kinaingia katika utafiti wa kufanya mambo ya ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia kuhusu *graduates*. Ni kweli *graduates* wengi wako nje na hatujui idadi yao, basi angalau kama alivyosema Mheshimiwa Membe tena japo tuwe na *data base* lakini vile vile tuwe na ki-*organization* ambacho tunaweza kukitumia kama *conduit* ili hawa wote wanaotoka nje kwenda kufanya kazi nje wawe wanapitia huko ili tuweze kujua basi na sisi ni *exporters* wa *manpower*. Hata hiyo hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Juma Mikidadi amezungumzia kuwa Maprofesa huko *University* wanapungua, kweli wanapungua na wengi wao wako hapa. Leo ukizungumza na Mheshimiwa Magufuli kwa fahari sana atakwambia yeye ni mchanganya madawa akiwa na maana ya kuwa ana *degree* ya *chemistry*. Sasa unaona ajabu kwa nini hayuko huko kuvumbua madawa ya kutibu magonjwa kama ya UKIMWI badala ya kuwa mnyapala mkuu anayesimamia ujenzi wa barabara. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Mwandosya *is a world class electrical engineer*. Profesa Kapuya mwaka 1987 alinifanyia mimi kazi nzuri sana. Nilikwenda kwake anifanyie utafiti juu ya kupanda uyoga lakini sehemu za Pwani zenye joto. Akatengeneza *hybrid* nzuri kweli ambayo unaweza kuiotesha kule Pwani. Mimi mwenyewe nikapoteza *interest* lakini Mheshimiwa Mzee Rashid Kawawa akachukua mradi ule na anaufanya kwa ufanisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Mikidadi nadhani angekuwa *first class Mufti* wa BAKWATA lakini yuko hapa. Sasa mimi silaumu kabisa. Nadhani naelewa kwa nini ile fikra iliyowaleta huku, ni kitu gani kilipelekea wao wakaja huku. Naelewa kabisa na naona ni sahihi na naiunga mkono kwa sababu Serikali kule walikokuwa ili wawe wabunifu katika *research* hawakupata hadhi, hawakupata marupurupu mazuri, hawakupata heshima na wala hawakuungwa mkono. Kwa hiyo, wakaona bora waje hapa labda watageuza mambo. Mimi nakubaliana na hilo. Lakini mnaona *system* ilivyokuwa ngumu kubadilika? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi inawajibika kubeba msalaba wake na hakuna mtu mwingine anaweza kukubebea msalaba huo. Nakumbuka miaka ya nyuma tulikuwa tunazungumzia habari ya *transfer of technology*. Hakuna kitu cha bure. *Transfer of technology,* nchi zilizoendelea haziwezi kukupa *technology* ya bure. Wakikupa wewe ukatengeneza gari lako, gari atakalolitengeneza yeye atamwuzia nani? Wewe utakuwa *market* tu! Ni wewe mwenyewe lazima utenge fedha, lazima ushawishi watu uwape moyo ili *research* na *development* iweze kukua katika nchi na unapokuwa na majanga kama vile janga la Ukimwi au malaria na vitu hivi nataka nizungumzie. *(Makofi)*

Kwanza kabisa wewe mwenyewe lazima uwe mbunifu, uweze kuunda *system* ya kuweza kukabiliana na janga hili. Lakini leo tumekaa sisi, fedha za kudhibiti Ukimwi zinatoka nje, madawa yanatoka nje, sasa tuna vitu vinaitwa *ARV* zinatoka nje. Lakini *South Africa* wana janga hilo kubwa wanatengeneza dawa zao wao wenyewe ni wabunifu, India wanatengenezea dawa zao, nchi nyingi za Asia wanatengeneza dawa zao wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema, nitagusia vitu hivi viwili, haya ni majanga makubwa, Ukimwi na Malaria. Nagusia makusudi kabisa ili iweze ku-*magnify* mapungufu yaliyokuwepo katika *scientific research organisations* tulizokuwa nazo sisi wenyewe.

**Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukimwi, tunaambiwa kuwa *prelevance rate* ya Ukimwi imeshuka kutoka asilimia 14 mpaka kufikia asilimia 7.3 mwaka 2004. Mimi sina uhakika kama takwimu hizi ni sahihi, nadhani bado wako watu wengi ambao wanakufa wanaokufa bila ya Mamlaka husika kujua. Kwa mfano Makete kwa mwenzangu hapa Mheshimiwa Dr. Kitine maambukizi bado yako kwenye asilimia 25 lakini yeye atakwambia iko kwenye asilimia 15, hajui. Huko Mbeya iko kwenye asilimia 17, 18 na kadhalika. *(Makofi/Kicheko)***

Sasa mimi nasema haya kwa uchungu, lakini inanibidi nishukuru *global fund* na Taasisi nyingine husika kwa ufadhili wao mkubwa wa madawa ya kurefusha maisha kwa Waathirika wa Ukimwi, wanaziita *ARV*. Msaada huu ni mkubwa kwa sababu ambao utawasaidia wao wenyewe waweze kujisaidia na kuendesha maisha yao na kutunza familia zao na vile vile kujenga Taifa.

Lakini vile vile tukae kitako tufanye *research* tutazame pamoja na hayo yote. Labda nisisitize juu ya ufikishaji wa madawa haya kwa walengwa kwa ufanisi zaidi. Hiyo peke yake inataka taaluma, inataka utafiti. Pili, nitahadhirishe kuwa suala la uadilifu lazima lihimizwe na kusisitizwa hususan kwa njia ya ushauri nasaha.

Kama hatutafanya hivyo, nachelea kusema kuwa tunaweza kujikuta tunatengeneza mtandao mpya na mpana zaidi wa maambukizi ambapo hawa ambao sasa watapata afya mpya wataanza kuanzisha zao jipya la kueneza Ukimwi kwa vijana wetu hususan wanafunzi na sehemu ya jamii ambao uelewa wao ni mdogo na wakaingia katika mtego wa hili janga. Kwa hiyo, uadilifu ni kitu muhimu. Vile vile tuunde chombo cha kuweza kuwafuatilia hawa kuhakikisha ya kuwa ni waadilifu.

Pia, janga la Malaria ambalo vile vile kwa sababu hatuna *scientific research* yetu sisi wenyewe tunayoifanya, tunakubali mawazo na ushauri kutoka nje. Tunaelewa janga hili lilivyokuwa kubwa, hapa kwetu Tanzania linaua watu 100,000 kila mwaka, lakini athari yake siyo kuua watu tu ina athari kubwa zaidi kwenye jamii.

Kwa mfano akina mama, wengi wao mimba zao zinaharibika *simply* kwa sababu ya *parasite* wanaingia kwenye *placenta* wengine wanapata *chronic anaemia* na pale

Malaria inapofanya urafiki na umaskini na *malnutrition* ambayo husababisha jamii yetu ya takribani asilimia 60 kuna na hii *haemoglobin* ya asilimia 30 mpaka 35 hawa wote ni wagonjwa watupu, ni kama maiti tu wanaotembea. Basi utaanza kujua janga hili lilivyokuwa lina hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ukosefu wa utafiti *(scientific)* pale unapomkuta mkulima akishafika saa nne analima na jembe la mkono, saa nne asubuhi amechoka anakaa chini ya mti unaweza ku-*understand problem* ya jamii, Taifa zima lilivyo. Mimi siamini kabisa ya kuwa vyandarua vya ngao eti ndiyo jawabu la kuondoa Malaria katika nchi hii. Huo ni udanganyifu. Sijui kwa nini Serikali yetu inaunga mkono hiyo. Ukiangalia matangazo ya kwenye *television* na matangazo mengine kwenye magazeti yote hayana ukweli. *(Kicheko)*

Mimi inanikumbusha Mheshimiwa Semindu Pawa siku alisimama hapa na amefanya *scientific research* kweli kweli akauliza swali akasema; je, Malaria iko kwenye kona nne za kitanda tu? Je, hao waendao *grocery* saa za jioni wavae hizi chandarua kama hijabu? Alifanyia *research* huyu bwana! Yeye hakupata jawabu la kutosheleza kwa sababu sisi wenyewe kwa ujumla wetu hatuna jawabu la kutosheleza kuhusiana na Malaria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akitokea Mganga akasema mimi nina uwezo wa kuweza kuondoa Malaria kwa kutumia ndumba, nitaweka vibuyu nitatundika kwenye milango ya nyumba mbu hawataingia, basi fedha za *WHO* na Wafadhili zitakuwepo zitampa. Kwa sababu nchi zilizoendelea hawana nia ya kutaka kutoa Malaria katika nchi za Afrika. Wanataka Malaria iendelee kwa sababu viwanda vyao vinavyotengeneza dawa za Malaria vyote vitafungwa. Sisi hatufanyi utafiti wetu na janga hili tumeanza kulipata toka tuanze kuacha kutumia *DDT*.

Wameipiga marufuku *DDT* lakini mpaka leo hakuna hata ushahidi mmoja unaweza kutueleza madhara ya *DDT*. Wao wenyewe *America* kulikuwa na Malaria, Canada kulikuwa na Malaria, nchi zote za *Europe* zilikuwa na Malaria na wakatumia *DDT* ku-*eradicate* Malaria. Sisi tunazungumzia *control* ya vyandarua, tunataka *eradication*, *eradication* itatokana na *DDT* kama walivyofanya wao. *(Makofi)*

Sasa labda nieleze vipi *DDT* ilipigwa marufuku. Nimefanya ka-*research* kadogo na mimi kama Mheshimiwa Semindu Pawa, alitokea mwanamke mmoja anaitwa Rachel Carson alikwenda kwenye Bustani yake akakuta ndege amekufa akatafutatafuta akasema; alaa, ndege huyu amekufa kwa sababu alikula funza wa ardhi ambaye aliathirika na *DDT*. Akaandika kitabu, kitabu kile kikadakwa na Makampuni ya Madawa na wakaifanyia *propaganda* wakailazimisha Serikali ya *America* kuunda Tume ili iweze kusikiliza athari za *DDT*. Tume ile ikakaa miezi saba wakasiliza wataalam kutoka nchi zote duniani na wote wakasema *DDT* haina madhara.

Yule *Chairman* wa Tume ile aka-*decide* mwisho akasema ningependa nim- *quote* akasema: "*DDT should not be banned*, *DDT is not casinogenic whatever that means*,

*mutagenic, teratogenic*, *to men and these uses of DDT do not have a deleterious effect on fish, birds, wildlife or estuarine organisms.*"

Yule bwana aliyesema hivyo jina lake ni Sweeney. Lakini baada ya miezi miwili, *Boss* wake aliyeunda ile Tume aka-*overturn decision* ya Bwana Sweeney aka-*ban DDT.* Alipo-*retire* yule bwana Waandishi baadaye wakamwendea wakamwuliza: "Kwa nini wewe uli-*overturn decision* aliyo-*decide upon Chairman* wa Tume yako? Akasema sikiliza bwana *and this is what he said* "*Science along with economics has a role to play in society but the ultimate decision remains political."* Kwa hiyo, *political decisions* za *America* zinaua mamilioni ya watu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umenipa nafasi, naomba ifanyike *research* ya *DDT* turudi kama wanavyorudi kwenye *DDT* nchi nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saggaf kwa kweli umefanya *research* nzuri sana nakushukuru sana. Dr. Hassy Kitine tukusikie na wewe. Mambo hayo!

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi siyo mtaalam wa *research,* lakini naweza kubabaisha wakati fulani fulani. Kwanza ninaomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi kwa sababu najua una ufinyu wa nafasi katika mchango. Halafu nimpongeze Mheshimiwa *Dr. Ambassador* Pius Ng'wandu kwa hotuba yake nzuri sana. Ni nzuri na fasaha. *(Makofi)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hivi, kwa kweli ningemshangaa sana Mheshimiwa Dr. Ng'wandu kama angetupa hotuba *anything less than that* kwa sababu gani, kwa sababu Waingereza wanasema *behind the success of every man there is a woman. In the case of Dr. Ng'wandu, he does not only have one woman and I will explain. According to him he was mentioning to me* kwamba ninajua *he has two women in the Office.***

***That is big enough to have him success, he has a women at home and he was telling me that one of his daughters is here. So,* kwa kweli huyu ana *women* wanne. Sasa angeshindwa vipi kutupa hotuba ambayo kwa kweli ni murua? Kwa hiyo, nampongeza sana, napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba naunga mkono hotuba hii. *(Kicheko/Makofi)***

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo akina mama wanne tu, lakini Mheshimiwa Dr. Ng'wandu ana *cream of our society behind his Ministry***.** Kwa hiyo, hawa watu wasomi wote *top brace in this country* na Wenyeviti wa *Vice Chancellors* wa Vyuo vyetu mbalimbali wako hapa. Mzee Kaduma, kaka yangu nimemwona hapa na wenzie na wengine. Sasa hana sababu ya kutoa hotuba mbaya. Kwa hiyo, pongezi hizi anastahili moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hivi, nataka kusema hivi, kuna matatizo mawili ambayo kwa kweli tunatakiwa tuyatafutie ufumbuzi. La kwanza,

Watanzania walikuwa hawana tabia ya kukaa huko nje. *This is the only country in Africa* ambayo watu wake *all the time* walikuwa wanakwenda nje wanarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekaa miaka 15 huko nje na nimefundisha, mimi ni Mwalimu mzuri tu, nimefundisha huko miaka kumi kwenye Vyuo vya Wazungu hawana akili hata kidogo! Vijana wetu wana akili kweli kweli hawa!

*This is true*, *this is a fact.* Hawa *they have a lot of machinery to support them, but* hawa vijana wetu, *they are better*. Nimefundisha huko, nimerudi nimefundisha hapa, nime-*compare*. *So I know what I am talking about.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukisema namna hiyo, halafu tunakuwa na vijana zaidi ya 6000 hawana nafasi, *this is criminal*. Tunafungua Shule kwenye Kata *as somebody said* halafu wanafunzi 6000 hawaendi Vyuo Vikuu. Sasa *this is lack of planning. If we cannot plan* kutoka chini mpaka juu, tatizo hili hatuwezi kulitatua *and it is a very serious problem in my view. (Makofi)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali itazame ni namna gani ya kuweza kulitatua hili tatizo *and to me this is much more serious* kuliko tatizo la Watanzania ambao wako nje wanatafuta maisha kama nilivyosema. Huko nje wako watu, kuna kijana mmoja, siyo kijana nadhani alikuwa nyuma yangu miaka miwili anaitwa Profesa Michigen inawezekana baadhi yetu tunamfahamu yuko Namibia sasa hivi. Wanamheshimu wale Viongozi wote wa nchi za *SADC.* Anakwenda kuwapa *lecture* Marais wote kwenye mambo ya *development* ya uyoga. Sisi tumeachana naye hapa akaondoka akaenda huko.**

**Yuko mwingine siyo msomi, lakini ni *engineer* kabisa aitwa Saimon Mhavile, yeye alikuwa mkubwa wa *TANESCO* hapa miaka sijui mitano/sita/saba tukamtupilia mbali, tukasema hafai, hana chochote! Sasa hivi ni mkubwa wa Shirika la Umeme Lesotho.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo tunayachezea chezea. *We have to solve some of these problems* na *return on investments in human capital investment, that is education, return* yake *takes a long time, it can take 20 years minimum*. Kwa hiyo, hawa watoto 6000 ambao hawajakwenda Vyuoni na wote wangekwenda *almost all of them* wangepata shahada. *It can take 20 years from now and 20 years from now is a long time*.**

**Kwa hiyo, kuna matatizo. Hawa vijana wapo, Ukimwi unasaidia wanaondoka wengine, Walimu wanakufa. Nchi yetu *is one of the poorest countries* katika dunia, *in terms of per capital income* watu wanaishi *on less than a dollar a day*. Sasa *we must be very serious* kwenye matatizo haya ya *long term investment*. Kwa hiyo,**

**matatizo haya mawili naomba sana Serikali ijue namna gani tunaweza kuyatatua. *I know it is difficult*, lakini *somehow* kuwe na *some vision* ya kutazama vitu gani Serikali itafanya. *(Makofi)***

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu, nina muda wa dakika kama sita/saba, lakini haya kwa kweli nimeyapata sasa hivi baada ya michango ya wenzangu hapa. Lakini niliyotaka kusema ninajua sana kwamba mimi kwa kawaida nimekuwa *controversial, I know it,* lakini na hili nakuonya inawezekana kabisa likaleta *controversy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu mmoja msomi mzuri sana, katika nchi hii akaniuliza siku moja kama mwezi mmoja uliopita akasema: "Ninyi bwana huko Bungeni kuna nini? Mbona hii *Ph.D* mnaionea sana?" Yeye ni msomi sana. Mnaionea hii *Ph.D* kila siku mnaamka asubuhi kuna mtu ana *Ph.D*, siku ya pili *Ph.D*, siku ya *tatu Ph.D*, siku ya nne, *Ph.D*, siku ya tano Dr. Kitine, siku ya sita Dr. Kahumbi, siku ya saba, Dr. Choya, siku ya nane Dr. Mjaka, siku tisa Dr. Wegga, siku ya kumi Dr. Wejja. Sasa huko kuna nini? *(Kicheko)*

Nikamwambia *look,* hii siyo ndani ya Bunge tu, hata huko nje wako. Wako kwa mfano Mheshimiwa *Chancellor* Kaduma *and I hope I am not right.* Nikamwambia kwa mfano kule kwa Mzee Kaduma, Chuo chake Kikuu kile wako watu wanasoma *program* sijui *Master of Science* au sijui *Master* ya nini, halafu wiki hiyo hiyo anamaliza na *Ph.D* anapata wakati huo huo. Sasa anakuwa amepata *M.A* au *M.Sc* halafu na *Ph.D* wakati wa hizi wiki mbili hizo hizo. Sasa nikasema *this is a very serious problem. It is criminal again* bwana *chairman* ni *criminal* haya mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa kifupi, maana yake nini hizi *Ph.D*, ziko namna mbili. Ya kwanza ni *Ph.D* za heshima na nitaomba nichukue mfano hapa. *Ph.D* za heshima, Baba wa Taifa alikuwa na *Ph.Ds* nyingi tu za heshima. Mzee wetu Malecela ni Dr. Malecela ana shahada ya heshima.

Halafu Dr. Mzindakaya ana shahada ya heshima. Mimi nawaheshimu sana hawa watu, kwa sababu hizi ni *ordinary Ph.D* ambazo ni *recognition* ya *institutions* ambazo zimewapa hizo shahada *for original contribution to these institutions in a way that they have done it*. Dr. Mzindakaya *knows*, Mzee Malecela anajua, Mwalimu alikuwa anafahamu, alikuwa anafanya *contributions*. Hizi ni *Ph.D honorary* na ni *recognized*. *(Makofi)*

Halafu *Ph.D* ya aina ya pili ni *academic,* ambayo ni *Intellectual*. Sasa ziko za aina mbili. Ziko za Ulaya, *Western Europe* hizi *mainly* ni *research Ph.Ds* ambazo mtu anakwenda anakaa pale na anakuwa na *Chairman* wake na Kamati ya *degree* yake hiyo anaandika *what they call executive summary* halafu anafanya utafiti kwenye *relevant area,* halafu ana-*produce* kitu kinachoitwa *contribution to original knowledge* katika *field* ambayo anafanya. *Then* anapata *Ph.D*. Hiyo ni *Europe,* wanachukua miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *North America*, Canada, Marekani na nchi zote zinazohusu kule huwezi kupata *Ph.D* chini ya miaka mitano, *impossible*! Huyu Mheshimiwa Membe alikuwa huko, hakuwa anasoma *Ph.D* alikuwa anafanya kazi, lakini anajua haya mambo na wote wengi mnajua. Mheshimiwa Dr. Ng'wandu anajua mwenyewe, unafanya *Ph.D* kule kwanza unafanya *what they call course work* miaka miwili, unakwenda darasani kama mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari. Baada ya miaka miwili unafanya mitihani ambayo ni lazima upate *an average of B+*.

*In fact* unapoingia kwenye *program* hiyo unakuwa umemaliza *Masters*, umefanya *Bachelor* na umepata wanaita *Cumulative (GPA)*. sehemu ya pili unapomaliza shahada ya pili kule, huchukui *less than two years. No, you don't,* ni lazima upate *an average GPA* ya B+ ndiyo unaendelea wanakuruhusu kuingia kwenye *program* ya *Ph.D*. Mheshimiwa Dr. Makongoro atakuwa anajua hivi vitu na wengine. *(Makofi)*

Halafu ukishamaliza *two years of course work* unatoka *and then* una-*propose your thesis/propose/title* halafu inakwenda kwemye *committee* ya Maprofesa watano, *Chairman* wako na Maprofesa wengine *in that particular area and then* uki-*propose* halafu unaandika na zile *chapters headings an then, in fact* nimeruka. Kabla ya hapo unafanya miaka miwili mingine ya *what they call comprehensive examination,* mwaka mmoja na nusu au miwili.

Ukifanya *comprehensive examination* ndiyo unapokuwa-*allowed* kuandika *thesis title* na kuweza *research proposal* zako, halafu unakwenda *into the field* kama unakuja nyumbani huku unafanya au kule kule unafanya unamaliza mwaka mmoja *and that takes five years*.

*Every time* unaandika *chapter* moja, *usually* ni *about 7 chapters*, unaandika ya kwanza, halafu wanapitia wale wote watano kila mmoja ana-*comment* wale Maprofesa wote watano *and these are real Professors* ni watu wenye kusoma kweli kweli. Wanapitia halafu unamaliza moja na *comment* wanaweka, halafu anapitia ya pili, ya tatu mpaka *chapter* ya saba *then* wanasema *now he can defend* unaweza kufanya unavyofanya. *It cannot take you less than five years.*

Sasa jamani hizi *Ph.D* mbona zimeanguka tunakutana humu kwenye *corridor PhD*, tunakutana kule barabarani Mitaani *Ph.D*, tunakutana wapi *Ph.D*. Sasa *this is wrong, it is a criminal*. *I challenge you Mr. Minister,* wewe ni mhimili wa *quality* ya *education in this country*.

Ningependa Mheshimiwa Waziri ujibu hili suala kama Wizara yako haina mahusiano na *quality* ya *education* ya ku-*check* watu, maana yake tunaharibu hii nchi kwa sababu *after another five years* watu wote milioni 35, tutakuwa na *Ph.Ds* wote, kila mtu atakuwa na *Ph.D*! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nieleweke, naweza nikaeleweka kwamba huyu bwana pengine *degree* yake *fake* na nini, pengine anaona wivu wengine wasipate *Ph.D*. Ukienda Marekani au Canada, *library* yoyote ya *College* na *University*, una-*type* tu Kitine, wala usiandike, unaona wameandika *Ph.D thesis, the study of the underground economy in Tanzania*, *Ph.D thesis defence* 1993 na kadhalika. Unakwenda kwenye *stacks* unachukua *call number* unaipata ile *document ya Ph.D*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo tunafanya vipi jamani, mimi *I am requiring,* hizi *document* hawa wanaziweka humu *Library.* Tuweke hapa, mtu anapata *Ph.D* aweke hapa *Library then electronic process* ziende katika Vyuo Vikuu vyote ndani ya nchi yetu hivi, halafu mtu ukienda unafanya *reference.* Unafanya *reference* na kweli unasema ana *Ph.D* huyu Bwana Jumanne Maghembe au mtu mwingine yeyote ana *Ph.D.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani *criminality* hii kwa kweli *we have to do something* na nashauri tulete sheria humu ndani. Kuna hiki kitu *National Accreditation Council* nadhani haina *muscles.* Humu ndani tunasema yeyote anayepata *Ph.D* na tunai-*back date* toka mwaka 1990 kwa mfano, mtu amepata *Ph.D document a full requirements* hizi *including* kuweka hizi *documents* kwenye *Library* maana yake, mambo haya ni *dissemination of original knowledge for the good of the society, so that society becomes better informed, better educated in the future, this is the meaning of it. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *I know this is controversial* kama ulipata feki feki *Ph.D* huwezi kunipenda. Mnanifahamu *it doesn't matter to me* kwa sababu *I don't have anybody in mind, all I am saying is the principal* kwamba *this country we are messing education* kwa kuweka feki *education* ambazo hakuna. Wewe ukiitwa *Ph.D* na hasa sisi Wabunge ni kwa sababu *at the end* unafikiri Bwana Kikwete kesho na keshokutwa akisema *Ph.D* bwana atanichagua kuwa Waziri wake. Kwa kweli *this is wrong, you have to do more*. *This is something to acknowledge, we must not play around* na mambo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tusizitafute hizi *Ph.D* za ku-*lob* pale nje, asubuhi unaona Kitine *Ph.D* kama nilivyosema. Mjaka *Ph.D,* Mzee Kahumbi *Ph.D,* sijui Mzee Janguo, aah! Mzee Janguo nilimsahau *Ph.D.* Lakini hana matatizo yeye. Yeye amesoma *North America,* anajua hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na *otherwise* nashukuru kwa kunipa nafasi na kusema tena. Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, nakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Aah! Mheshimiwa Dr. Kitine leo umetufanyia jioni iwe nzuri sana. Ahsante sana, tunashukuru kwa elimu. *(Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mbunge, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Hotuba hii ni dira nzuri ambayo inatoa mwelekeo wa programu zetu katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tunataka kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara katika kuongeza idadi ya vyuo vya elimu ya juu na ufundi katika nchi yetu kutoka vyuo 23 mwaka wa 1995 hadi vyuo 43 mwaka wa 2005. Katika hali hii Watanzania wengi zaidi wameendelea kupata elimu ya juu jambo ambalo wote tunajivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuona kwamba bajeti zaidi inatengwa kwa elimu ya juu ili kuwawezesha Watanzania zaidi kupata elimu ya juu. Zipo nchi katika Afrika ambazo kwa sasa wamepania kutenga 50% ya bajeti yao kwa ajili ya elimu na Namibia ni moja ya nchi hizo.

Mwisho, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta hoja ya kuanzisha *The Mwalimu J.K. Nyerere Memorial Academy* ambayo huko nyuma ilikuwa ni Chuo cha Itikadi ya Chama Tawala, Kivukoni na baadae kuwa *Kivukoni Academy of Social Sciences.* Ni matumaini yetu na kama nilivyochangia wakati wa kupitisha hoja hiyo kuwa tutaendelea kutengea chuo hicho bajeti kubwa ili kiweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekit, naomba nitumie nafasi ya awali, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri na Bibi Ruth Mollel, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na machache ya kuomba ufafanuzi na ushauri katika kuchangia hoja hii. Je, utaratibu upi unaotumika katika kuwasaidia wanafunzi ambao wazazi hawana uwezo wa kuwasomesha. Hili ni muhimu ili kila mtu aelewe hatua zote muhimu zinazochukuliwa. Kuna hisia za wazazi kutufuata sisi Wabunge kusema kuna upendeleo wa kuchangia. Kwa kuwa wengi huwa hawapati maelezo, ni vizuri Wakuu wa Wilaya hadi Tarafa, Kata wakaelezwa kupitia Serikali zao za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vinavyoanzishwa na watu au Taasisi binafsi vichunguzwe vizuri ili visije vikawa vya utapeli wa kutafuta fedha tu badala ya kutoa elimu inayohitajika kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inafanya mpango upi ili kuangalia mfumo mzima wa bodi ya mikopo. Pia inafanya nini ili kuangalia upya viwango vya posho ili kusiwe chanzo cha malalamiko ya mara kwa mara. Vurugu nyingi hutokana na maslahi. Lazima liangaliwe vizuri na kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuongeza wanafunzi toka 14,076 hadi 48,236 kwa kipindi cha miaka takriban kumi katika vyuo vya elimu ya juu na ufundi, pia kwa kuongeza idadi kubwa ya walimu wa kike. Muhimu pia ni kujaribu kuona ni mafunzo yapi yanayohitajika hapa nchini ili kusaidia kusukuma maendeleo kwa kasi zaidi, ni vizuri fedha zaidi ziwekwe kwenye mafunzo kama hayo kuliko kuendelea kutoa kwa kila kozi bila kuzingatia umuhimu wa mafunzo yenyewe kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mikoa ambayo kodi iko nyuma kimaendeleo ya elimu kama Rukwa, Lindi, Kigoma, Singida na Shinyanga; je, Wizara na Serikali kwa ujumla, si ingejitahidi sasa kutoa upendeleo rasmi kwa wanafunzi wanaotoka maeneo hayo ili wapewe *(quota)* yao, sawa na tunavyowafanyia wanawake? Naunga mkono hoja hii.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam waliopo Wizarani, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa hotuba hii nzuri na yenye upeo wa kuthibitisha msingi sahihi ya uchumi wa maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania katika karne hii ya ishirini na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba hii 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelezwa kuwa dira na majukumu ya Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu inalenga kuiwezesha nchi yetu ifikapo mwaka 2025 kuwa nchi yenye misingi imara, wenye kuipa uwezo wa kuwa mshindani katika nyanja za sayansi na teknolojia miongoni mwa Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka dira na malengo kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, tuongeze nguvu katika kujenga uwezo mkubwa na wa Kimataifa kwa wataalamu wetu katika sekta za kilimo na viwandani pamoja na wataalam wengine na wasomi mbalimbali waliomo nchini ili tuweze kufikia malengo yetu haya tuliyojipangia hadi kufikia mwaka huo wa 2025 kwa mafanikio makubwa na kama yalivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama tutaimarisha wataalamu wetu vizuri na kuwapa uwezo wa kifedha na vifaa katika sekta hizi za viwanda na kilimo tutajenga Taifa kubwa na lenye maendeleo makubwa. Kwa hiyo, Serikali itoe fedha nyingi kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza dira na majukumu yake haya yaliyolengwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri sana Serikali yetu kujenga Chuo cha Kimataifa ambacho kitatuwezesha kuwaomba wataalamu wa Kimataifa wa fani

mbalimbali kutoka nchi marafiki kama vile China, Japan na Korea Kaskazini ili tuwe nao hapa nchini na kutoa elimu ya juu kwa wataalamu wetu mbalimbali ambao watateuliwa na Serikali yetu ili tuliwezeshe Taifa letu kuwa moja ya Taifa kbwa sio kwa Afrika tu hata duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina rasilimali nyingi sana kama madini ya aina mbalimbali na kadhalika hakuna sababu Taifa letu lisiwe katika moja ya Taifa kubwa hapa duniani. Tunao uhusiano mzuri na Mataifa na mashirika mbalimbali ya Kimataifa. Tuutumie uhusiano huu kujenga Taifa lenye nguvu duniani, kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Benjamin William Mkapa kualikwa katika kuhudhuria mkutano wa wakubwa wa dunia, *G8* ni faraja kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakubwa hawa *G8,* Marekani, Uingereza, Ujerumani, Japan, Italia, Canada, Ufaransa na Russia, kwa kweli hatuna budi kuzishukuru sana kwa kumthamini Mheshimiwa Rais wetu na kuwa pamoja naye kwa muda wote wa uongozi wake. Kwa kweli huu ndio muenzi wa Taifa letu kuliweka katikati ya *G8* hadi kufikia maendeleo makubwa ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia kama yalivyo Mataifa haya ya *G8.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa kuwa katika mwaka huu wa mwaka 2005/2006 wanafunzi wenye sifa za kuingia vyuo vikuu ni 22,992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza kidogo tu katika wanafunzi hawa 22,992 ni wangapi waliotoka Zanzibar. Kama hakuna ni sababu gani ambazo zimepelekea kutokuwepo wanafunzi kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumza kupitia hotuba hii ni juu ya suala la mafuta ya Zanzibar. Je, wataalam wetu nchini wanasemaje juu ya suala hili lipo au halipo? Nikinukuu gazeti la Nipashe la tarehe 24/1/2005 mafuta hayajathibitika kuwepo Zanzibar Wizara. Wizara ya Nishati na Madini imesisitiza kwamba bado haijathibitika kitaalamu kwamba mafuta yapo Visiwani Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelezwa kuwa taarifa zinazohusiana na ugunduzi wa petroli au gesi asilia katika eneo lolote la Muungano, zimewekwa bayana katika sheria za utafutaji na uzalishaji wa mafuta ya mwaka 1980. Kifungu 31(a) na 31(b) zinamtaka mwenye leseni ya kutafuta mafuta kutoa taarifa za kugunduliwa kwa mafuta kwa Kamishna na Waziri anayeshughulikia masuala ya petroli ambaye ndiye mwenye mamlaka kisheria kutangaza kuwa mafuta yamegunduliwa mahala fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa kampuni za BP na *Shell* ambazo kwa pamoja zilikusanya taarifa za kijiolojia na kijifiziokia na hatimaye kuchoronga visima viwili vya utafiti vya Zanzibar - 1 mwaka 1952 na Pemba - 5 mwaka 1961. Hata hivyo hayakugunduliwa mafuta ya petroli wala gesi asilia katika Visima hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na migongano inayojionyesha katika suala hili ndio maana nawaomba wataalmu wetu waliopo nchini kutueleza ukweli juu ya suala hili ili kuwaondolea wananchi wasiwe na mivutano inayojitokeza hapa nchini kwetu ambapo kwa asilimia fulani suala hili linachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu gazeti la Uhuru la tarehe 16/7/2003 ukurasa wa saba, liliandika habari kutoka Baraza la Wawakilishi. Serikali bado haijaridhia uchimbaji wa mafuta Visiwani. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na wataalam mbalimbali nchini, katika Kisiwa cha Pemba yapo mafuta mengi Vitongoji. Kwa upande wa Unguja ni Rasi ya Chwaka. Mafuta hayo yanaweza kabisa kutosheleza mahitaji ya matumizi ya ndani na kusafirishwa mengine nje ya nchi na kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu taarifa ya habari ya *Radio Tanzania* ya tarehe 24/6/2005 ya saa 7.00 mchana na saa 10.00 jioni ilisema kuwa Kamati Maalum iliyoundwa kushughulikia kero za Muungano imewasilisha ripoti yake. Miongoni mwa kero hizo ni suala la uchimbaji wa mafuta huko Pemba na Uvuvi katika Bahari Kuu.

Pia gazeti la Majira la tarehe 27/6/05 liliandika kuwa suala la mafuta kuingizwa katika mambo ya Muungano limeibuka tena katika mijadala ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huku zikiwepo habari njema za kupatikana kwa mafuta katika Kisiwa cha Pemba. Kwa mujibu wa wataalam wanaolishughulikia suala la mafuta yalionekana kuwepo katika Kisiwa hicho. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba ya bajeti ya Wizara yao.

Naomba kutoa ushauri ufuatao, Wizara itafute fedha ili kuongeza mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hili litaondoa tatizo la wanachuo kubebana katika mabweni yaliyopo hasa huko Mabibo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa nafasi za mabweni wanafunzi wa kike kutoka mikoani wapewe kipaumbele. Serikali iendelee kuwatafutia nyumba wanachuo ili kuwaepusha na tatizo la kujitafutia na kupanga mitaani. Tutawaepusha wanachuo na matatizo mengi ya mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyumba vya mihadhara viongezwe kulingana na idadi ya wanachuo. Tatizo la wanachuo kukaa chini au kusimama nje wakati wa mihadhara litafutiwe ufumbuzi. Chuo Kikuu Huria tawi la Kigoma. Kinahitaji jengo la chuo, vitabu vinahifadhiwa sakafuni. Hatuna viti hata *bench,* meza, sehemu ya kusomea na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezwe azma ya kuanzishwa kwa tawi hili bila matayarisho yoyote. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kukisaidia chuo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuendeleza sekta ya elimu ya juu, sayansi na masuala ya teknolojia ya sasa. Pili, navipongeza vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kwa kazi nzuri.

Pili, ningependa kuwashukuru Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu walionichagua mara mbili kuwakilisha Bunge hili katika Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)*. Kwa miaka karibu mitano niliyokuwa kwenye Baraza hilo nimepata uzoefu mkubwa ktika masuala ya elimu ya juu, hususani katika fani ya kilimo. Hata hivyo, ningependa kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haijatilia mkazo mkubwa katika kutenga bajeti ya kutosha ili kupanua elimu ya juu ili nchi hii iwe na wataalamu wa kutosha kupambana na dunia ya sasa ya ushindani wa kibiashara, utandawazi na mwelekeo wa regional intergretions kama *EAC, SADC, AU, NEPAD* na kadhalika. Tanzania bado iko nyuma kwa idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu katika kanda hii ya Afrika. Aidha, wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo hivi bado hailingani na wanafunzi wenye sifa za kuingia vyuo viku. Kwa mfano, *SUA* inadahili 40% ya wanafunzi wanaostahili na kuacha 60% ingawa wana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuongeza bajeti kwa vyuo vyetu na kuanzisha vyuo vingine. Aidha, kuna haja ya kutumia *unit cost* kama kigezo cha kutoa ruzuku kwa vyuo hivi. Hili limezungumziwa muda mrefu sana. Kwa upande wa *SUA* ningependa kusema kwamba tubadilishe mwelekeo ili pamoja na kuzalisha wataalam wa kilimo, ni lazima sasa tukazanie kuzalisha wakulima wataalamu wanaohitimu pale wawe na ari na motisha kwenda kuwa wakulima waataalamu vijijini, badala tu ya kwenda maofisini kama wataalamu wa kilimo na kubaki chuoni kufundisha. Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa katika mhadhara wake aliotoa pale *SUA* tarehe 12/4/2005 katika mhadhara wa kumi wa kumbukumbu ya Marehemu Edward Moringe Sokoine, alisisitiza hilo.

Sasa ili upate wahitimu wanaokubali, kupenda na kuthamini kilimo kiasi cha kwenda kuwa wakulima, lazima uwaandae mapema kabla ya kuingia Chuo kikuu. Ndiyo maana mimi bado nadhani mchepuo wa kilimo katika shule za sekondari ungeachwa ili uwe ndiyo *breeding ground* kwa wanafunzi watakao chaguliwa kuingia *SUA.* Wanafunzi wa aina hiyo, walioandaliwa mapema kupenda kilimo ndio hatimaye wanaweza kuwa wakulima wakitoka Chuo Kikuu. Lakini hatuwezi kutegemea wanafunzi waliojifunza kilimo kwa miaka minne tu Chuo Kikuu, wakapenda kilimo. Wengi wao wanataka tu kupata digrii, siyo kuzoea na kupenda kilimo.

**MWENYEKITI:** Sasa kulingana na muda wetu naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, aje atoe baadhi ya maelezo kuhusu hoja zetu za leo. Karibu sana Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Mkutano huu wa Bunge, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa msiba mzito wa Mheshimiwa Margareth Bwana.

Kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma tunatoa pole kwa familia, watoto, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu. Tunamwomba *Subhana Allahu Wataala* aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi. *Amin.*

Pili, ningependa kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na pia Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Niruhusu nimshukuru Mheshimiwa Balozi, Mheshimiwa Dr. Pius Yasebasi Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuwa mwalimu wangu na kiongozi bora katika utendaji wangu wa kazi.

Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wenu ambao mmenipa kwa kipindi chote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, mwanamama mahiri wa Kimasai, Wakurugenzi, Wakuu wa Vyuo, Makamu Wakuu wa Vyuo, Wataalam wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao wa karibu waliokuwa wakinipa mara kwa mara na bila ya kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawasahau Magili, Christina, Mnyalukolo, Mwamwesa ,dereva wangu, ambaye amekuwa na mimi wakati wote tukisafiri usiku na mchana. Mwisho lakini si kwa umuhimu wake, mume wangu, samboni, Dr. Mohamed Mhita, wanangu wapenzi, Mboni, Kimweri, Muhaji na Najma kwa ushirikiano wa hali ya juu walionipa kwa kipindi chote cha miaka mitano. Muda mrefu sikuwepo nyumbani, lakini walinielewa. Kwao nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hoja hii, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Esha Stima, alichangia katika hoja ya Waziri Mkuu, alizungumzia kuhusu Serikali isaidie wanafunzi wa Vyuo Vikuu kupata nafasi ya kufanya kazi za mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kufanya kazi za mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu uwekwe na vyuo vikuu husika vikishirikiana na Wizara inayohusika na aina ya mafunzo anayofanya mwanafunzi. Aidha, Serikali inatoa fedha za mafunzo kwa vitendo kwa wale wanafunzi wenye udhamini wa Serikali kwa ruzuku ya shilingi 6,000 kwa siku.

Mheshimiwa Beatus Magayane, naye alichangia katika hoja ya Waziri Mkuu na aliongelea kuhusu Serikali iboreshe elimu ili vijana wa Kitanzania waweze kushindana kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa ujumla vinajitahidi sana kuandaa mitaala yao ambayo inazingatia mahitaji ya soko huria, utandawazi, mabadiliko ya mfumo ya utendaji na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha, Wizara kupitia Baraza ya Elimu ya Juu imeendelea kuhimiza Vyuo Vikuu kuwa na mipango mikakati ambayo inalenga kuzingatia mabadiliko ya changamoto zinazotokea kutokana na maendeleo ya teknolojia na uchumi katika dunia.

Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuber, naye pia alichangia katika hoja ya Waziri Mkuu. Yeye anasema Serikali iimarishe mfumo wa elimu ya juu ili mitaala ilingane kwa Tanzania nzima yaani Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile elimu ya juu ni suala la Muungano, mitaala ya elimu ya juu kwa Tanzania nzima inasimamiwa na kuidhinishwa na vyombo viwili ambavyo ni Baraza la Elimu ya Juu na Baraza la Elimu ya Ufundi, hivyo hakuna tofauti yoyote katika mitaala ya elimu ya juu kwa Tanzania Bara na kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aridi Uledi, yeye alichangia kwa maandishi. Alizungumzia kuhusu ajira kwa wahitimu. Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwapangia ajira wahitimu wa Vyuo Vikuu. Utaratibu huo haukua endelevu. Ili kukabiliana na hali hiyo mpya, Vyuo vimechukua hatua zifuatazo kuhakikisha kuwa wahitimu wanaopata ajira, wanapata ajira kulingana na fani zao. Kuangalia na kupitia mara kwa mara mitaala ya vyuo ili iwe inakidhi mahitaji ya soko na kuanzisha masomo ambayo yanasukumwa na utashi wa soko na vile vile kumpa mwanafunzi stadi ambazo zitamwezesha kujiajiri.

Pili, kwa nyakati mbalimbali vyuo hufanya mapitio na wahitimu wake walio kazini na kujadiliana na waajiri ili kujua mapungufu ya wahitimu hao katika kutekeleza majukumu yao kazini.

Tatu, kuwapeleka wanafunzi katika sehemu mbalimbali kama vile mashambani, viwandani na maofisini ili kupata uzoefu wa fani husika. Nne, kuwapa wanafunzi stadi za ujasiriamali ili kuwapa mbinu za biashara na waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tano, kuanzisha vitengo vya kutoa ushauri wa ajira kwa wanafunzi kuhusu ajira zinazopatikana katika Taasisi husika.

Mheshimiwa Paul Kimiti, yeye alichangia kuhusu uanzishwaji wa vyuo vikuu binafsi. Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu linao utaratibu ulio wazi wa kudhibiti uanzishwaji wa vyuo vya elimu ya juu. Utaratibu huo na vigezo vyake vimeainishwa katika Kanuni zilizotolewa mwaka 2001 na umeelekeza wawekezaji, taratibu na hatua zote zinazotakiwa pamoja na hati zinazotolewa katika kila hatua hadi kufikia ithibati ya chuo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Elimu ya Juu huhakikisha kwamba wamiliki wa vyuo binafsi au wawekezaji wao wanao uwezo na mipango endelevu ya kuendesha vyuo kwa maslahi ya Watanzania na si kwa kutuma faida bila kutimiza malengo ya kutoa elimu ya juu. Vile vile aliuliza kuhusu uwezekano wa Serikali kuweka *quota* katika kuingia vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu unategemea mambo yafuatayo:-

Kwanza, uwezo wa mwanafunzi kitaaluma, pili, nafasi katika vyuo vyetu. Hivyo Serikali haina utaratibu wa kuanzisha *quota* kwa udahili katika vyuo vya elimu. Aidha, Serikali inawaomba na tunawasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusaidie kuhamasisha, kusimamia, kufuatilia, uboreshaji wa elimu katika Mikoa yetu. *(Makofi)*

Pia alikuwa na hoja ifuatayo, akauliza utaratibu gani unatumika kuwasaidia wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwapatia elimu. Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 iliyoanzisha Bodi ya Mkopo. Chini ya Sheria hii kila mwanafunzi mwenye udahili anastahili kuomba mkopo kugharamia elimu yake. Kila mwombaji wa mkopo mwenye udahili hupitishwa katika mchakato wa kutambua uwezo wake wa kiuchumi wa mwombaji ili kuwezesha kuamua kiwango cha mkopo atakachopata.

Pamoja na kuwa na taratibu ya uwezo wa kiuchumi wa mwombaji, Kanuni za kutekeleza Sheria ya Bodi ya Mikopo zinatoa kipaumbele kwa makundi yafuatayo ya wanafunzi wanaohitaji mikopo. Kwanza, mwombaji ambaye ni yatima anawekewa maanani. Mwombaji mwenye ulemavu, Mheshimiwa Margareth Mkanga, nadhani utafurahi hapo. *(Makofi)*

Mheshimiw Mwenyekiti, mwombaji toka familia yenye mzazi mmoja na toka makundi yaliyotwezwa, mwombaji wa kike anayechukua au anayatarajia kuchukua masomo ya sayansi, uhandisi na teknolojia.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, yeye alizungumzia kuhusu kujenga Chuo cha Kimataifa kitakachokuwa na wataalam wa Kimataifa wa fani mbalimbali, akatoa mfano, China, Japan na Korea Kaskazini.

Mheshimiwa kaka yangu, Omar Mjaka Ali, tumepokea ushauri wako wa kuwa na Chuo cha Kimataifa. Hata hivyo, tunapenda kukumbushana na ninamiini Mheshimiwa

Omar Mjaka Ali, unafahamu na Bunge lako Tukufu kuwa Vyuo vyetu Vikuu vina hadhi na vinatambulika Kimataifa. Aidha, vyuo hivi vinapokea wanafunzi na wataalam kutoka Mataifa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, pia alitaka kufahamu takwimu za wanafunzi wanaotoka kila Mkoa kuingia Vyuo Vikuu. Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, panahitajika muda kufanya uchambuzi kutoka vyuoni, pindi taarifa ya takwimu hizi zitakapopatikana tutakupatia kwa maandishi. Naamini unatuamini kwamba tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ndugu yangu Bernadine Ndaboine, yeye alikuwa na hoja nne. Ya kwanza kutoa nafasi za mabweni kwa wanafunzi wa kike. Nilijua utauliza hivyo, ukiwa Mbunge wa Viti Maalum ukiwakilisha wanawake wa Mkoa wa Kigoma na umekuwa ukifanya hivyo mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Bernadine Ndaboine na ningependa wanawake wa Mkoa wa Kigoma waelewe hivyo. Katika kuhakikisha wanafunzi wa kike wanapewa nafasi za bweni katika Vyuo Vikuu, Vyuo vyote nchini vimejiwekea taratibu za kuhakikisha kuwa wanafunzi wa kike wanapewa kipaumbele na kupewa nafasi za bweni katika hosteli za vyuo. Aidha, vyuo vikuu pia vimetoa vipaumbele kwa wanafunzi wenye ulemavu na wanafunzi wa kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, pia uliuliza kwamba Wizara itafute fedha ili kuongeza mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Serikali inatambua tatizo la ukosefu wa nafasi za mabweni kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ingependa kuhakikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinakuwa na mabweni ya kutosha. Hata hivyo Wizara hutenga fedha za maendeleo kulingana na Bajeti yake na kwa mwaka 2005/2006 Wizara imevitengea fedha Vyuo Vikuu vya Sokoine, shilingi bilioni 3 na Chuo cha Mzumbe bilioni 4 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa mabweni kwa vyuo vingine katika bajeti zitakazofuata. *(Makofi)*

Pamoja na juhudi za Serikali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeingia mkataba wa maelewano na mwekezaji kutoka Ardhi. Mwekezaji katika Ardhi ya Chuo ilionyesha nia ya kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi na wasichana watapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa na hoja ya kumbi za mihadhara ziongezwe. Mheshimiwa Bernadine Ndaboine hazungumzii mabweni peke yake anakwenda mpaka kuomba kumbi za mihadhara pia ziongezwe. Serikali imeendelea kutoa fedha za ujenzi kwa kumbi za mihadhara katika Vyuo Vikuu kupitia mfuko wa Elimu Tanzania. Vyuo Vikuu vya umma na vile vya binafsi vimepata ruzuku kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu vyuoni.

Vile vile ameendelea Mheshimiwa Bernadine Ndaboine katika mchango wake wa maandishi alitumia kurasa kama sita leo. Amezungumzia kuanzishwa kwa kituo cha Chuo Kikuu Huria cha Kigoma bila kuwa na matayarisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa hali ya jengo ya kituo cha Kigoma siyo nzuri. Jengo linalotumika ni la muda na lina vyumba viwili tu, kwa ajili ya Katibu Muhtasi na Mkurugenzi wa Kituo. Kwa hali hiyo hapawezi kuwepo nafasi ya kuweka viti, madawati au mabenchi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza. Kuhusu vitabu kuwekwa sakafuni, Mheshimiwa Mbunge alikuta vitabu vikiwa sakafuni. Ilikuwa tatizo la muda wakati wa kuhesabu mali ambapo vitabu hulazimika kutolewa makabatini. Si kama kawaida ya Kituo hicho kuweka vitabu sakafuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Bernadine Ndaboine wa kuitaka Serikali itoe majengo yasiyotumika huko Mikoani ili yatumiwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa lengo ya kupanua udahili na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hatua hii itakiwezesha Kituo cha Kigoma na vituo vingine kupata majengo yaliyo bora na yanayokidhi mahitaji. Tungeomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kwa hilo kuweza kutambua majengo ambayo yapo katika mikoa yetu na hayatumiki kikamilifu ili yaweze kutumika katika vituo vyetu vya Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aridi Uledi, pia alikuwa na hoja nyingine. Alikuwa anazungumzia kuhusu kuhimiza wanafunzi wachukue masomo ya sayansi na kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili kuhamasisha walimu na wanafunzi wachukue masomo ya sayansi. Aidha, Wizara imekuwa ikitoa tuzo kwa wasichana wanaofanya vizuri katika masomo haya na walimu wao kuanzia mwaka 2001. Kwa mwaka huu tumeanza kutoa zawadi kwa wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu vya umma na vyuo vikuu binafasi. Shughuli nzima ya kutoa tuzo mwaka huu ilionyesha vile vile katika kipindi cha Jarida Maridhawa kupitia kituo cha *television* cha *Star Television.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu pia imekuwa ikiwalipia karo wanafunzi hawa wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maria Watondoha, yeye alichangia katika hoja ya Waziri Mkuu na alizungumzia ufadhili wa wanafunzi vyuo vikuu na pia akasema Serikali itoe ufadhili kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita mwaka 2005 ili nao waweze kujiunga na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita mwaka 2005 ambao wana sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, ni 11,553 yaani hawa ni wenye kuanzia *point 4, point 5* kwenda juu na waliomaliza mwaka 2004 wenye sifa hizo ni 11,439. Aidha, vyuo vya elimu ya juu nchini vina uwezo wa kudahili wanafunzi 16,660. Serikali imebajeti kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wenye sifa ya kupata mkopo pamoja na waliomaliza kidato cha sita mwaka 2005 watakaopata udahili katika vyuo vikuu kwa mwaka wa masomo 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tayari vyuo vya elimu ya juu vinatoa *form* za udahili kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita mwaka 2005 na watakaodahiliwa watapata ufadhili kwa utaratibu wa Bodi ya Mikopo. Hata hivyo, kwa vile utaratibu wa mikopo ndiyo umeanza na fedha kutokidhi mahitaji yote, wazazi, walezi na wenye uwezo waendelee kuwekeza katika elimu kwa kuwadhamini wanafunzi ili wale wasio na uwezo waweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Shamim Khan, popote ulipo naamini utakuwa unatusikia saa hizi. Yeye alizungumzia kuhusu wanachama wa *TAS* hasa kwa akinamama. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Shamim Khan, kwa kupongeza uanzishwaji wa *Tanzania Academy of Sciencies,* mchango na maoni yake yamezingatiwa. *(Makofi)*

Aidha, uanachama wa *TAS* unazingatia zaidi mchango wa mtaalam binafsi wa Sayansi na Teknolojia katika jamii na maendeleo. Wito unatolewa kwa akinamama wenzangu, natoa wito kwa wote ambao mmetoa michango kwa jamii katika Sekta hii ya Sayansi na Teknolojia, mjitokeze ili mtambuliwe na kupewa vyeti. Naamini wako wengi popote mlipo mtakuwa mnanisikiliza akinamama, mfanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki kitaleta changamoto kwa kukuza mashirikiano na Taasisi za ndani na Taasisi za nje juu ya kuongeza uwezo wa wataalam wetu. Juhudi zaidi zitaelekezwa kwa akinamama na wasichana ili wajiunge na kutoa michango yao na wawe *roll models* kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Aidha, uhamasishaji utafanyika kupitia semina, makongamano, warsha na vyombo vya habari hasa kipindi cha Sayansi na Teknolojia kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shamim Khan, pia alitaka kujua tofauti kati ya *Course Take* na *TAS.* Tuanze na *Course Take* ni chombo kilichoanzishwa na Sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 1986. Majukumu yake yametajwa kisheria. Ina masharti ya ajira ya Serikali, inaendeshwa kikamilifu chini ya uongozi wa Serikali kwa watendaji na Kamati zilizoundwa kisheria. *TAS* ni chombo cha hiari kinachoendeshwa nje ya Serikali lakini kinapokea misaada toka Serikalini, sekta binafsi na kutoka kwa wafadhili. Kina watendaji wachache sana. Ujumbe wa chombo hiki ni kwa sifa binafsi za usomi na si kwa sifa nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki hakina umri wa kustaafu kwa mjumbe, kwani umri mkubwa ni wa manufaa kwa ajili ya uzoefu. Hakiendeshwi kwa bajeti ya Serikali, ni changamoto kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na utumiaji wake. Inatoa ushauri wa bure kwa vyombo vya Serikali na Sekta ya binafsi katika kuchangia maendeleo na utumiaji wa sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena namshukuru Mheshimiwa Waziri wangu kwa ushirikiano wake wa hali ya juu kabisa. Yeye binafsi pamoja na familia yake. Nitauthamini sana ushirikiano wake daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kunipatia nafasi hii tena kuweza kuhitimisha hoja ya Wizara yangu.

Napenda kwa sababu ya muda wenyewe hautoshelezi kujibu hoja zote, nikiri kwamba nimepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa kwa mchango wa kuzungumza humu ndani ya Bunge na vile vile kutoa maelezo kwa maandishi. Ningependa kuwatambua sasa Waheshimiwa Wabunge hawa ambao wametoa maelezo yao kwa maandishi na vile vile kwa hotuba.

Kwa hotuba ningependa kwanza nimtambue Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa uliyepo sasa Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Musa Lupatu na Mheshimiwa Dr. William Shija. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine na Mheshimiwa Zabein Mhita. Ningependa nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Kitine. *(Makofi)*

Napenda nitoe shukrani zangu tena kwa Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu wangu Ndugu Ruth Mollel na wataalam wote ambao nimewataja asubuhi ambao wako hapa na wengine wako juu kwa msaada wao mkubwa walionipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Dr.Hassy Kitine, amenichokoza na nadhani imekuwa makusudi nisisahau. Napenda kuchukua nafasi ya pekee hii kumshukuru mwanamke mmoja ambaye sikumtaja hapa asubuhi ambaye anaitwa Lucy Francis Ngalula Ng'wandu, binti wa Chifu Ngalula wa Misungwi ambaye amenienzi kwa miaka 25 yote nikiwa Bungeni, siiondoi ile miaka mingine lakini kwa sababu tunazungumza mambo ya Bunge na kuwa karibu na mimi na kunisaidia mpaka nikafikia hatua hii. Bila matunzo hayo nisingekuwa na ujasiri wa kusimama mbele yenu na kuweza kutetea hoja hii. *(Makofi)*

Napenda vilevile nitoe shukrani kwa watoto wangu ambao nimewalea mwenyewe, mmoja sasa yuko hapa Letisia Ng'wandu *number two* sio *number one, number one* anaitwa Doeres Mbuke Ng'wandu ndio *number one* ambaye namshukuru aliniuliza baba utamaliza lini kusoma na kila wakati ameniona nasoma mpaka sasa na yeye anasoma na hatujamaliza kusoma na *number three* anaitwa John Ng'wandu yupo Mwanza, wanne anaitwa Alex Masangu Ng'wandu yuko *DAWASA* na watano anaitwa Stella Matutina Nzambe Ng'wandu na mjukuu wangu mdogo anaitwa Yasebasi, acha mliyemwona hapa, huyo ambaye hamjamwona, wote nawashukuru sana. Nakushukuru Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, kwa kuhakikisha kwamba hawa siwasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nasema kwa heshima kubwa kabisa nimekiri kupokea ushauri wenu na tutaufanyia kazi na majibu tutayatoa kabla Waheshimiwa Wabunge hamjarudi nyumbani kwa sababu hakuna nafasi nyingine. wakati huu tumeyapata na majibu haya kwa kweli tumejitahidi kuyajibu na wataalamu wangu wameniandalia majibu yote yako hapa, yapo sawa kabisa hakuna hata moja ambalo halijajibiwa. Ila tu muda wenyewe sina na ni muda wa dakika thelathini na lengo lilikuwa ni kwamba siwezi kuwajibu wote ila tu kukiri tu kwamba nimepokea haya yote ambayo umetuelekeza kufanya, na mengi yao waliulizwa na Kamati ambayo ningependa kuishukuru kwa kazi yake nzuri walioifanya na tukajibu na tumeshawawekea majibu hayo tumeyaweka katika maandishi, yote tutaunganisha pamoja ili kwa faida la Bunge lako Tukufu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshuru Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa mchango wake binafsi na mchango wa Kamati ambao kwa kweli ninyi mliusikiliza hapa, umetosheleza kabisa na umesaidia kabisa kuboresha hoja yangu. Jibu langu ni kwamba yale yote aliyotuasa na yale ambayo ametushauri na kutuagiza tutayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu baadhi tu ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo nitachukua chache sana, labda nianze hii ya Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, inayosemwa mwishoni ndio inayokumbukwa kumbukwa zaidi kuhusu masuala ya udaktari, ameeleza vizuri sana na Sheria ya Vyuo Vikuu mliyoipitisha hapa pamoja na Sheria nyingine ambayo tutaileta hapa katika Bunge lako Tukufu. Italazimisha kwamba utambuzi wa *degree* hizo ufanywe kwa makini, lakini mtu ana uhuru wa kujipachika majina anayotaka kwa mfano, Profesa Miti Mirefu, Dr. Fulani, wale waganga wa kienyeji wanajiita huwezi kuwakataza, lakini kama anaombea kazi au umaarufu fulani lazima ithibati ifanye kazi, kwamba majina hayo yathibitiwe. Wazo la Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, lilikuwa zuri sana ambalo kwa kweli ni Sheria ambayo haijaandikwa katika nchi yetu lakini huwa inatekelezwa kwamba kila *thesis* au andiko ambalo linahitimisha kisomo cha udaktari, andiko lazima liwekwe katika *library. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani lazima liwekwe katika *Library of Congress* ndio ili ijulikane kwamba wewe umesoma *thesis* yangu inategemea kama unatoka Marekani utaita *thesis,* ukitoka Uingereza unaita *dissertation* yaani andiko la mwisho la *Ph.D* liko katika *Library of Congress.*

Nilipofanya *Ph.D* yangu *Stanford* lazima andiko liwekwe huko wewe ndio unaonekana umesoma. La maana na la msingi ni kwamba ufuate masharti na taratibu ya Vyuo Vikuu ambavyo vina ithibati, kama wewe umesoma kwenye vyuo ambavyo vina ithibati basi utambulike kule ulikotoka na huku hatuwezi kukutambua ndio utaratibu ambao tumejiwekea.

Kwa hiyo, tunatambua vyeti ambavyo vinatokana na vyuo vikuu vyenye ithibati yaani ambayo ni *accredited institutions in their own countries* unakotoka na sisi hapa *reciprocally,* tunatambua kwamba kweli umepata hiyo taaluma. Kwa hiyo, hili

tutalifanyia kazi na awamu inayokuja naishauri na inapokea na ushauri wa Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine kwamba tutakuwa makini kabisa katika kutambua madaktari hao.

Hata Marekani na Ulaya udaktari unao *rescuers* yaani udaktari waheshima. Kuna utaratibu uliowekwa na *charter* au Sheria iliyoweka chuo hicho ni wangapi ambao wanaweza kupewa udaktari waheshima. Sio wengi sana ni wachache sawasawa na *fellowships chartered* za *accountants, ACCA* kwa namna hiyo huwezi kuwa unaingia mpaka zitokee *vacancies* ndio unakarabishwa kuwa *fellow*. Kuwa daktari *honoris causa* lazima watu wakupendekeze, *senate* ya chuo hicho ikubali kama kweli wewe umetoa mchango wa maana katika nchi, katika dunia ambao unahusiana na chuo hicho ndio wakupatie hadhi hiyo ya *doctoris honoris causa,* walau hilo tumelizingatia.

La pili lilivyozungumzwa hapa siwezi kutaja majina sasa nani alisema nini kwa sababu nakumbuka ni nini kilisemwa. Mpango ambao utapokea mipango hii ya elimu ambayo ni mipango nyumbulifu ambayo inaungana kama mkufu toka MMEM kwenda MMES na kuingia katika elimu ya juu. Sisi kwa kweli tulikamilisha mipango yetu mapema hatukukaa tu, tulikuwa *pre-active,* si mmesema ukimgharamia msomi basi utafuata nyendo za msomi, hakai kungojea tatizo, analiona tatizo mbele anafanya hiyo kazi, tumefanya hiyo na kujuzu hapa hizi tatu hapa na naomba na zimo kwenye tovuti zetu tutaziona tatu, ya kwanza inasema *higher and technical sub master plan 2003/2018* imekamiliaka miaka mitatu iliyopita.

Ya pili inasema *science and technology sub master plan 2003/2018* kutekeleza mpango ambao umewekwa kwa vigezo vya kisayansi kwa kuangalia jinsi tunavyo plan mambo yetu ndio tumeutengeneza mpango huu. Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, unafahamu, sasa huu mpango huu kuutekeleza utahitaji dola za Kimarekani wala sihitaji kuzitafuta ziko kichwani, dola za kimarekani zisizopungua milioni 360 kutekeleza mpango kwa miaka 15 na umewekwa kwa vigezo na kwa kipengele, kwa kipengele na tumetumia wataalam wetu wa vyuo vikuu vyetu kuandaa mpango huu. *(Makofi)*

Sasa baada ya hapo tukaona kwamba je ili tusomeshe vijana wetu katika vyuo vikuu vyetu *unit cost* yake ni kiasi gani? Wataalam hao, hao hao na wengi naweza kuwatambua wako hapa namwona Tony Mbwete na wenzake ambapo ningechukua watu kutoka nje ingenigharimu fedha mamilioni, lakini nilitumia fedha ya kutosha tu ndio kuwalisha posho zao wakamaliza hiki kitabu kinaitwa *Method for Determination and Updating of Student Unit Cost in Higher Education Tuitions in Tanzania* na sio hivyo tu, tukaanza *a pilot project* katika sehemu mbili, vyuo vikuu viwili au *Institutions* mbili, ya kwanza Mzumbe na pili *DIT* ambapo tumejaribisha mpango huu wa kuweza kuandaa mambo yetu na kutekeleza mambo yetu kutumia *unit cost,* matokeo yake yametokea Serikali inayazingatia ili yaweze sasa kuenezwa katika vyuo vyote. Kwa hiyo, nina furaha kuonyesha kwamba kazi hiyo imefanywa, hatukukaa tu na kungoja. *(Makofi)*

Lingine ni hili la sheria zetu tunapotunga hapa Bungeni na sheria ambayo inatuhusu kwa mujibu wa hotuba yangu hapa ni ile sheria ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Tunapotunga sheria inafuatwa sasa sheria ndogo au kanuni za kuiwezesha sheria hiyo kutekelezeka. Huwezi kuanza na hizo sheria mpaka ipite kwanza Bungeni,

mabadiliko yatatokea unaweza kusema mbona hamkujiandaa kwanza kabla ya kuja Bungeni, huwezi kuanza kutunga sheria ndogo ndogo kwa mujibu wa uwezo mlionipatia kwa sheria hiyo, baada tu ya Rais kuidhinisha hii sheria na kuifanya iwe sheria ndio unaanza kuandika sheria, sheria ya utekelezaji ambayo sio ya ujumla jumla inaenda katika hatua ndogo ndogo si kazi rahisi.

Lazima ifanywe na wataalam wangu, imefanywa na *age chambers* na ninyi kwa kuniruhusu kusoma sheria nimeifanya mwenyewe kupitia hatua kwa hatua, na kuridhika kwamba inafaa na juzi nikaiwekea mkono kwamba hatua kwa hatua tumekamilisha ila vipengele kama viwili, vitatu, ambavyo nimewaambia kwamba hivi watavirudia rudia. Lakini hiyo haifanyi sheria isifanye kazi, sheria imekwishaanza kazi ya kuweza kutekeleza sheria ya mikopo na mmeona katika matangazo katika vyombo vya habari nadhani karibu vyombo vya habari kama magazeti sita wameshatangaza tayari utaratibu wa vijana wetu wa kuchukua fomu na kuweza kuomba mikopo hiyo, utaratibu huo unajieleza wenyewe upo wazi kabisa. Kwa hiyo, hilo siwezi kulikalia kwa muda mrefu sana.

Lingine ambalo limezungumzwa sana kwa makini yaani kwa haki kwamba limezungumziwa kwa makini na kwa haki yaani limezungumziwa kwa makini ni fedha inayotolewa katika sekta hii ya sayansi elimu ya juu na teknolojia. Tunajua fedha ni ndogo lakini afadhali fedha ni ndogo ingeweza hata kutokuwepo zamani haikuwepo, sasa ipo, kwa upande wa utafiti ilikuwa 300 milioni sasa ahueni ni milioni 600 tunaendelea na tunafanya utafiti kwa kutumia wataalamu wetu sisi wenyewe kuwaangalia, hivi kweli tunatumia kiasi gani kweli ni hizi tu milioni 600 zipo ni kwamba si kweli kuna milioni nyingi ambazo zinatumika ila tu *coordination* bado haijawa haijakamilika sawasawa.

Mimi nahakika tunatumia karibu ya nusu *percent* ya ile ambayo inatakiwa, lakini hatuwezi kufanya kazi kwa kisia ndio sababu nimeagiza utafiti ukamilike *and the re-commission of science and technology* inafanya hiyo kazi na itakamilisha. Nawaomba taasisi zote na Wizara zote tunaohusika na Wizara zote tutafanyia *research* mtupatie ushirikiano wa karibu tukamilishe utafiti wetu. Nafahamu kabisa Wizara ya Maji na Mifugo, juzi walifanya tamasha hapa Mpwapwa nadhani kwa miaka mia moja ya utafiti *the bovine studies* kuhusu *wizebu* ambao ameboreshwa na alikuwa anafikisha mia moja.

Mheshimiw Mwenyekiti, sasa utafiti huo ni muhimu sana, utafiti wa mbegu za katumani, utafiti za mbegu za tegemeo, utafiti mbalimbali wa zana za kujengea, kila Wizara inafanya utafiti. Je, kweli kabisa hatutumii fedha za nchi hii kwenye utafiti? Jibu ni kwamba tunatumia, tunataka tu kujua kwa uhakika natumia kiasi gani, tunaomba hazina tunaomba Wizara zote na mashirika yote watusaidie ili tuweze kukamilisha utafiti wetu mapema iwezekanavyo.

La mwisho, maana yake muda unakwenda, nataka tusitumie muda mwingi sana hapa, ambalo nalikumbuka vile vile ni kwamba kuna tatizo hili la wanafunzi ambao limetokea, limetokea kwa kweli kwa sababu ya maamuzi sio kwa sababu ya *local planning, plan* zetu ilikuwa ni kwamba wanafunzi wanakaa mwaka mmoja kabla hajaingia kwenye chuo.

Sasa maamuzi yakatolewa, maamuzi anayepiga sidhani kama unayapiga, sioni kama kuna mzazi hata mmoja anapiga watoto wake kwamba wasiwahi kwenda chuoni kwamba tuwawahishe watoto wetu kwenda katika vyuo vikuu yalikuwa ni maamuzi mazuri tu Serikali, na siwezi kusema kuwa yamefanya na Waziri wa Elimu, tulifanya Serikali wote pamoja. Lakini tukamtuma Waziri wa Elimu na Utamaduni akafanye maamuzi hayo, sasa maamuzi hayo yalihitaji maandalizi, ndiyo haya maandalizi tuliyofanya, Chuo Kikuu kishirki cha wapi *Dar es Salaam Teachers Colleges* inabadilishwa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vijana wetu wakitaka kusomea ualimu watapata nafasi kule, labda wakatae kwenda kule, Chuo Kikuu kishiriki cha Mkwawa watapata zaidi ya 2000-3000 kule tumeongeza nafasi au Chuo Kikuu cha Mtwara, Chuo ambata halafu kuna vyuo vingi tumevileta kama vile Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi na vyuo vingine ambavyo tumevileta na kama ilivyoelezwa, alivyowaeleza Naibu Waziri wangu hapa kwa kweli kuna matatizo aina mbili, uwezo wa vyuo vetu kuwachukua wanafunzi hawa hata kama wangekuwa na mamilioni kiasi gani ni ndogo tumetaja ni 16,000 uwezo.

Sasa la pili na uwezo wa bajeti, uwezo bajeti wala sio tatizo kubwa, tatizo ni uwezo wa vyuo vyetu kuchukua wanafunzi wetu hapa. Hatutaki wanafunzi wakajazane kule kama dagaa, wote mmezungumza juu ya hadhi na ubora wa elimu, elimu ya Chuo Kikuu inayotolewa lazima ifanane kabisa kama ya Chuo Kikuu. Kwa hiyo, kuandalia na maktaba, kuandalia vyumba vya mihadhara na mambo mengi na vyumba vya maabara. Hayo tunafanya nimeona kwenye bajeti yetu tumeombea, kwa utaratibu ambao tumeufanya na kwa kuzingatia kabisa mambo yote yale tumeona kwamba tuyachukue makundi wale ambao mmeshinda vizuri sana lazima tuaanze na hawa, tuchukue waende vyuo vikuu sasa watabakia 6,000 badala ya kubakia 10,000 na kitu inabakia 6,000. Sasa hawa 6,000 uzuri wa nyumba yako Tukufu inatoa ushauri mmetushauri na sisi tumekubali na tulikuwa na mpango wetu, mpango wa kuhakikisha wale 6,000 wanatawanywa katika vyuo vingi hapa nchini na nje lakini hasa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Wizara yangu na mimi mwenyewe tumeanza kuzungumza na Mabalozi na watu wa mashirika mbalimbali, na Mheshimiwa Bernard Membe alizungumza hapa tumezungumza na watu wa kutusaidia, tuanze programu ambayo unaweza kuita *marshall plan* au *the air lift plan* kuhakikisha watoto wetu hawa ambao wanauwezo hawa hawakwami katika shughuli za kwenda kusoma na sio hivyo tu sisi Serikali huwa tunazungumza na kushauriana, mmeshashauriana na Mheshimiwa Basil Mramba hapa ambaye ni Waziri wa Fedha tufanye nini katika hali hii.

Pamoja na kwamba tunaenda wengi, tunaenda kwenye majimbo yetu na kugombea tena, Serikali huwa inaendelea *in perpetuity.* Tuwepo sisi au tusiwepo Serikali ipo maana yake maamuzi yameshafanywa, kwa hiyo, nataka nimalizie kusema hivi katika suala hili la kurudisha na kupata msaada kutoka nchi za nje tutaupokea msaada huo, tutaainisha aina tatu, tutaupanga vizuri sana, tutapata kutoka kwa marafiki zetu ambao wanataka kutusaidia. Aina tatu za msaada ni:-

(i) *Full funded scholarships* yaani *scholarship* ambazo zinalipwa kikamilifu, wanatusaidia, hizi ni chache nataka kuonya hizi zitakuwa chache. Kwa hali ya sasa ya *globalization* hizi zitakuwa chache.

(ii) *Partially Funded* zile ambazo zimelipiwa nusu na Serikali ya kule ya wale marafiki zetu na nusu na sisi na zile *unfunded places.*

(iii) *Unfunded Scholarships* watuchukulie wanafunzi wetu ni kama watoto wao, kwa hiyo, tuzilipe hizo *capitation fees* ili tukawasomeshe watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalizungumzwa hapa ni mengi lakini niliona kwamba haya nisingeyajibu ningekuwa bado sijafanya kazi, nadhani nimeona yametosha haya ni wewe tu na heshima kuwashukuru ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nirudie tena kuwatakia heri na baraka na naona pindi mtakaporudi kwenye majimbo yenu Mungu awabariki wote mrudi katika nyumba hii na mtufanyie kazi tutakuja kuomba kazi hapa na mtupatie, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 1,590,470,900/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 191,184,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 694,067,600/=

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi *thesis* yangu ya *PhD* bahati nzuri iko *library.* Katika hiyo *Vote 68* programu ya 10 katika *sub vote* hiyo 1003 masuala ya Sera, Mheshimiwa Waziri hapa ametuonyesha vitabu na kimoja wapo kilikuwa ni kile kilichozungumzia masuala ya *Unit Cost* na mimi nakumbuka toka mwanzoni mwa miaka ya 1990 nilipokuwa *bursar* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulipoanza kushughulikia suala la *unit cost* mpaka sasa nafurahi kwamba imetoka kama Sera. Lakini na mimi nilipokuwa nikichangia kwa maandishi hapa nimeeleza umuhimu wa kutumia *unit cost* katika *fund* hizi *university.*

Sasa nilichotaka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri licha ya kwamba kuna kitabu hicho kizuri sasa *application* au Serikali itaanza kutumia *unit cost* kama *basis* ya kuweza kutoa fedha kwa vyuo vikuu ili kwa kweli elimu yetu ya vyuo vikuu ilingane na mahitaji halisi ya Vyuo Vikuu hivi.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema *unit cost* ndio inafanyiwa kazi katika *a pilot programme* ya Chuo Kikuu cha Mzumbe na *DIT.* Nimesema matokeo yake ndio Serikali sasa inayatathimini. Lakini la msingi ni kwamba Wizara imepokea ushauri huu na ushauri wenyewe ni ushauri wake yenyewe yaani ushauri wa Wizara yenyewe kwa sababu *unit cost* ilitokana na utafiti ambao tumefanya, lililobakia sasa ni uwezo wa Serikali kuweza kutoa bajeti ambayo inakidhi ama hitaji la *unit cost.* Mimi ninaimani kabisa jinsi tunavyokwenda hivi na maendeleo makubwa ya kiuchumi ambayo yamevuka asilimia sita ya Pato letu la Taifa linaongezeka, uchumi wetu unaongezeka basi na uwezo wetu wa kuhimili haya mahitaji utaongezeka ninayo imani kubwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba baada ya *pilot project* hii sasa baada ya tathmini, hatua inayofuata ni kutekeleza awamu kwa awamu hili suala la *unit cost* ili Serikali iweze kubeba mzigo huo kwa urahisi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001- *Unesco Commission* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...382,550,600/=
Kifungu 3001- *Higher Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...95,564,912,600/=
Kifungu 3002 - *Technical Education* ... ... ... ... ... ... ... . ... ... 9,936,457,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3003 - *Science and Technology* ... ... ... ... ... ... ... ... 2,753,806,200/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilipokuwa nikichangia nilizungumza katika hicho kifungu 3003, Sayansi na Teknolojia na nafikiri wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwemo ndani na ulinisikia nikitoa takwimu kuhusu nchi zilizoendelea zinatenga asilimia ngapi ya Pato la Taifa. Nimezungumza kwa kirefu na tunapozungumza na Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu tunaamini Serikali kwa ujumla wake inasikia akiwemo Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikwambie kwamba mwaka wa 1997 nilishamwandikia Mheshimiwa Rais katika masuala ya Sayansi na Teknolojia na alinijibu kwa maandishi kitu ambacho nikijua wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na Mbunge hawezi kusema uwongo adhibitiwe, kuna vyombo vya usalama na ulinzi kwa Mbunge anayetoa taarifa za uwongo ili asiingizie jina la Rais kwa sababu kanuni zinazuia.

Sasa nikazungumza kwamba hela zinazotolewa ni kidogo kwa hiyo, shilingi milioni 600 na Mheshimiwa Waziri akajibu kwamba tena angalau zinaongezeka, hii asilimia 600 ukiwauliza wataalamu wa Sayansi na Teknolojia, hata angeunganisha Wizara ya Kilimo na zingine ni asilimia 0.0006 sijui ngapi. Sasa kama kweli tunataka kuendesha sayansi na teknolojia, kwa sababu hata tukilima mazao kwa ajili ya kutengeneza dawa wengine watatengeneza *scientific* na nini sasa tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie na Serikali na Waziri wa Fedha yuko hapa, ni lini wataliangalia suala hili kwamba sio suala la mzaa,wafuate Sera wameiweka mwaka 1996, kwamba tunataka kutenga asilimia moja ya bajeti ya Taifa ya Pato la Taifa ili iende kwenye Sayansi na Teknolojia, ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie kwa sababu na Mheshimiwa Rais anajua suala hili kwa sababu alikuwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nafurahi sana kwamba kwa miaka mitano amefuatilia suala hili, suala la Sayansi na Teknolojia ni suala muhimu sio la kufanyia mzaha, asingekuwa analiingiza la mzaha halipo kabisa juu ya mzaha wowote, ni ufukara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimshauri Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, asome kitabu cha Profesa Mshigeni, *The Cost of Being poor* ambapo malighafi zetu, kwa mfano uyoga wa aina fulani unaenda Ulaya unatajirisha wengine na sisi tunabakia maskini, sasa ndio tatizo letu hapa ni ufukara wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu mimi situkuzi ufukara, ushauri ni kwamba awe na subira Serikali kwa miaka yote imesikia ndio sababu ikaongeza, pale unapoona kwamba kuna mabadiliko ya kwenda juu, kwa nini usifikie? Nimefikia kwa sababu hiyo kwamba walau zile juhudi zetu, zako wewe, za Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na zangu na za Kamati na za nchi, walau zimepiga hatua. Kwanza hii ni haki yetu kusema kwamba walau Serikali imesikia kwamba Serikali inaweza kupiga hatua, mimi nina hakika kabisa kwamba hatua zitachukuliwa kuweza kurekebisha hili.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri lakini sijaridhika, mimi sioni kama kukiri udhaifu wako kwamba ni dhambi, kukiri udhaifu wako ni hatua ya ushujaa na ndio nguvu zako. Kwa sababu tunachozungumza hapa milioni 300 na milioni 600 kwa Sayansi na Teknolojia tukijua kwamba dunia hii ni ya Sayansi na Teknolojia kama tunavyoimba, mimi angekiri tu kwamba tumelisikia, tutalifanyia kazi siyo kuniambia tumeongeza shilingi milioni 300. Kwa kweli hapo nadhani Mheshimiwa Waziri hawatendei haki Watanzania wanaotusikiliza, akiri tu kwamba tumelisikia, tunaenda kulifanyia kazi kuliko kusema tumeongeza shilingi milioni 300.

**MWENYEKITI:** Mimi kama Mwenyekiti nimesikia kwamba ni ufukara wetu na kwa kweli kuna udhaifu ambao tunao. Lakini tulifanyia kazi na tuwe na matumaini hayo kwamba huko siku za usoni tutapiga hatua, ndivyo alivyosema nilikuwa namsikiliza, sasa sijui angesema namna gani zaidi ya hapo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi*

*bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ...256,000,000/=

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya dunia ni Sayansi na Teknolojia na baadhi ya matukio yanayotokea duniani mengine vile vile yanaweza kusababishwa na hali ya kisayansi ilivyo. Sasa hivi siku za karibuni yameanza kusikika maneno kwa baadhi ya wanasiasa ambayo mimi nadhani watakuwa hawaelewi, lakini mimi nataka *clarification* kutoka kwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia.

Kwa mfano, mtu anaposema yeye atapata ushindi wa kishindo wa *Tsunami* maana yake nini? Kwa sababu *Tsunami* ni tukio lililotokea, baya sana huko Asia, ni baya halina sifa, limeuwa. Sasa kushinda katika uchaguzi ni kitendo cha sifa, cha ushujaa wa kisiasa sasa mimi nataka *clarification* kwa Waziri wa Sayansi kwamba je, maneno haya ni ya busara kweli kutumika? *Sorry,* yanatufedhehesha.

**MWENYEKITI:** .Nilikuwa najaribu kumwangalia Waziri mmoja hayupo, basi Mheshimiwa endelea kujibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tsunami* ni matukio yanayoleta gharika, yanaleta matetemeshi ndani ya Bahari, ni tukio hilo linaweza kutoleta maafa likakomea huko huko ndani ya Bahari. Lakini kwa kawaida linaleta maafa, watu wanaumia yaani wanaolitumia ni kwamba ile *scale* ya tukio ni kubwa sana inakuwa kama kwa kiingereza wanaita *metaphor* ni mfananisho wanatoa kama mfano wa kwamba tukio la ghafla, kubwa kabisa ndivyo watakavyoshinda. Kama tafsiri ndio hiyo mimi sioni tatizo lolote kisayansi. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tuna maneno ya busara na ya hekima ambayo tunaweza kuendelea kuyatumia katika mambo yetu. Hasa tukizingatia kukomaa kwa nchi yetu, sasa jambo kama la kimbunga cha *Tsunami* ni tukio ambalo limevuma siku hizi baada ya tukio la kuuwa watu. Kwa hiyo, bado mimi nataka kusema kwamba hata maelezo ya Waziri mwenyewe kwa *percent* kubwa si jambo la kuleta matukio mazuri, lakini sifa yake ni nguvu hiyo ya kimbunga, lina maana gani kutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi nafikiri si jambo zuri kulitumia neno hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Najua kwamba matukio ya mabadiliko ya tabia ya nchi ni suala la mazingira. Lakini pia niseme katika kusoma nimegundua kwamba neno *Tsunami* maana yake ni tetemeko la ardhi linalotokea chini ya Bahari. Sasa kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu, linapotumika kwa wale tunaotegemea kwenda kuomba kuwatumikia Watanzania kupitia ridhaa ya wapiga kura tunajipa matumaini kwamba ushindi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu lazima uishi kwa matumaini, tunajipa matumaini kwamba ushindi wetu hasa wale tunaotokana na Chama cha Mapinduzi ambacho mimi ni mwanachama wake. Tukio la ushindi wetu itakuwa kama tetemeko chini ya bahari inayosababisha mawimbi makubwa sana na hayo mawimbi sijui yataelekea wapi, lakini nahakika najifahamu, nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha yoyote ile ina tabia ya kulipamba jambo kwa kutumia lugha inayoficha karaha. Sisi tungeweza kusema, kwa mfano tutawamaliza safari hii wapinzani, lakini badala ya kusema maneno makavu namna hiyo kwa nini tusitumie neno gharika, kwamba watapata tetemeko kubwa linalofanana na lile la *Tsunami* na hivyo kuwaweka roho juu na ni maneno tu ya lugha, mimi nafikiri tusipate taabu na hili. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya ameridhika na sisi tunataka iwe hivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote )*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 2,200,000,000/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua katika kifungu hiki cha 1003 *Policy and Planning,* kwamba kwa uzoefu tulioupata katika shule za msingi ambako walimu wengine kutoka kidato cha sita watafundishwa kwa wiki tatu au miezi mitatu, kwamba sasa kama tunavyoelekea najua wakati haujafika kwa ajili ya mpango ule wa vyuo vikuu tukishakuwa na wanafunzi wengi wakiingia pale ma- *lecturers* wao na wao wataufundisha kwa miezi sita au inabidi tuwaandae huku kabla hatujafikia kule wakati kuna miaka miwili, mitatu ijayo ili tuweze sasa kuwa na kitu ambacho kinafanyika, sasa pale sikupata majibu, naomba majibu.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale mwanzoni nilipoanza kujibu kwamba nisingeweza kusoma majibu yote ambayo yameandaliwa lakini swali hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja tunayo majibu yake. Sera yetu sasa hivi katika vyuo vikuu vyetu wala hatungojei hiyo tsunami ya kutoka MMEM na MMES, tumepanga kwamba tutarudisha utaratibu wa zamani wa *staff development* yaani maendeleo ya utumishi katika kila chuo

na ile kada ya *tutorial assistant* inarudi ambapo wanachuo wanamaliza, wanapokelewa kwenye chuo halafu wanafundishwa pale kuwa Walimu. Kwa hiyo, hilo ni mkakati au mchakato wa aina moja. Wa pili ni makusudi kabisa kuongeza uajiri wa walimu waweze kutumikia wimbi hili ambalo linakuja la wanafunzi wengi ambao watafikia kama tulivyo sema zaidi ya wanafunzi 125,000 katika vyuo vikuu vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi tulikuwa tunazungumza tutatumia vile vile mbinu zingine kama vile *Distance Learning,* tuna Chuo Kikuu Huria na vyuo vikuu vingine vyote tutavibadilisha viweze kuwa na *TEKNOHAMA* yaani Teknolojia ya Mawasiliano, waweze kuwafundisha Walimu kwa *Distance Learning.* Wengine wakiwa kazini, wengine wakiwa kwenye makazi yao na ndiyo maana kwa ushauri wangu ambao nilidhani Wabunge mngeutoa lakini kwa sababu mimi naondoka nataka nishauri Serikali na Wabunge kuna mali zetu ambazo zinakaa *idle* ambazo zinaleta hasara wakati mwingine, pengine wakati huu inaweza kuonekana hazileti hasara, nimeziona kule Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile nyumba za Mamlaka ya Korosho zile, zikitumika vizuri inaweza kuwa Chuo Kikuu kikapanuka vizuri kabisa chuo chetu cha *Open University* na tunaweza kuangalia katika sehemu zote hapa Dodoma, nilikuwa namtegemea labda rafiki yangu Mheshimiwa John Malecela, aliangalie lile jumba la Chimwaga kama linatumika vizuri au namna gani na nyumba hizi mnazoziita za Magufuli zilizokaa pale mziache zioze hivi hivi, zitumike kwa pamoja, pamoja na jumba hilo kupanua Chuo Kikuu Huria. Tujipatie miaka kumi kwamba tuwe na wanafunzi katika Chuo Kikuu Huria wanafunzi wasiopungua 100,000 na walimu wapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi juzi nilikuwa Cuba, Cuba wana mpango wa kimapinduzi kila *secondary school,* imejengwa vizuri sana baada ya saa nane kila *secondary school* ni Chuo Kikuu. Ndiyo sababu ni Taifa la pekee katika dunia ambayo ina *Universal Higher Education* ni Cuba. Mambo haya yanaweza kuzingatiwa.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri na nampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya, lile jengo la Chimwaga lilikuwa ni jengo la chama na tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi, chama kikaliuza jengo lile kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi kutafuta watu wa kuweza kulitumia na nakumbuka safari moja wamisheni wa KKKT walijaribu kulichukua ingawa Askofu wa hapa alipata uwezo, aliruhusiwa achukue lakini wenzake hawakumuunga mkono kwamba kiwe Chuo Kikuu. Ninachotaka kusema ni kwamba, kazi ya jengo lile litumikeje imo mikononi mwa Serikali, si Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote )*

Kifungu 3001 - *Higher Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 22,794,451,700/=

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hilo 3001, kifungi kidogo 4398, nilipokuwa nachangia nilizungumzia kwa uchungu mkubwa sana Chuo Kikuu Huria, ukiangalia fedha zilizotengwa kwa maendeleo na ukilinganisha na Vyuo vingine mimi nafikiri kama hii ni dhihaka kwa chuo hiki. Majengo yanayotakiwa kulipiwa kwa mfano jengo la Mbeya, jengo la Mwanza hayo tukijumlisha ni karibu milioni 600 au 800. Leo ukiwapa milioni 100 unamtaka huyu Makamu ya Mkuu wa Chuo afanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hapa kwamba huko Kigoma Mbunge mmoja aliingia katika ofisi au Chuo chetu, aliyoyakuta pale ametueleza yametetewa tetewa lakini kwa kweli Waziri amejitahidi tu kujibu lakini ukweli uliopo ni kwamba huduma zilizopo pale majengo yaliyoko pale hayastahili kuitwa Chuo Kikuu.

Sasa tunapofika tumetenga milioni 100 sasa labda Waziri wa Fedha atuambie na pengine hili niombe tutasamehewa haya madeni siyo vizuri kusamehewa samehewa. Lakini litolewe kauli hapa hiki Chuo Kikuu Huria sikutania kusema hili ni kokoro lakini naamini wengi wasio na uwezo watapita huko. Kwa hiyo, tunaomba basi Serikali ikipe uwezo. Waziri atueleze tutapataje hela kwa ajili ya maeneo haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Fedha hana majibu ya kifedha basi sitatoa majibu ya kifedha, nitatoa majibu ya kisera. Ni kwamba Chuo Kikuu Huria ambacho Mheshimiwa Henry Shekiffu ni mjumbe wa bodi yake, kimeanzisha mpango wa chuo chenyewe, *strategic plan* kifanye nini kutafuta fedha yake yenyewe na maendeleo katika nchi nzima na mpango huo utakapokamilika utawasilishwa katika Serikali ambayo Serikali itahitaji kuhudumia na mwingine utahudumiwa na chuo chenyewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Henry Shekiffu awe na subira tu asikilize au ashughulike na uwe mpango wa chuo chenyewe ambao umeanzishwa tangu Profesa Tolly S.A. Mbwette ameingia pale ambao ni *Strategic Institution Plan* ambayo ni pamoja na kuendeleza chuo katika nchi nzima.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani mimi kwa kweli sikubaliani na Waziri, mpango mkakati uliowekwa ni mpango ambao unahitaji kwanza msingi wa kuufanya huo mpango wenyewe. Kwa hiyo, matawi ya chuo hiki kikuu yapo, sasa tukisubiri mpango mkakati kila chuo hapa kina mpango mkakati. Lakini hiki Chuo kimeshaanzishwa na kinahitajika kiendelezwe angalau Serikali ingeonyesha *seriousness* au vinginevyo basi ni vizuri chuo hiki kisingepanuka kiambiwe ubaki Dar es Salaam na malengo yake yabadilike kabisa badala ya kuwa Chuo Kikuu Huria kinachohitaji kudahiri wanafunzi 21,000 basi kiambiwe tu kidahiri wanafunzi 1000 kama vyuo vingine. Kwa hiyo, malengo yake yatatimilika Waziri atamke wazi hivi kwa kweli tatizo liko wapi kama vyuo vingine vinatengewe bilioni 4 au bilioni 250 hiki chuo chenye wanafunzi 21,000 inatengewe milioni 100?

**MWENYEKITI:** Mimi nimekaa hapa naongoza kama Mwenyekiti, kwa hiyo, nikitaja mtu, mtu asinifanyie mkono hivi. Mimi nataka Serikali ijibu Wabunge kwa hiyo, sitaki tena kuona mikono mtu anasema huyu hapana, hatuwezi Serikali ni moja.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sielewi kwa nini Mbunge hanielewi ninavyosema. Mimi kwanza siridhiki na Baraza lake hawaridhiki kwamba twaweze kudahili wanafunzi 20,000 tu, haitoshi. Nimesema tudahili wanafunzi hata 100,000. Lete mpango Serikalini ili uweze kuwa *funded* ndivyo hivyo ninavyosema, *bring a fundable project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo gani hapo? Nasema Serikali haikukataa kutoa *funding.* Ni kwamba hakuna mpango ambao ni *fundable* lazima uletwe mpango na chuo chenyewe ndio maana chuo kinakuwa na Baraza lake linalojitegemea. Serikali haiwafanyii mipango, vyuo vyenyewe vinajitegemea vina *charter* zake na ina sheria yake, walete mpango Serikalini wao watapata fedha kiasi gani kutoka wapi? Na sisi Serikalini ni wajibu wetu kutafuta fedha hizo. Tufanane na wenzetu *South Africa (UNISA).* Pale leo katika chuo hicho wanafunzi wanatoka laki moja kila mwaka. Leo sitajivunia na 20,000 tunababaika na 20,000 kwa sababu gani? Leta mpango na ninasema Profesa Tolly Mbwette, mtaalam wetu hapa na wenzake na kwenye Kamati hiyo wamekwishaanza utaratibu wa kuweka mpango huo na nimeona ule mwanzo wake, lakini huu mpango lazima tuuze tuweze kupata fedha.

Naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kwamba tuendelee na shughuli. Hizi milioni 100 ziwe kama fedha za mbegu *(seed money)* kwa ajili ya kutekeleza mpango huo. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu tena kuuliza. Wakati nachangia katika lile Fungu 3001 aya *Higher Education* lakini kifungu cha 4381 ukurasa wa 113. Nilizungumza kwamba *Mwalimu Nyerere Memorial Academy* wametengewa milioni 100 na wakati ule tunapitisha wote hapa tukiwa tunafurahi tuliiambia Serikali kabisa kwamba katika Bajeti hii kwa heshima ya Mwalimu Nyerere watenge hela za kutosha kukarabati yale majengo kwa sababu ni machafu lakini nilieleza *concern* yangu kwamba wakati wanawapa milioni 100 Wizara ya Sayansi na Teknolojia ukiangalia kitabu cha II, fungu la 310500 wametenga shilingi milioni 140 kununua magari mawili pale Wizarani wala siyo ya Waziri wala siyo ya nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikasema haki iko wapi magari mawili milioni 140 wakati hapa tunawapa milioni 100 nikataka maelezo kwa nini tunafanya hivyo maana yake Chuo hiki kinaweza kupelekewa wanafunzi 300. Sasa unachukua magari mawili pale Dar es Salaam sijua ni Mhasibu sijui ni nani? Sasa nikataka maelezo sikupata maelezo kwa nini Serikali imefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuchelewesha kikao chako, ninamsubiri Waziri wa Fedha kwa sababu nilimwambia wakati ule kwenye Bajeti yake atupe *circular* ni magari ya aina gani watumishi wa Serikali lazima waendeshe na kwa hela ngapi? Hakutoa jibu, sasa namsubiri kule kwake. Lakini kwa hili nataka maelezo hapa. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini kwanza hiyo imeshapita kwenye ile ya kwanza ile. Lakini kama Waziri ana maelezo basi atoe maelezo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo utaratibu wa Bajeti Waziri wa Fedha kuja kuulizwa maswali hapa. Siyo utaratibu kabisa ndio maana nimekataa kujibu kwa sababu hela nikishagawa mimi, mimi ni mpakuaji tu nimeshapakua. Sasa kila nyumba inajua jinsi ya kuwapa watoto wake, sasa siwezi kuulizwa tena wewe mzee ulinunua chakula na huku umekwishapakua sasa vipi mjukuu fulani hajashiba, siyo utaratibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maelezo ya Mheshimiwa Henry Shekiffu amesharidhika wapeleke mpango. Maelezo haya yametosha. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Technical Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,194,625,000/=
Kifungu 3003 - *Science and Technology* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 500,000.000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Baada ya hayo nina tangazo moja, kuna Waheshimiwa Wabunge walipewa *questionaire* kutoka *UNDP* sasa walijaza zile fomu na kama wamemaliza tunaomba sana wazirejeshe pale kwa *receptionist* wetu yuko pale karibu na

*pigeon holes* zetu, mkabidhi yule binti pale leo, kesho au kesho kutwa, zinatakiwa tunaomba sana. Tumefanya kazi njema tunaomba muwarudishie wanazihitaji. Wote tunajua kama kesho ni sikukuu kwa hiyo, Bunge halitakuwepo. Sasa nitaahirisha Bunge mpaka Siku ya Ijumaa saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.21 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 8 Julai, 2005 saa tatu asubuhi)*